# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 10 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha, 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2013/2014.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya a Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA-NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali yetu leo tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, atauliza swali la kwanza kwa leo.

Na. 179

### Ujenzi wa Kituo cha Afya Shelui.

**MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2010 Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Kata ya Shelui kuwa Serikali itajenga kituo cha Afya Kata ya Shelui na kwa sababu hiyo wananchi wameanza kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi huo:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha Afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kujenga vituo vya huduma za afya ni la kila Halmashauri husika.

Katika kutekeleza jukumu hilo Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa kushirikiana na wananchi imeanza ujenzi wa kituo cha Afya cha Shelui ujenzi upo katika hatua za awali za maandalizi ya kiwanja kwa ajili ya kuanza kuchimba misingi ya majengo. Ujenzi huu unatekelezwa kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya rasilimali vikiwemo wananchi ambao wamechangia shilingi milioni 2.0 pamoja na tofali 700.

Aidha, Halmashauri kupitia mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo, imetenga kiasi cha shilingi milioni 2.5 kuunga mkono michango ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa umma, Halmashauri itaendelea kushirikiana na wananchi katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu unakamilika kwa wakati na wananchi wananufaika kama inavyotarajiwa.

Aidha, Halmashauri iweke katika Bajeti yake ya mwaka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho. *(Makofi)*

Na. 180

**Jimbo la Mwibara Kuwa Wilaya**

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA** aliuliza:-

Jimbo la Mwibara lilianzishwa mwaka 1995 na kufikia sasa lina umri wa miaka 17.

Je, ni lini Jimbo hili litakuwa Wilaya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 2(2), Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye pekee mwenye mamlaka ya kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Mikoa na Wilaya na maeneo mengine kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria na taratibu za uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya Mwaka 1994.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vigezo mbalimbali vinavyozingatiwa katika kuanzisha Wilaya mpya ambayo ni pamoja na ukubwa wa eneo la Wilaya mpya na ya zamani usiopungua kilomita za mraba 5000, idadi ya watu wa Wilaya mpya na ya zamani wasiopungua 250,000 mpaka 300000, idadi ya Tarafa kwa Wilaya mpya na ya zamani zisizopungua

tano, idadi ya Kata kwa Wilaya mpya na ya zamani zisizopungua 15, idadi ya vijiji kwa Wilaya mpya na ya zamani visizyopungua hamsini na wananchi kuwa tayari kuchangia uanzishwaji wa Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Mheshimiwa Mbunge ameona Jimbo lake linakidhi vigezo hivyo, anashauriwa kupeleka maombi kupitia Baraza la Madiwani ambalo likishapitisha hupelekwa kwenye Kamati ya ushauri ya Wilaya *DCC* na Kamati ya ushauri ya Mkoa *RCC* na hatimaye mamlaka ya uanzishwaji wa maeneo hayo itashauriwa kwa ajili ya uamuzi wa mwisho. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasikitika kabisa kutopata majibu kuhusiana na swali langu na Wanamwibara.

Kwa kuwa, majibu ya msingi yanasema kuna vigezo vya ukubwa wa eneo, Idadi ya watu, idadi ya Tarafa, Kata na Vijiji. Kwa kuwa, sisi tuliiuliza Serikali yenyewe ituangalie katika vigezo hivyo wanavyotuambia leo, ili watuambie kwamba kwa vigezo walivyonavyo hivyo, Mwibara tunastahili kuwa Wilaya au hapana, matokeo yake sentensi ya mwisho anatuuliza tena kwamba endapo Mbunge anaona, sasa ni vipi tena swali linajibiwa na swali tena?

Tunataka atuambie kwa vigezo hivyo anavyovisema sisi Wanamwibara tunafaa au hatufai kwa sababu vigezo anavyo yeye, hilo ni swali la kwanza.

Lakini swali la pili, vigezo hivyo anavyovisema vya ukubwa wa eneo tunashuhudia Mikoa inatengwa ikiwa haikidhi viwango vya ukubwa wa eneo, tunashuhudia Wilaya zinatengwa zikiwa hazikidhi viwango vya idadi ya watu na hata hivyo, kuna kijiji kimoja utakikuta kwa mfano Ukerewe Nkirizya ni Kijiji kimoja, utakuta Kata ya Neruma Kama moja ina vijiji saba, sasa katika masuala haya ya kusema tuangalie Tarafa wakati hivi vinawekwa kisiasa, haoni kwamba vigezo

hivi vimepitwa na wakati, wana Mwibara tunataka Wilaya yetu kwa sababu ziko Wilaya ambazo sisi tunazizidi ukubwa na idadi ya watu?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Lugola, Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Ndugu yangu Lugola maswali yake mawili ya nyongeza akitaka yawe matatu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Serikali imeeleza utaratibu unaotakiwa kufuatwa, nilitegemea Mbunge aseme sisi Mwibara kwenye kikao chetu cha *DCC* cha tarehe fulani tulipendekeza hivi na Mkoa ukapendekeza hivi.

Je, mambo yetu yamekwama wapi? Nadhani lingekuwa swali hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hapa Bungeni hatupati Wilaya hapa ndani ya Bunge, Wilaya inaanzia na vikao kule Wilayani na Mkoani. Halafu tumesema Wizara husika kwa maana ya TAMISEMI inamshauri sasa Rais kwamba tumepitia muhtasari wa Mwibara, tumepitia muhtasari wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mara tunadhani kwamba vigezo hivi vinafaa. Pale mwenye madaraka sasa anaamua kutoa Wilaya au kutokutoa Wilaya. Hapa Bungeni ni mahali pa kupokelea taarifa kwamba Wilaya mpya imeanza, siko kunakozaliwa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili amesema ziko Wilaya maeneo yake madogo, Kata nyingine ina Kijiji kimoja tu, Hivi vigezo tulivyoweka havifuatwi kama msaafu. Kuna maeneo mengine ni *exceptional*, tumezungumza hapa habari ya watu mpaka laki tatu. Mafia wamepewa Wilaya hawafiki laki mbili, Pangani wamepewa Wilaya kwa sababu ya kijiografia. Sasa vijiji vingine unavyosema sijafika Ukerewe nimeishia tu pale Mjini. Huko vijijini inawezekana kabisa Kijiji kikapewa Kata kutokana na Jiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichoeleza hapa ni vigezo na nataka nikubalie ndugu yangu Lugola kwamba yapo mazingira ambayo watu hupewa Wilaya wakiwa pungufu, yako mazingira ambayo Kata hupatikana ikiwa ni ya kijiji kimoja tu. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Pamoja na sababu za kimsingi za kuweza kuwasogezea maendeleo wananchi ni kuwapa utawala ambao utaweza kuwasaidia. Lakini sambamba na hilo ni vema ikawepo bajeti ya kuweza kuhudumia maeneo hayo.

Uzoefu tulioupata katika Bunge hili kila Waziri akijibu anasema kwamba fedha zinakuwa chache kwa sababu tuna Wilaya mpya na hiyo Wilaya mpya itakuwa imepewa pesa kidogo sana.

Je, hatuoni Serikali inapotoa vigezo hivi, viangalie vilevile na uwezo wa Serikali wa kuweza kuongeza *administration* ambayo itakuwa na manufaa kwa wananchi badala ya kugawa tu bila ya kuangalia suala zima la kiuchumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa anatoa ushauri kwamba tunapoanzisha Wilaya tuzingatie na kigezo cha upatikanaji wa fedha za kuweka miundombinu ya kuifanya Wilaya ile kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa niaba ya Serikali nataka nikubali ushauri wake kwa sababu katika kuanzisha hizi Wilaya mpya tumepata matatizo ambayo yanasababisha wakati mwingine Kituo cha Polisi kiko Wilaya Mama, Mahakama iko Wilaya Mama, Mahabusu inabidi wapelekwe Wilaya nyingine waje wasikilize kesi warudishwe. Kwa hiyo, kigezo cha fedha ushauri wake tunaupokea. *(Makofi)*

Lakini nataka niseme kwamba mara nyingi tumejenga Sekondari za Kata hapa, unaanza kumwandaa mwalimu au unaanza kuianzisha shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachofanya tunaanzisha Wilaya basi na hayo mengine yakawa yanafuata. Kwa kweli wananchi maeneo mengi sana wanashiriki katika kazi za kujenga Taifa ili mradi wamepata Wilaya yao. *(Makofi)*

Na. 181

**Wafugaji Wahamiaji Kuwasumbua Wananchi - Korogwe**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI (K.n.y. MHE. YUSUPH A. NASSIR)** aliuliza:-

Wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe hususan Kata za *Old Korogwe,* Kwamsisi, Ngombezi na Kilole wamekuwa wakisumbuliwa na wimbi la wafugaji wahamiaji Mang'ati kutoka Manyara ambao wamekuwa wakizusha migogoro, kupiga, kuwadhuru watu na kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wananchi:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kadhia hiyo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kusimamia uondoshwaji wa wafugaji hao katika eneo la Halmashauri ya Mji wa Korogwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wapo wafugaji wahamiaji kutoka maeneo mbalimbali wakiwemo wa kutoka Mkoa wa Manyara. Hadi Oktoba, 2012, Kata za Mgombezi, Kwamsisi, *Old Korogwe* na Kilole zilikuwa na ng'ombe 16,300.

Wapo wafugaji ambao wamehamia maeneo yaliyotajwa bila kufuata utaratibu na kusababisha migogoro. Zipo sheria na Kanuni zinazosimamia taratibu za kuhamisha mifugo, sheria hizi ni pamoja na sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na.17 ya mwaka 2003, sheria ya maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010 na sheria ya mipango ya matumizi bora ya ardhi Na. 6, ya mwaka 2007.

Kwa kuzingatia sheria husika Wilaya ya Korogwe imeweka utaratibu wa kuhakikisha wafugaji wote wanaohamia wamefuata utaratibu uliopo na wana vibali. Serikali inawataka wafugaji wote nchini kufuata sheria Kanuni na taratibu zilizopo wanapohamisha mifugo ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza. Aidha, Serikali inauelekeza uongozi wa Wilaya ya Korogwe kuendelea na utaratibu waliojiwekea wa kuzingatia sheria husika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji ambao wameingiza mifugo katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe wataondolewa kwa kuzingatia sheria, Kanuni na Taratibu zlizopo. Mkuu wa Wilaya ya Korogwe kuanzia Mwezi Oktoba 2012, ameanza kutekeleza zoezi la kuwaondoa wafugaji ambao wameingiza mifugo yao bila kufuata sheria, Kanuni na Taratibu.

Zoezi hili litawekewa mkazo katika vikao alivyoviandaa Mkuu wa Wilaya kuanzia tarehe 13 Mei, 2013 katika Kata ya *Old Korogwe* na tarehe 15 Mei, 3013 katika Kata ya Kwamsisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kuhimiza kila Halmashauri kuhakikisha inatekeleza utaratibu wa mpango wa Matumizi bora ya ardhi kwa kuainisha maeneo kwa ajili ya wakulima, wafugaji na makazi ili kuondokana na migogoro isiyokuwa ya lazima. Aidha, wananchi wote wafugaji kwa wakulima wanatakiwa kuheshimu sheria zilizopo kuhusu matumizi bora ya ardhi ili kuepuka migogoro. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri.

Kwa kuwa, tatizo la Korogwe Mjini linalingana kabisa na Korogwe Vijijini hasa kwenye Kata ya Kwagunda katika Kijiji cha Gereza, Mkwakwani na Kwamzindawa, Kata ya Mnyuzi katika kijiji cha Lusanga na Ngomeni, na Kata ya Mswaha katika kijiji cha Mswaha Darajani.

Je, Serikali hawa wengine ambao wameingia na kuwasumbua sana wananchi wakulima wa kule kwa kuwapiga na kuwafungulia kesi zisizokuwa na msimamo mtawaondoa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mheshimiwa Chiku Galawa, tarehe 27 Mwezi Aprili, 2012 aliandika barua katika Wilaya zote nane zilizopo kwenye Mkoa wa Tanga akawaelekeza Wakuu wa Wilaya, Kamati za Ulinzi na Usalama, moja, wabainishe mifugo iliyohamia katika maeneo yao bila kufuata utaratibu na pili, waweke utaratibu wa kuwaondoa na kuwaelekeza mahali ambapo ama pamepangwa kwa ajili ya mifugo ama waondoke kurudi walikotoka kama hawakufuata utaratibu wa kuhamia.

Suala la kwamba ni lini hawa wataondolewa, tayari Wilaya ama Halmashauri ya Korogwe Vijijini kama walivyofanya Halmashauri ya Mji na wao wameanza utaratibu na hivyo, wao watatekeleza utaratibu huu katika ngazi yao kama walivyofanya wenzao wa Korogwe Mjini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Katika Mikoa karibu yote hapa nchini kuna matatizo kati ya wakulima na wafugaji na jibu la Serikali, limekuwa linafanana kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuiuliza Serikali, ni lini italeta Sheria au ni lini itaelekeza maeneo ya wafugaji na wakulima yatambuliwe Kisheria, ili kuondoa haya majibu kwamba, wanaondolewa? Wanaondolewa waende wapi, wakati nao ni Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria tayari zipo na katika jibu la msingi nimetaja Sheria husika. Kinachotakiwa ni kuhimiza katika kila Halmashauri, ambayo Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe katika Baraza la Madiwani, kuhakikisha kwamba, wanafuata utaratibu uliowekwa Kisheria, ili kubainisha maeneo na kupanga matumizi ya kila ardhi.

Moja, kwa kutenga maeneo ya makazi, maeneo ya kilimo, maeneo ya mifugo, maeneo ya hifadhi na kuhakikisha kwamba, kila Halmashauri inatunga Sheria ndogondogo kuhimiza kufuata Kanuni na taratibu hizo zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tatizo linakuwa pale ambapo Halmashauri haikuwajali na kuwawekea wafugaji maeneo yao ya malisho na kuwawekea miundombinu, hasa ya maji na huduma nyingine za jamii kama elimu pamoja na afya. Kwa sababu, hili likifanyika kwa uhakika wafugaji wataishi maeneo hayo waliyotengewa na waliyoendelezewa kwa sababu, kuhama ni adha hata kwao. Wao hawapendi kuhama, ila wanapolazimika. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kama alivyojibu Waziri, vizuri sana hili jibu la mwisho. Ni ukweli kwamba zoezi la kuwaondoa wafugaji, kuwarudisha katika maeneo yao linasababishwa na matumizi yasiyo bora ya ardhi.

Lakini Bunge, limekwishaeleza kwa kipindi kirefu sana umuhimu wa Serikali, kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza mipango ya matumizi bora ya ardhi. Halmashauri hazina uwezo wa kusimamia zoezi hili, kwa nini Serikali, hailichukui hili suala kama tulivyochukua *operations* nyingine, zikatengwa fedha za kutosha kuweka mipango bora ya matumizi ya ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria imekaa vizuri, Sera imekaa vizuri. Na tunaposema kwamba, ni Halmashauri Serikali, maana yake ni pamoja na Halmashauri zetu kwa sababu, Halmashauri ndio wakala wanaotekeleza shughuli hizi katika ngazi ya Hakmashauri na ngazi ya Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, kwa pamoja tushirikiane kuona kama fedha zaidi zitapatikana na Halmashauri ichukue kuendeleza maeneo haya ya malisho kwa ajili ya wafugaji kama pia ni eneo la kipaumbele kwao. *(Makofi)*

Hata fedha inapotengwa ikaenda kule isibainishwe ikabadilishwa kwenda kwenye shughuli nyingine badala yake iende kwa ajili ya shughuli hizo za kuwaandalia wafugaji maeneo ya kufanyia shughuli zao hizo za kiufugaji. *(Makofi)*

Na. 182

**Hitaji la Sheria Kudhibiti Madalali**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini kutakuwa na Sheria ya Kuwadhibiti Madalali *(Estate Agenchy Regulatory Bodies)* kama ilivyo Kenya, Uganda na Nchi nyingine za Afrika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Mariam Kasembe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu btunayo Sheria ya Madalali, Sura ya 227, *(The Auctioneers Act Cap. 227);* Sheria hii ilitungwa mwaka 1928 kama Sura 282 ya Sheria za Tanganyika. Ilifanyiwa marekebisho mwaka 1972 na mwaka 1994.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii inatambua kuwepo kwa shughuli za Dalali *(Business of Auctioneer)* kama mtu yeyote anayeuza mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika. Sheria ya ya Madalali, inampa Mamlaka Katibu Mkuu Hazina ya kutoa Leseni kwa Madalali kupitia Wilaya anayokaa mwombaji au anayotarajia kuweka shughuli zake za Udalali. Sheria hii haijaanzisha chombo chochote cha kusimamia na kudhibiti utendaji wa Madalali. Aidha, Sheria hii haijatoa Mamlaka ya kuanzishwa kwa chombo cha aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Sheria yetu ya Madalali, haitoi Mamlaka kwa Madalali kufanya shughuli za upangishaji wa ardhi au majengo. Sheria ya Madalali haisimamii au kudhibiti Mawakala wanaojishughulisha na uwakala wa majengo na ardhi.

Pia, ni kweli kwamba, Sheria yetu ya Madalali ni ya muda mrefu sana karibu miaka 85; yako mambo mengi ambayo yamebadilika na kupitwa na wakati. Na kwa kutambua hili, taratibu za kuifanyia marekebisho zimeanza. Baada ya kukamilisha mawasiliano ndani ya Serikali, Muswada utaletwa Bungeni, ili kukidhi mahitaji ya sasa na yajayo yanayohusiana na suala hili. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, hivi sasa Madalali wasio rasmi ni wengi na wamesababisha kupanda kwa kodi za nyumba, viwanja, hata mashamba na kuchukua kodi ya mwezi mmoja kwa nyumba au asilimia kwenye uuzaji wa mashamba na vitu mbalimbali.

Je, Serikali, ina mpango gani au maelekezo gani kwa madalali hawa, ili kukomesha tabia hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwaacha madalali hawa wakifanya biashara ambayo haina leseni wala kulipa kodi, Serikali, haioni inapoteza mapato?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Kasembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli madalali wasio rasmi wana usumbufu mkubwa. Sasahivi sisi katika Wizara ya Fedha, tunayo idadi ya madalali ambao wamesajiliwa kwa hivyo, naomba kuchukua fursa hii kuwaeleza Wabunge, pamoja na wananchi kwamba, wawe wanafuata wale madalali ambao wamesajiliwa, listi yao ipo inapatikana Wizara ya Fedha. Na kama itawezekana, basi sisi tunaweza tukaleta hapa tuka-*share* na Waheshimiwa Wabunge, Madalali wale ambao wamesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa maana hiyo wale Madalali ambao wanafanya biashara ambayo haijsajiliwa ni kweli wanakosesha mapato Serikali. Kwa hivyo tunaomba Waheshimiwa Wabunge, tulisimamie hili kuna Madalali ambao wamesajiliwa na ambao wanalipa mapato yao Serikalini.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kuna mianya ambayo Serikali, inapoteza mapato mengi sana. Kwa mfano, mtu amepangisha nyumba ameweka biashara, anapoenda kulipa kodi *TRA, TRA* inamlazimu alipe na ile kodi ya yule mwenyenyumba, yaani *percent* ya kodi ambayo aliilipa kule kwenye nyumba. Kwa hivyo, inatokea kwamba, sasa mtu anapoenda ku-*declare* kule *TRA* kwamba, nyumba alilipa labda kama ni 12,000,000/= kwa mwaka anaamua kuiweka makadirio ya chini anasema labda alilipa 6,000,000/= ili anapoenda kulipa kule alipe kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni kwamba, Srrikali, ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba, mtu anapolipwa kodi kwenye nyumba, inaweka mfumo ambao utamwezesha huyu anayechukua ile kodi, kulipa ile *percent* kule *TRA* pasipo kupitia huyu mtu, ambaye anafanya biashara kwenye kile chumba?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wenje, kama ifuatavyo:-

Nadhani tunachozungumza hapa ni Madalali, sina uhakika kama hao ambao wanalipa wako katikati ni Madalali rasmi ambao sisi kama Serikali, tunawajua. *Ofcourse on that matter* lazima tutakuwa tunapoteza mapato, lakini hata hivyo, kama ulihudhuria semina yetu ya Jumamosi *Big Result Now,* tunaweka mkakati maalum sasa wa kuweza kuweka mfumo ambao wananchi wataweza kulipa kodi ya nyumba wao wenyewe, moja kwa moja, bila ya kupitia kwa Madalali hapa katikati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nina swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba, wapo Madalali ambao wanafanya kazi ya udalali kinyume cha Sheria na kufanya kazi kinyume cha Sheria ni kosa kwa mujibu wa Sheria. Anatoa Tamko gani la Serikali, kwa Madalali wa nyumba, ambao wanawadhulumu wananchi wa Dar-es-Salaam, kwa kujitia udalali wa kuwapangisha nyumba na mara nyingine wanafanya utapeli? Tunataka Tamko la Serikali, juu ya hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, tayari tunayo Sheria, isipokuwa Sheria yetu ya sasa hivi ina mapungufu makubwa sana. Imetoa adhabu kwa wale Madalali ambao wanafanya kazi kinyume cha Sheria, lakini bado kutokana na mazingira ya sasahivi tunaona kwamba, hii adhabu haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ndio maana tunachukua hatua madhubuti kuweza sasa kubadilisha hii Sheria kwa haraka zaidi kuweza kuwadhibiti hao Madalali ambao wanafanya kazi kinyume cha Sheria. Lakini vilevile Serikali, ni sisi sote, tunatakiwa pia vilevile wananchi nao wachukue wajibu wao kama wananchi, wasikubali kupotezewa fedha zao. Wasikubali vilevile na wao wanapoteza fedha za Serikali, kwa ku-*deal* na hao Madalali ambao hawajasajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Wizara ya Fedha, tunayo orodha ya Madalali ambao tumewasajili. Wananchi wote, Waheshimiwa Wabunge na kila mtu atakapoitaka hiyo orodha sisi tunayo na inapatikana. Wasikubali kabisa kufanya biashara na Madalali ambao hawajasajiliwa.

Na. 183

**Huduma za Afya kwa Wafungwa na Mahabusu**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali, ina taratibu gani kwa kutoa huduma za afya kwa Wafungwa na Mahabusu waliopo Magerezani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafungwa na Mahabusu wanayo haki ya kupata huduma bora ya afya kama ilivyo kwa raia wengine. Ili kufanikisha utoaji wa huduma bora za afya Magerezani, jeshi la Magereza limeajiri Wataalamu wa Afya wa fani mbalimbali, kama vile Madaktari, Madaktari Wasaidizi, Maofisa Tabibu, Matabibu Wasaidizi, Wauguzi, Maafisa Afya, Wataalamu wa Lishe, Wataalamu wa Maabara, Wahudumu wa Afya na wengine.

Aidha, kila Gereza, lina zahanati ndani na nje; zahanati za ndani hutumika kutoa huduma za tiba kwa Wafungwa na Mahabusu na zile za nje hutoa huduma kwa wananchi, familia za watumishi na wananchi waishio jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea tatizo la mgonjwa kuhitaji uchunguzi au huduma nyingine ambazo hazipo katika Kituo husuka, mgonjwa hupewa rufaa kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Mkoa au ya Wilaya ya karibu. Kwa wale wenye matatizo yanayohitaji huduma za Madaktari Bingwa, Wafungwa na Mahabusu kupewa rufaa kwenda kutibiwa katika Hospitali za Rufaa Maalum kama Muhimbili, *KCMC,* Bugando, Mbeya, *Ocean Road* au Mirembe.

Changamoto zilizopo ni uhaba wa madawa, ambao haukidhi mahitaji kutokana na ufinyu wa bajeti na vilevile ukosefu wa magari ya kuwapelekea wagonjwa Hospitali. Hata hivyo, Jeshi la Magereza linafanya jitihada za kuwajumuisha Wafungwa na Mahabusu katika mfumo wa matibabu kupitia mfumo wa Bima ya Afya.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninayo maswali ya nyongeza mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja. Kwa kuwa, Mahabusu walio wengi na Wafungwa, wanakufa na kuugua kwa kukosa madawa na lishe bora. Mahabusu wanatolewa kwenye mahabusu asubuhi wanapelekwa Mahakamani, wanarudi saa 10.00 saa 11.00 jioni na wakati wengine ni waginjwa wa kifua kikuu na wengine wameathirika na *UKIMWI.* Wanashinda wakitetemeka na njaa Mahakamani, pamoja na juhudi kubwa za Serikali, za kuwapatia madawa. Je, Serikali, ina mkakati gani wa kudumisha huduma bora za lishe na malazi bora kwa mahabusu?

Kwa kuwa, zahanati zilizopo kwenye maeneo ya Magereza, zinawasaidia Mahabusu na Jamii inayozunguka, pamoja na familia za Maaskari. Je, Serikali, ina Mkakati gani wa kuweka huduma bora, pamoja na vipimo mbalimbali katika zahanati za Magereza na hasa tukianzia na Segerea, Keko na Ukonga Magereza?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifyatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada kubwa zinafanywa kuhakikisha kwamba, Wafungwa na Mahabusu wanapata chakula chenye virutubisho vya kutosha. Kwa upande wa wale ambao wana maradhi, kuna jitihada za kuongeza kwenye hicho kima 10% kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, wao wanapata lishe bora kuliko wengine.

Kwa hiyo, pia kuna huduma kwa wale ambao wanaugua kifua kikuu na *VVU,* kuna maeneo maalum wanatengwa, lakini pia wanapatiwa madawa ya ziada pamoja na lishe bora kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upungufu wa madawa, upungufu wa lishe, tumeuzungumza juzi hapa na hata jana tulikuwa tunazungumza, sio tu kwa Wafungwa, lakini hata kwenye Halmashauri zetu. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo Serikali bado inaendelea kuyafanyia kazi na kuna siku Wafungwa na raia wa Tanzania wote watapata madawa wanayoyahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zahanati ambazo zinatoa huduma kwa wananchi; Jeshi la Magereza limeanza kufanya uboreshaji wa zahanati hizi na kuna mfano mzuri pale Ukonga. Tayari zahanati ya pale ina vipimo, *bio-chemical* na vingine, na pia zinapima kama *CD4* na mambo mengine *ultra sound* na vifaa vingi ambavyo vipo sasa. Lengo ni kuhakikisha kwamba, Hospitali za namna hii zote zinapata vifaa hivi, ili familia na wananchi waweze kupata vipimo hivi kwa urahisi na madawa yanayohusika na maradhi yao. *(Makofi)*

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kumekuwa na tabia ya Askari Magereza kuwapiga Mahabusu na Wafungwa mpaka kuwaumiza, wakati mwingine kuwasababishia vifo na Wauguzi au Madaktari kushinikizwa kuandika ripoti tofauti na tukio lenyewe. Je, Serikali, inasemaje kuhusu Manesi hawa ambao wanakiuka taratibu za kazi zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mashishanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kumbukumbu zetu hili halipo. Sasa kama lipo, tunamwomba Mheshimiwa atuletee, ili tulifuatilie na tutoe adhabu inayofaa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, Wafungwa ama Mahabusu, wanapokuwa na hali mbaya ya ugonjwa hupewa rufaa kwenda Hospitali kubwa.

Kwa kuwa, wanapokuwa Hospitali kubwa kumekuwa na mbinu za Maaskari, kuwalegezea pingu, kwani hulazwa na pingu zao, na inasababisha mfungwa kutoroka, hasa wale wenye kesi kubwa kama ujambazi. Je, Serikali, haioni kwamba, kuwapeleka Wafungwa hawa kwenye Hospitali za wazi inasababisha utoro wa majambazi, ambao ni tishio kwa nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kuna mbinu za namna hii. Lakini pamoja na kuwa, zipo hizi mbinu hatuwezi tukasema huyu mtu ameambiwa aende kwenye Hospitali ya Rufaa, tukaogopa tusimpeleke moja kwa moja kw asababu, tatizo linaweza likawa na haki za binadamu.

Isipokuwa tunawahamasisha Madaktari na wengine ambao wanahusika, kuhakikisha kwamba, hawashiriki katika kuandaa mazingira ya hawa watu sugu kutoroka, lakini na sisi kule Magerezani tunawafahamu wepi wana dalili ya usugu na wepi hawana. Kwa hiyo, tunapowapeleka kule kwenye rufaa tunawapeleka na ulinzi stahiki.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea muda wetu ni mdogo maswali bado mengi Wizara ya Ardhi swali la Mheshimiwa James Mntangi.

Na. 184

**Kufutwa kwa Hati za Mashamba ya Mkonge**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kumekuwa na ucheleweshaji wa maombi ya kufutwa Hati za mashamba ya Mkonge yasioendelezwa Wilayani Muheza na Korogwe.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kufuta hati hizo iliyotolewa na Mheshimiwa Rais kwa mashamba ya Kibaranga, Kwafungo, Lewa, Azimio na Bwembwere?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inathibitisha kuwa ilipokea mapendekezo ya kufuta Hati Miliki za mashamba ya Mkonge yasioendelezwa kwa muda mrefu kutoka Wilaya ya Mheza na Korogwe mwezi Oktoba 2009 yakiwemo mashamba ya Kibaranga lenye Hati Namba 4856 na ukubwa wa hekari 5730, Kwafungo Hati Namba 13,896 lenye ukubwa wa hekari 362 na Lewa lenye ukubwa wa hekari 7412.9, shamba la Azimio lenye Hati Namba 5106 lenye ukubwa wa hekari 12,107 na Bwembwera Hati Namba 5628 na ukubwa wa hekari 5,730.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchambua mapendekezo hayo Wizara iliridhika kuwa yalikidhi vigezo vya ufutaji hati miliki kwa mujibu wa kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 inayoruhusu Serikali kubatilisha miliki ya ardhi yoyote ambayo mmiliki ameshindwa kutimiza masharti ya uendelezaji.

Baada ya uhakiki kukamilika mapendekezo hayo yaliwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano mwezi Disemba 2009 ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kuidhinisha ufutaji wa Hati Miliki ya ardhi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukisubiri uamuzi wa Mheshimiwa Rais naomba kupitia Bunge lako tukufu nimshauri Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Muheza na Korogwe kuwa wawe na subira na kudumisha amani jambo linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri naomba tu kumkumbusha kwamba mwaka ulipita mwezi kama huu niliuliza swali hilo hilo na majibu yalikuwa hayohayo. Hata hivyo ninapenda kutoa ushauri ufuatao, kwanza maeneo mengi ya mashamba hayo yamevamiwa lakini ni kwa kiasi kidogo kwa mfano Kibaranga kati ya hizo heka 5700 pengine ni heka 1000 tu zilizovamiwa.

Sasa tuna busara kwa sababu nchi hii inaongozwa na watu wenye hekima na busara wakati Hati za zamani zikifutwa ni kwa nini tusikae kabla ya kutoa Hati mpya tukapunguza yale maeneo ambayo tunadhani yamevamiwa ili tutoe Hati mpya katika maeneo ambayo yamebaki yenye salama kabisa na kupunguza migogoro na wananchi. Je Waziri anasemaje ushauri huo utafaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili watu wa Muheza wamekuwa na busara na hekima na kupenda amani. Mwaka uliopita nilimkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alikuja Naibu Waziri wake lakini siku moja baada ya Naibu Waziri ambaye alitembelea baadhi ya hayo mashamba alipoondoka tu Muheza aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Muheza aliamrisha wawekezaji kuvunja mazao ya watu waliokuwa wameingilia baadhi ya mashamba.

Sasa hii inatutia wasi wasi kwamba hivi kweli kwa kufanya hivyo tutadumisha amani. Sasa kwa sababu hiyo ninaomba nimuulize Mheshimiwa Waziri je atakubaliana na mapendekezo ambayo yeye mwenyewe aliniandikia miaka miwili iliyopita na kutaka kutukutanisha watu wote hawa wawili ili kufikiria namna ya kupunguza migogoro hiyo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba nimwelezee Mheshimiwa James kwamba tunapofuta Hati Miliki ya shamba sasa katika suala la mashamba ya mkonge tunasubiri uamuzi kama nilivyosema ufanyike mara tu uamuzi utakapofanyika ardhi ile kimsingi inarudi chini ya mamlaka ya Mheshimiwa Rais na tunapanga na kugawa utumiaji wa ardhi hiyo upya.

Sasa nadhani nifariji tu kwamba hakuna wasiwasi kwamba kuna watumiaji ambao wako juu ya ardhi ile kwa vyovyote vile matumizi bora ya ardhi yatazingatia matakwa yao kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu jambo la pili kwamba kuna wanaowabugudhi wananchi katika hali hiyo ni hali ambayo siyo tu mashamba ya Mkonge ni sehemu nyingi sana kwamba migogoro ya namna hii tunakuwa nayo na katika sehemu nyingi ambapo tuna migogoro ya namna ile pendekezo langu na maagizo yangu yamekuwa ku-*maintain status quo* kwa sababu hali halisi ni kwamba uvamizi wa kiholela umetokea inatakiwa udhibitiwe.

Lakini wenye mashamba wengine wenyewe wameyatelekeza wao hawakuweza kuyalinda inavyotakiwa sasa unakuta kwamba yamevamiwa hali halisi ili kulinda amani kwa sababu ulinzi na usalama ndiyo kitu cha kwanza pendekezo ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *status quo* mpaka hapo Sheria inapochukua mkondo wake.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Waheshimiwa Wabunge muda tuliokuwa nao ni mdogo swali refu, majibu marefu na jibu hili lina *multiple factor* kwa wote wengine. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Martha Mlata.

Na. 185

**Usafiri wa Barabara toka Mtwara – Bukoba**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI (K.n.y. MHE. MARTHA M. MLATA)** aliuliza:-

Serikali iliwahi kuahidi kuwa katika kipindi cha awamu ya nne wananchi wataweza kusafiri kwa *taxi* toka Mtwara hadi Bukoba.

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefika wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, viti maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kwamba nia ya msemo huo ilikuwa kuonyesha kwamba wananchi wataweza kusafiri kutoka Mtwara hadi Bukoba kwenye barabara ya lami.

Aidha napenda kuliarifu Bunge lako kwamba lengo hili limetekelezwa kwa mafanikio makubwa hadi kufikia 99% ya barabara yote kutoka Mtwara hadi Bukoba barabara yote kuanzia Mtwara- Dar es Salaam- Dodoma- Singida- Nzega- Tinde- Usagara- Geita- Bwanga-Kyamyorwa hadi Bukoba yenye urefu wa kilomita zipatazo 1,989 imejengwa kwa kiwango cha lami isipokuwa sehemu fupi yenye urefu wa takribani kilomita 26 katika barabara ya Ndundu - Somanga ambayo itakamilika kujengwa kwa kiwango cha lami kabla Desemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya awamu ya nne itahakikisha ahadi ya wananchi kusafiri kwenye barabara ya lami toka Mtwara hadi Bukoba inatekelezwa.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri wanayofanya katika sekta hasa hii ya miundombinu ya barabara. Lakini pamoja na hayo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa kuwa barabara hizi zinajengwa kwa kweli kwa hadhi nzuri sana lakini kuna maeneo mengine kwa sababu ya kuongezeka kwa magari na uzito zinaharibika.

Kwa mfano katika barabara hii ambayo imezungumziwa maeneo ya Sekenke na maeneo ya Mabuki kule ukarabati hauendi na kukidhi kile kiwango cha awali kilichokuwepo sasa Serikali inampango gani kuhakikisha kwamba ule ukarabati unafanyika kwa haraka lakini kwa kiwango kile cha awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili sera hii ya kusafiri kwa taxi kutoka eneo moja hadi jingine ni nzuri sana kwa Taifa letu. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia lini sera hii itatekelezwa vile vile kutoka Dar es Salaam hadi Musoma kupitia Maswa na Bariadi na Lamadi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge kwamba yamekuwa yameharibika sisi Wizara tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha maeneo hayo kama yameharibika kwa sababu ya Kandarasi yanarudiwa kwa gharama za Kandarasi kwa mfano ametoa mfano sehemu ya Sekenke kandarasi tulimrudisha pale na amefanya kwa gharama zake na sehemu hiyo amemaliza na atakaa pale kwa mwaka mzima akiangalia hata likitokea shimo lazima alirudie kwa gharama zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maeneo mengine pia yamekuwa yakiharibika suala lingine ni kutokana na uzidishaji wa mizigo kwa kuvunjwa kwa Sheria namba 30 ya mwaka 1973 na kwa bahati mbaya katika nchi yetu *gross weight* ya magari yanayopita kwenye barabara zetu ni tani 56 wakati ukitoa mfano katika nchi nyingine zilizoendelea kwa mfano Marekani ni tani 40, Uingereza tani 44, Denmark tani 48 na kuna sehemu zingine kama Amenia tani 36 kuna sehemu zingine tani 40 sisi ni tani 56 *gross weight* kwa hiyo tuko kwenye mchakato wa kuipitia hii sheria ili uzidishaji wa mizigo katika barabara zetu uweze kuzingatiwa na nina uhakika Sheria hii tutakapoileta ya mabadiliko Wabunge mtaipitisha ili barabara zetu ziweze kudumu zaidi kwa sababu hata nchi ya Kenya na Uganda *gross weight* ni tani 54 sisi ni 56 wakati ni nchi maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upitishaji wa maeneo ya barabara kama ile ya Lamadi aliyoizungumza tumekwisha kwenye sehemu ya Lamadi hadi Bariadi Kilometa 71.1 kandarasi yuko kwenye *site* na kutoka sehemu nyingine ile ya Mwigumbi kuja Bariadi nayo tumeshaitangaza tenda ili siku nyingine watu kwenye maeneo hayo nao wapite kwa taxi wakitoka Dar es Salaam kwenda Musoma na kwanza watakuwa wamepunguza zaidi ya kilomita 101 badala ya kupita barabara ndefu ya kupita mpaka Mwanza.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma ni moja ya Mikoa ambayo imefaidika sana na miradi ya barabara. Lakini barabara za Mkoa wa Kigoma hazina maana yoyote kama barabara za Mikoa ya jirani kama Tabora hazitengenezwi kwa sababu watu wa Kigoma watatoka waende wapi.

Leo hii tunavyozungumza barabara ya kutokea Tabora kwenda Urambo Mkandarasi amesimama. Kutokea Tabora kwenda Nzega Mkandarasi amesimama, kutokea Tabora kulelekea kuja Ikigi Mkandarasi amesimama Serikali, Waziri anatoa kauli gani kuhusiana na barabara za Mkoa wa Tabora ili watu wa Kigoma waweze kuunganishwa na sehemu nyingine ya Tanzania?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zitto kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Zitto kwa kuipongeza Serikali ya CCM kwamba inajenga barabara hicho ni kitendo cha kishujaa kwa kumuona Mbunge wa upande mwingine anapongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani ya uchaguzi kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa 66 hadi wa 72 wa Ilani ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Zitto kwamba barabara za Tabora ambapo ni kutoka Nzega hadi Tabora, Tabora kwenda Chaya, Tabora kwenda Urambo na kwa sasa hivi tumeshatangaza kutoka Kalihuwa hadi Kazilambwa barabara hizi zote zitakamilika kulingana na Mkataba ulivyopangwa.

Ni ukweli kwamba katika miezi miwili iliyopita kwa sababu *stage* ya kazi zilizokuwa zinafanyika kwenye barabara pale zilikuwa zimefikia kwenye *stage* ya kufanya *stabilization. Stabilization* huwa ni kuchanganya kokoto, udongo pamoja na simenti.

Kazi hizi hazikufanyika kwa sababu katika mwezi uliopita miezi miwili iliyopita palikuwa na mvua nyingi sana Tabora, isingeweza kuwa busara kuanza kuchanganya simenti ya *stabilization* kwenye barabara hizo wakati mvua zinanyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge Zitto pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Tabora barabara hizi zimeshawekwa jiwe la msingi na Mheshimiwa Rais zitaendelea kujengwa.

Kwa sasa hivi tumefikia *stage* ya kufanya *stabization* na baadae tutaanza kujenga *prime* na kwa bahati nzuri karibu yote imeshafikia zaidi ya 30% hadi sasa hivi nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Sitta na Wabunge wote wa Tabora na Urambo.

Kwa bahati nzuri wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi barabara hizi zitakamilika kulingana na mkataba wake uliopangwa na katika bajeti hii tumepanga fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha miradi inayoendelea kwa barabara za Tabora ili zikaungane na daraja la Kikwete.

Aidha zikaungane na kule anakotoka Zitto kwa barabara ya Mwandinga, Manyovu mpaka watu wawe wanatoka Burundi kuja Dar es Salam kwa barabara za lami na ikiwezekana kwa Bajaji.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru tunaendelea, sasa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo namwita Mheshimiwa Israel Yohana Natse.

Na. 186

**Mtandao wa Barabara za Lami**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY (K.n.y. MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE)** aliuliza:-

Mtandao wa barabara za lami nchini ni moja ya nyenzo muhimu katika kuharakisha maendeleo.

(a) Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara ya lami inayounganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara kutoka Karatu kwenda Mbulu hadi Hydom?

(b) Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara toka njia panda-mang'ola-matala hadi Lalago kwa kiwango cha lami hasa ukizingatia kuwa barabara hiyo inaunganisha Mikoa ya Arusha, Singida na Shinyanga?

(c) Je, ni lini itatimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutengeneza barabara kilomita 2 kwa kiwango cha lami ndani ya Mji wa Karatu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mchungaji Israel Y. Natse Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Karatu- Mburu –Hydom yenye urefu wa kilomita 155.5 ambayo inaunganisha Mikoa ya Arusha, Manyara na Singida katika kijiji cha Kidarafa ni miongoni mwa barabara zilizopangwa kufanywa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina chini ya Mradi wa *Transport Sector Investment Program.* Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umepangwa kufanywa katika mwaka wa fedha 2014/2015 na ujenzi utaanza baada ya kazi ya usanifu wa kina kukamilika na fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kuu ya kutoka njia panda ya Oldeani-Mang'ola –Matala Kilomita 136 ilikuwa ya ngazi Wilaya na ilipandishwa hadhi kuwa barabara kuu mnamo mwezi Julai 2010.

Hadidu za rejea za upembuzi yakinifu na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami hadi Kolandoto jumla ya kilomita 336 ziliandaliwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Zabuni za kumpata Mhandisi mshauri ili kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zitatangazwa katika mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Aidha sehemu ya barabara hiyo inayohusisha ujenzi wa daraja la Sibiti na maingilio yake tayari ipo ina mkandarasi anaitwa *Hainan International Limited* ambaye anaendelea na kazi kwa gharama ya shilingi bilioni 16.32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutengeneza kilomita 2 za lami ndani ya mji wa karatu itatekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kwa kutenga fedha za ujenzi wa barabara husika.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante suala la kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ila naomba Mheshimiwa Waziri awaelezee wakazi wa eneo la Karatu-Mbulu hadi Hydom kwa lugha raisi ni lini watapanda gari kwa kupitia barabara ya lami katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hiyo inasomba tani nyingi za mizigo, mifugo na abiria binadamu na kusababisha *raps* yaani *raster* katika sehemu nyingi kwa sababu ya upungufu wa *maintenance.*

Je, kwa kipindi wananchi wakingojea barabara ya lami Serikali iko tayari kuongeza pesa ya *maintenance* kutoka *Road Fund Board*?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Akunaay kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunashukuru kwa pongezi na shukurani ulizozitoa na lini watapanda magari kwenye barabra ya lami ni kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba mara tutakapomaliza usanifu wa barabara hizo basi tutatafuta fedha ili tuweze kutangaza tenda kujenga ziwe barabara za lami.

Kwa hiyo barabara ikiisha watatembea kwenye barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya matumizi ya barabara hiyo kwamba magari makubwa yanapita na maombi yako kwamba tuongeze fedha za *Road Fund* kwa ajili ya kuweza kufanya matengenezo ombi hilo tunalipokea na tutalizingatia kwenye mapendekezo ya Bajeti ambayo Waziri wa Ujenzi atawasilisha siku ya Jumatatu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara ya Elimu Mafunzo ya Ufundi, namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa.

Na. 187

**Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA** aliuliza**:-**

Uko mpango mahasususi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi wa Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi kwenye kila Wilaya nchini ili kukuza vipaji vya vijana wetu waweze kujiajiri au kuajiriwa kwenye sekta rasmi nchini.

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi kutekeleza mpango huo?

(b) Je, kuna ratiba inayoonyesha kuwa kila Wilaya itakuwa imepatiwa Chuo hicho?

(c) Je, Serikali imeandaa mikakati gani mahasusi ya kukiwezesha Chuo cha Taifa cha Ualimu cha Ufundi Stadi kilichopo Morogoro ili kutoa Walimu wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali iameahidi kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya zote nchini katika kutekeleza ahadi iliyotolewa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 na 2010. Katika kutekeleza azma hii, Serikali imedhamiria kujenga vyuo vipya katika Wilaya zisizo na Chuo cha Ufundi Stadi cha aina yoyote.

Ujenzi huu utafanyika katika awamu mbili, awamu ya kwanza itahusisha Wilaya 28 na awamu ya pili itahusisha Wilaya 15 zisizo na Chuo cha Ufundi wa aina yoyote. Ujenzi huu utafanyika katika awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza, Ujenzi wa Chuo cha Wilaya ya Makete ambao umekamilika, na katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali

imeanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi katika Wilaya za Ludewa, Namtumbo, Kilindi, Ukerewe na Chunya. Wilaya nyingine zilizopo katika awamu hizi mbili zitaendelea kujengewa vyuo vya *VETA* kulingana na upatikanaji wa fedha kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jitihada hizo, Serikali ina mpango wa kuviwezesha na kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs)* kutoa mafunzo ya Ufundi Stadi. Mpango huu utatekelezwa katika awamu tatu ambapo katika awamu ya kwanza Serikali imevijengea uwezo Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 25 kati ya 55 vilivyopo katika Wilaya mbalimbali nchini.

Vyuo hivi vimeshaanza kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi ambapo kila kimoja kimedahili wanafunzi 50. Katika awamu ya pili na ya tatu, Mpango huu utahusisha vyuo 30 kuanzia mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa na kuanza kutekeleza mpango mahsusi wa kuongeza udahili wa Walimu wa Ufundi Stadi kwa kutumia Chuo cha Ualimu cha Ufundi Stadi Morogoro. Ambapo katika mwaka wa fedha 2013/2014 Chuo kinatengemea kuanza ujenzi wa Mabweni ambayo uwezo wake utakiwa na nafasi 90 ambazo zitaongeza idadi ya walimu watakaohitimu kutoka 120 wa sasa hadi 210 kwa mwaka.

Pia, Chuo kupitia vituo vyake Nje ya Chuo (*Off – Campus Centres*) vinatoa Mafunzo ya ualimu katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Shinyanga, Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mtwara na Ruvuma, ambapo jumla ya walimu wa ufundi stadi 500 wanahitimu kwa mwaka ni walimu 500.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba niulize maswali madogo ya nyongeza yenye sehemu a) na b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana wengi wanapenda sana kusoma masuala ya ufundi hasa kwenye fani ya ushonaji na ujenzi lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba wanakuwa hawana vitendea kazi mara tu wanapomaliza masomo haya. Ukizingatia hata kwenye chuo cha *VETA* Mbeya wanafunzi hawa pia hawana vitendea kazi. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie Serikali ina mkakati gani kwa vijana hawa mara tu wanapomaliza mafunzo yao?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi amelieleza Bunge hili kwamba Serikali itaboresha vile vyuo vya maendeleo ili viwe vinatoa mafunzo stadi. Mimi ningeomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri katika Mkoa wangu wa Mbeya ni vyuo vingapi ambavyo vimetoka kwenye Vyuo vya Maendeleo kuwa Vyuo vya Mafunzo Stadi ili kupunguza soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi muda wetu umekwenda.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjerwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mheshimiwa Mbunge anapenda kuona kwamba je vijana hawa wanaomaliza vyuo vya *VETA* hasa kwa Mkoa wa Mbeya wanapokuwa wanamaliza wanafanyaje ili waweze kujiendeleza na kupata vifaa vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wa Serikali tunasema kwamba au tunashauri kwamba vijana hawa kwanza waungane wakishamaliza vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA).* Waungane kuanzia vijana watatu mpaka kumi, wanatengeneze vikundi vidogo vidogo vya ujasiliamali, halafu watengeneze mikakati ya ushirika au *Joint Venture* ili

waweze kupeleka maandiko *bank* na Serikali iko tayari kuwakopesha fedha kupitia *SACCOS* au *Bank* ya *NMB*.

Swali la pili ambalo ni b) katika Mkoa wa Mbeya ni vyuo gani vya *FDCs* vimekuwa vimeshauwishwa kutoa mafunzo ya *VETA?*

Ni kweli nimshukuru Mheshimiwa Mary Mwanjelwa kwa jitiada hizi ambazo kwa Mkoa wa Mbeya ni kama Wilaya mbili mpaka sasa, Wilaya ya Rungwe, Chuo cha Katumba kilikuwa ni Chuo cha *Folk Development College,* tayari mafunzo yameshaanza kutolewa kwa kozi za Umeme na *Computer.* Kwa Wilaya ya Mbeya Mjini Chuo kile cha Nzomve kiko kwenye awamu ya pili. Namshauri Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa namfahamu ni mpambanaji kwa vijana wa Mbeya, awashauri tu wakae mkao wa kula. Baada ya Chuo hiki kubadilika wataanza kupata ajira pale Nzomve na kusoma masomo ya ufundi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha sana, swali letu la mwisho Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Tekinolojia.

Na. 188

**Mawasialiano ya Simu za Mikononi Jimboni Kwela**

**MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA** atauliza:-

Kumekuwepo na ahadi ya muda mrefu ya kuvipatia mawasialiano ya simu za mikononi vijiji mbalimbali vya Jimbo la Kwela:-

Je, ni lini Serikali itafikisha mawasialiano hayo katika Kata ya Milepa, Vijiji vya Milepa, Kisa, Msia, Kata ya Kaoze Vijiji vya Kianda, Igonda, Tululu na Chombe na Vijiji vyote vya Kata ya Mtinga?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Tekinolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)* imehakiki mahitaji ya huduma za mawasialiano katika maeneo mbalimbali nchini na kubaini maeneo mengi yasiyokuwa na mawasialiano mazuri au kutokuwa na mawasiliano kabisa.

Utafiti huo umejumuisha vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge vya Kisa, Milepa, Msia, pamoja na vingine vya Ilemba, Kinambo, Nankanga, Sakalilo na Solola katika Kata ya Milepa.

Aidha, katika Kata ya Kaoze, vijiji vya Tululu, Mkusi, Kianda, Igonda, Kawilo, Kapenta na Chombe vimefanyiwa utafiti kwa ajili ya kupeleka huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutangaza zabuni ya kwanza Desema, 2012 kati ya Kata 152, ni Kata 52 tu ndizo wazabuni waliweza kukidhi masharti ya zabuni na kushinda zabuni hizo. Aidha, tayari mikataba ya kuanza kazi katika Kata hizo 52 imeshasainiwa na utekelezaji unatengemewa kuanza mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa vijiji vilivyoko katika Jimbo la Kwela vinapata mawasiliano ya simu za mikononi, mfuko wa mawasialiano kwa wote umeorodhesha vijiji vilivyoko katika Kata za Milepa, Kaoze na Mtinga kwa lengo la kuvifanyia upembuzi yakinifu ili hatimaye viweze kujumuishwa katika zabuni inayotarajiwa kutangazwa mwezi Juni, 2013.

**MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi majibu ya tatizo hili yanakuwa yakionyesha matumaini, lakini utekelezaji wake unasuasua na sijui ni lini matatizo haya yatakamilika katika nchi yetu.

Je, hakuna njia nyingine mbadala ya kuharakisha jambo hili?

Swali la pili, ukanda wa Ziwa Rukwa katika vijiji nilivyovitaja ni Ukanda wa kibiashara kutokana na umaarufu wa kilimo cha mpunga, uvuvi wa samaki na ufugaji. Kutokana na umaarufu huo kumekuwa na uvamizi wa mara kwa mara wa majambazi na taarifa hushindwa kufika mapema kwenye vyombo vya dola. Je, Serikali inafanya nini kuharakisha mawasialiano katika maeneo hayo?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyoamua kuingia katika biashara hii tulitoa leseni kwa makampuni ya simu na kuyaachia uamuzi wa kupeleka mawasiliano kule ambako wanataka. Tulikuwa tunadhani hilo ni kosa kwa sababu tungeweka masharti ya leseni ya kwenda vijijini ambako wananchi wanahitaji mawasiliano vilevile. Kutokana na kubaini kosa hilo tukaanzisha mfuko wa mawasialiano kwa wote ili tutoe ruzuku kwa makampuni haya kwenda kupeleka mawasiliano maeneo ya vijijini. Tumebaini kwamba ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu fedha nyingi katika mfuko huu zinatokana na mkopo wa Benki ya Dunia. Kumekuwa na matatizo makubwa sana na asubuhi ya leo kabla sijaingia nilikuwa nagombana na watu wa Benki ya Dunia na *UCAF* kuhusu ucheleweshaji wa jambo hili.

Mheshimiwa Malocha naomba nikuhakikishie kwamba hata kwangu mimi nina Kata kumi na sita na kata nane hazina mawasiliano. Kwa hiyo, katika mambo ambayo tumefanya Mheshimiwa Waziri na mimi ni kuwaomba wataalam kujaribu kufikiria njia mbadala kwa sababu mikopo kama tunavyofahamu na Waheshimiwa Wabunge muna

uzoofu na mradi wa maji wa banki ya dunia, taratibu zinachukua muda mrefu mpaka upate *no objection* kwenye kila hatua na nadhani ahadi yetu sisi ni kutekeleza jambo hili kabla ya mwaka 2015. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kama ikiwezekana tukapata fedha zetu wenyewe za ndani kupitia Bajeti tunaweza kulifanya jambo hili kwa haraka sana. Kwa sababu Bunge lina uwezo wa kuandika bajeti kwa utaratibu mpya wa sasa tunaomba mtusaidie katika hilo ili tuweze kuharakisha jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mawasiliano kwenye maeneo ya mipaka. Hilo ni kweli Mheshimiwa Deogratius A. Ntukamazina, kwake kuna mpaka, ukienda Kyela na Ileje kuna mpaka, Manyovu kunampaka pia. Kutokana na utaratibu ambao nimeeleza awali ambao umetunyima *control* ya kupeleka mawasiliano kule ambako tunahitaji, imepelekea kwamba maeneo ambayo ni muhimu na nyeti kwa usalama wa Taifa hayana mawasiliano.

Hata hivyo, katika mazungumzo tunayofanya na wenzetu wa mfuko na *Bank* ni kwamba bila kujali biashara katika maeneo haya lazima yapate mawasiliano kwanza kwa ajili ya usalama wa nchi yetu.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, nina matangazo mawili. Semina, Mwenyekiti wa TWPG Mheshimiwa Anna Abdallah anaomba kuwatangazia Wabunge wanawake wote kwamba kesho tarehe 11 Mei, 2013 kutakuwa na semina itakayofanyika kuanzia saa 4 asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa Idd Azan, anaomba kuwakumbusha Wabunge wote kwamba kutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* katika Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo kesho tarehe 11 Mei, 2013 Jumamosi. Mechi hiyo itahusisha mpira wa miguu na pete, Kikapu na timu zote zitaondoka Ofisi za Bunge kuelekea Hombolo. Usafiri umeandaliwa na itifaki imezingatiwa. Waheshimiwa Wabunge wote wanaombwa kuzingatia muda. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2013/2014
### Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Mohammed Ghalib Bilal, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa uongozi wao mahiri ambao umewezesha kushamiri kwa usawa wa jinsia na uzingatiaji wa haki za mtoto katika jamii ya watanzania. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge. Tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili muweze kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Makamu Mwenyekiti

Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda (Mb.) kwa kuichambua na kuijadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo yametuwezesha kuboresha na kukamilisha bajeti katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu aipokee na kuilaza mahali pema peponi roho ya Marehemu Salim Hemed Khamis aliyekuwa Mbunge wa Chambani. Umahiri wake katika kuchangia mijadala Bungeni tutaukumbuka daima.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na majanga pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini. Aidha, kwa namna ya pekee ninachukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa ndugu wa marehemu waliofariki dunia kutokana na kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16 jijini Dar es Salaam. Vilevile, natoa salamu za pole kwa ndugu wa marehemu waliofukiwa na kifusi katika machimbo ya kokoto huko Arusha.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 kwa kipindi cha januari, 2011 hadi machi 2013. Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2011 hadi Machi, 2013 Wizara iliendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 kwa mafanikio makubwa. Ilani ilitekelezwa katika maeneo manne ambayo ni: Ajira na Uwezeshaji wa Wananchi, Elimu ya Juu, Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali na Demokrasia na Madaraka ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Ajira na Uwezeshaji wa wananchi. Ilani ya CCM, Ibara ya 78 imeelekeza kuimarisha na kupanua mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili vipokee vijana wengi zaidi na kuwapatia mafunzo ya maarifa ya kisasa katika fani za kilimo, biashara, ufundi stadi na ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ujuzi na stadi mbalimbali kwa wananchi yana umuhimu wa pekee kwa sasa kwa sababu yanawawezesha wananchi kujiajiri na

kuajiriwa. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia vyuo 55 vya maendeleo ya wananchi, iliwapatia mafunzo ya ujuzi na stadi za maisha wananchi 105,691 wakiwemo wanawake 49,000 na wanaume 56,691. Mafunzo hayo yanawawezesha wahitimu kujiajiri na kuajiriwa, hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi.

Mafunzo hayo ni pamoja na: uashi, useremala, ushonaji, umeme wa majumbani, kilimo, ususi na upishi. Stadi hizi zinachukua vijana wengi ambao wanatoa mchango mkubwa katika shughuli nyingi za maendeleo ya jamii nchini. Aidha, Wizara imeanza kutoa mafunzo ya ufundi stadi kupitia vyuo 25 vya maendeleo ya wananchi na kuanzia Januari 2013, jumla ya wanafunzi 1,173 walianza masomo. Pia karakana tano zilijengwa ili kuboresha mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu. Ibara ya 85 (e) ya Ilani ya CCM imeelekeza kuongeza udahili kwa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu. Wizara kupitia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru iliendelea kudahili wanafunzi katika Shahada ya kwanza ya fani za Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Miradi, Maendeleo ya Jamii, Maendeleo ya Jinsia na Stashahada ya Uzamili ya Maendeleo ya Jamii. Jumla ya wanafunzi 312 wakiwemo wanawake 178 na wanaume 134 walidahiliwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa mafunzo ya elimu ya juu, Wizara vilevile ilitoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii kupitia vyuo vinane vya kawaida ambavyo ni Buhare, Missungwi, Rungemba, Uyole, Ruaha, Mlale, Mabughai na Monduli. Jumla ya wanachuo 8,741 wakiwemo wanawake 5,904 na wanaume 2,837 walidahiliwa. Mafunzo yalitolewa katika ngazi mbili ambazo ni Stashahada (wanachuo 1,854) na Astashahada (wanachuo 6,887). Wahitimu katika fani hizi huwezesha jamii kutekeleza shughuli zao za maendeleo kwa kutumia mbinu shirikishi na kuzingatia usawa wa jinsia na haki za mtoto.

Mheshimiwa Spika, Kuyaendeleza makundi mbalimbali. Ibara za 204 na 205 ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2010, imeelekeza kuwa mikataba ya haki za wanawake na watoto iliyoridhiwa itekelezwe kikamilifu. Mikataba hiyo inaelekeza kuyaendeleza makundi maalum ya watoto na wanawake.

Mheshimiwa Spika, Watoto. Katika azma yake ya kuendeleza na kuhakikisha watoto wanapatiwa haki zao, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau imefanya utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi. Utambuzi umefanyika katika halmashauri 95 ambapo watoto 849,051 wametambuliwa wakiwemo wasichana 407,544 sawa na asilimia 48 na wavulana 441,507 sawa na asilimia 52.

Watoto hao kwa sasa wanapatiwa huduma za elimu, afya, chakula na msaada wa kisheria na kisaikolojia kupitia wadau mbalimbali. Baadhi ya wadau hao ni pamoja na; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, *Save the Children*, *Family Health International (FHI 360)*, *Compassion*, *World Vision Tanzania*, *UNICEF* na *Plan International*.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 imetafsiriwa katika lugha nyepesi na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Lengo ni kuwawezesha watanzania wote kuielewa na hivyo kurahisisha utoaji wa haki za mtoto ambazo ni: kuishi; kulindwa; kuendelezwa; kutobaguliwa na kushirikishwa.

Vilevile, Wizara imeandaa na kusambaza Kielekezi cha Ushiriki wa Mtoto (*Child Participation Toolkit*) cha mwaka 2012 na Mwongozo wa Uundaji wa Mabaraza ya Watoto katika ngazi za kijiji, kata, wilaya na mkoa ili kuongeza ushiriki wa watoto katika masuala yote yanayohusu maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na *UNICEF* na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa *(CDC)* ilifanya utafiti kuhusu Ukatili Dhidi ya Watoto hapa nchini na kubaini kuwa watoto wengi hapa nchini walifanyiwa ukatili wa kingono, kimwili na kunyanyaswa kisaikolojia kabla ya kufikisha miaka 18. Utafiti huu umebaini kuwa watoto wa kike watatu kati ya 10 walifanyiwa ukatili wa kingono na mvulana mmoja kati ya saba alifanyiwa ukatili huo.

Aidha, zaidi ya asilimia 70 ya watoto wote walifanyiwa ukatili wa kimwili na kisaikolojia kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Kutokana na utafiti huo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa kutokomeza ukatili huu.

Kwa kuanzia, Mpango wa mwaka mmoja (2012/13) unatekelezwa na Mpango Kazi wa miaka mitatu (2013–2016) umezinduliwa hivi karibuni. Matokeo ya utafiti huu yaliwezesha kuanzishwa kwa Madawati ya Jinsia na Watoto katika Vituo vya Polisi na fomu ya Polisi Na. 3 *(PF 3)* imeboreshwa ili kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wanaopata madhara kutokana na ukatili huo.

Mheshimiwa Spika, Wanawake. Halmashauri mbalimbali ziliwezesha wananchi kiuchumi hususan wanawake, kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF).* Jumla ya shilingi milioni 168 zilitolewa kama mikopo kwa wanawake wajasiriamali katika halmashauri 21. Halmshauri hizo ni:

Mkinga, Kibaha, Dodoma Manispaa, Meatu, Korogwe H/W, Mkindani, Kilolo, Korogwe H/MJI, Njombe, Handeni, Kilosa, Ulanga, Loliondo, Chato, Bukoba, Lushoto, Ngara, Siha, Biharamulo, Chamwino na Maswa. Uwezeshaji pia ulifanyika kupitia Benki ya Wanawake Tanzania ambapo jumla ya shilingi 12,149,873,029.00 zilitolewa kama mkopo kwa wajasiriamali wakiwemo wanawake 11,931 na wanaume 3,097.

Mheshimiwa Spika, suala la kuzuia ukatili dhidi ya wanawake ni la msingi katika kuendeleza familia na Taifa kwa ujumla. Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto imefanya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufuatilia na kuzuia ukatili wa wanawake hasa watoto wa kike wasikeketwe.

Aidha, Mwongozo wa Kudhibiti Ukatili wa Kijinsia na Mkakati wa Taifa wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia nchini umeandaliwa. Mwongozo huo unatumiwa na kamati za ukatili wa kijinsia, ulinzi na usalama katika ngazi za mikoa, halmashauri za wilaya pamoja na wadau wengine nchini. Vilevile, mafunzo ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na albino yalitolewa kwa kamati za wilaya za ulinzi na usalama katika mikoa ya Mwanza, Manyara, Mara na Shinyanga. Mafunzo hayo yaliwapatia ujuzi na mbinu za kushughulikia na kupunguza tatizo la ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Demokrasia na Madaraka ya Umma. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 Ibara ya 188 (a) imeelekeza Serikali kuhakikisha kwamba Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanajishughulisha na majukumu ambayo yameandikishwa kuyatekeleza na kwamba hayapati nafasi ya kujiendesha kinyume na makusudio hayo.

Katika kutekeleza hilo, Wizara ilitoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 na Kanuni za Maadili ya NGOs kwa wadau 4,989. Wadau hao walitoka katika taasisi za elimu, taasisi za fedha, taasisi za kiserikali, mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Wizara ilifuatilia na kukagua shughuli za NGOs 38 kutoka nje na 183 za ndani kwa kuchambua taarifa za fedha na kazi zilizowasilishwa na mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyotajwa hapo juu, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na: kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; mazingira duni ya

kujifunzia na kufundishia katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; kutokuwepo kwa uwazi na uwajibikaji kwa baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na ufinyu wa bajeti katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Sekta ya maendeleo ya Jamii na Changamoto zilizopo. Majukumu ya Wizara yangu ni kufanikisha ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, kuleta usawa wa kijinsia, upatikanaji wa haki za mtoto na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Majukumu haya yanatekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, ushiriki wa wadau umechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji na uboreshaji wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo kwa kupitia mafunzo ya stadi za kazi yanayotolewa na vyuo vyetu vya maendeleo ya wananchi ambavyo tumeendelea kuviimarisha. Walengwa wakuu wa mafunzo haya ni wahitimu wa shule za Msingi na Sekondari, ambao hukosa fursa za kuendelea na masomo ya juu. Mafunzo haya huwawezesha kujiajiri na kuajiriwa, hali inayowasaidia kukuza uchumi wao na kupunguza umaskini katika jamii. Udahili katika vyuo hivi kwa mwaka 2012/2013 ni wanafunzi 41,681.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendelea kuimarika kwa hali ya vyuo vyetu vya maendeleo ya wananchi bado kuna changamoto nyingi zinazovikabili vyuo hivi katika kufikia lengo la kukuza ajira hapa nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na: uchakavu wa majengo na miundombinu; upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali; na uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia, vyombo vya usafiri, nyumba za watumishi, madarasa, karakana na mabweni. Jitihada mbalimbali zinaendelea katika kuzikabili changamoto hizi, zikiwemo ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa zana za kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo ni muhimu katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu katika kuraghibisha na kuhamasisha jamii ili kuongeza ushiriki huo. Wataalam hawa hufanya kazi katika ngazi za Wizara, sekretarieti za mikoa, halmashauri za wilaya, wakala na idara mbalimbali za Serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi. Hapa nchini kuna jumla ya wataalam wa maendeleo ya jamii 2,742 walioajiriwa na Serikali kuu na halmashauri. Pamoja na kuwepo kwa wataalam hawa bado kuna upungufu katika Kata nyingi.

Mfano, hadi kufikia Machi, 2013 asilimia 40 tu ya Kata zote Tanzania Bara zilikuwa na angalau mtaalam mmoja wa maendeleo ya jamii kama inavyoelekezwa katika Sera ya Maendeleo ya Jamii. Wizara yangu imekuwa ikihimiza halmashauri na taasisi nyingine kuwaajiri wataalam hao ili kuongeza uhamasishaji wa wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, usawa wa kijinsia ni nyenzo muhimu katika kufikia maendeleo endelevu ya Taifa letu. Naomba kulitaarifu bunge lako tukufu kuwa hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini imeendelea kuboreka. Kwa upande wa uongozi, ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi umeongezeka, mfano idadi ya Mawaziri Wanawake imeongezeka kutoka asilimia 15 mwaka 2005 hadi asilimia 30 mwaka 2012 wakati Majaji wanawake waliongezeka kutoka asilimia 33 hadi 61 katika kipindi hicho.

Aidha, kumekuwepo na ongezeko la uelewa wa masuala ya jinsia katika jamii ambao umechangiwa na uingizwaji wa masuala ya jinsia kwenye sera, mipango, mikakati, miongozo, programu na bajeti za taasisi mbalimbali. Kuwepo kwa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999 kumetoa fursa kwa wanawake kumiliki rasilimali kubwa kama vile ardhi.

Pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto ya kuwepo mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke. Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea na jitihada za kuelimisha na kuhamasisha jamii kuachana na mila zenye kuleta madhara kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, watoto ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa lolote. Ili watoto waweze kukua na kuwa raia wema, wanahitaji kupewa haki zao za msingi ambazo ni pamoja na: Kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kutobaguliwa na kushirikishwa. Serikali imejitahidi kuweka mazingira yanayowezesha upatikanaji wa haki za mtoto ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera ya Mtoto ya mwaka 2008 na kutunga Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009.

Aidha, uanzishwaji wa Madawati ya Jinsia na Watoto katika Vituo vya Polisi nchini pamoja na kutoa mafunzo kwa Polisi kuhusu kusimamia madawati haya kumeongeza ufanisi katika kuchangia upatikanaji wa haki za watoto na wanawake. Juhudi zingine ni pamoja na kuwezesha uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Halmashauri. Mabaraza hayo yanawezesha ushirikishwaji wa watoto katika masuala yanayohusu maendeleo yao.

Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau imebuni na kutekeleza mipango mbalimbali kama vile Mpango wa Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto. Mpango huo unahusisha uhamasishaji wa wazazi kuwapeleka watoto kupata chanjo ya maradhi mbalimbali ya utotoni, lishe bora na upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyotajwa hapo juu, maendeleo ya mtoto bado yanakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, ndoa na mimba za utotoni na ukatili dhidi ya watoto.

Kumekuwepo na jitihada mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kituo cha Huduma za Pamoja (*One Stop Centre*) katika kuhudumia watoto wanaofanyiwa aina mbalimbali za ukatili.

Kituo kimoja cha majaribio kimeanzishwa katika Hospitali ya Amana iliyopo Manispaa ya Ilala. Matarajio ni kuvianzisha katika maeneo mbalimbali hapa nchini kulingana na uwezo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha kuanzishwa kwa Mtandao wa Simu wa Watoto (*Child Helpline*) namba 116 ambao utatumika na jamii kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto na ukiukwaji wa haki za watoto. Aidha, Mkakati wa Jamii wa Kuondoa Tatizo la Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi umekamilika.

Mheshimiwa Spika, wapo viongozi wa ngazi mbalimbali ambao wanashirikiana na jamii kuwezesha watoto hasa wa kike waendelee na masomo kwa kuhakikisha wazazi na wanaume wanaosababisha waache masomo wanadhibitiwa. Naomba kumpongeza Mkuu wa Wilaya ya Handeni Bw. Mhingo Rweyemamu kwa kuanzisha kampeni ya “Niache Nisome” inayofuatilia na kuhakikisha watoto wa kike walioolewa au kuacha shule wanarudi shule na waliohusika wanashitakiwa. Pia nalipongeza Shirika la *Plan International* linaloendesha kampeni iitwayo “Kwa Kuwa Mimi ni Msichana (*Because I am a Girl*)” inayomhamasisha mtoto wa kike adhamirie kukamilisha masomo yake. Nawaomba viongozi wengine wawaunge mkono na kushiriki katika juhudi hizi ili tuweze kupunguza idadi ya watoto wa kike wanaoachishwa shule na mimba za utotoni.

Mheshimiwa Spika, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yana mchango mkubwa katika kuwezesha maendeleo katika nyanja mbalimbali zikiwemo elimu, afya, mazingira, kilimo, ustawi wa jamii, utawala bora, haki za binadamu na maendeleo ya jinsia. Hadi kufikia Machi, 2013 idadi ya Mashirika haya hapa nchini imeongezeka na kufikia jumla ya Mashirika 5,734 ambayo yanafanya kazi katika ngazi za wilaya, mkoa na Taifa.

Kati ya hayo, Mashirika 4,937 yamepatiwa Cheti cha Usajili na mengine 797 yamepatiwa Cheti cha Ukubalifu. Ubadilishanaji wa taarifa zinazohusu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini umeendelea kuimarika ambapo taarifa mbalimbali kuhusu *NGOs* zimekuwa zikipatikana kupitia tovuti ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*http//www.tnnc.go.tz*), benki ya taarifa za *NGOs*, Baraza la Taifa la *NGOs* na Wasajili Wasaidizi wa *NGOs* katika ngazi za Wilaya na Mkoa.

Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto ya kutokuwepo kwa uwazi na uwajibikaji kwa baadhi ya Mashirika hayo hasa kuhusu masuala ya fedha. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inaandaa utaratibu ambao utawezesha Serikali kupata taarifa kuhusu fedha ambazo wafadhili wanatoa kwa *NGOs* ili ziingie kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mapatio ya Utakelezaji wa Mpango wa Mwaka 2012/2013 na Malengo ya mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2012/2013 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Maeneo yaliyotekelezwa ni pamoja na: utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na mafunzo ya maarifa, ujuzi na stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili washiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo.

Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusu ustawi, haki na maendeleo ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/14, maeneo yafuatayo yamepewa kipaumbele: Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika Vyuo Vya Maendeleo ya Jamii na mafunzo ya maarifa, teknolojia sahihi, ujuzi na stadi pamoja na chekechea katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; kuhamasisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vya Maendeleo ya Wananchi kubuni miradi ya kujitegemea; kuendelea kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto; kuwezesha wanawake kiuchumi; na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda inayohusu ustawi, haki na maendeleo ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2012/13 na Malengo ya mwaka 2013/14 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ni chachu ya kuiwezesha jamii kujiletea maendeleo. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu kupitia vyuo vyake tisa vya maendeleo ya jamii iliendelea kutoa mafunzo ya taaluma katika fani za Maendeleo ya Jamii, Maendeleo ya Jinsia na Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Miradi ya Maendeleo katika ngazi za Shahada, Stashahada na Astashahada. Katika kipindi cha mwaka 2012/13, Wizara yangu ilidahili jumla ya wanachuo 5,989 wakiwemo wanaume 2,142 na wanawake 3,847. Wanachuo 139 walidahiliwa katika ngazi ya Shahada ya Kwanza, 1,466 ngazi ya Stashahada na 4,384 ngazi ya Astashahada. Aidha, Wizara yangu ilikarabati majengo matatu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Missungwi yaliyoharibiwa na mvua kubwa zilizoambatana na upepo mkali. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kudahili na kutoa mafunzo hayo. Aidha, itafanya ukarabati wa maktaba, majengo ya utawala na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Mabughai, Mlale na Missungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni muhimu katika kuwawezesha Wananchi kujiajiri na kuajiriwa na hivyo kupunguza umaskini uliokithiri katika jamii. Wizara yangu kupitia vyuo 55, iliendesha mafunzo ya

muda mfupi na mrefu, ndani na nje ya chuo, yaliyolenga kutoa stadi na maarifa mbalimbali. Katika mwaka 2012/13, Wizara yangu iliwapatia mafunzo ya ujuzi na stadi mbalimbali Wananchi 41,681 wakiwemo wanawake 17,959 na wanaume 23,722. Vilevile, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya kiliwezeshwa kuweka miundombinu ya umeme wa jua. Katika mwaka 2013/14, Wizara yangu imepanga kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Katumba, Kilosa, Ikwiriri, Mto wa Mbu, Msaginya, Mputa, Kisarawe, Ilula, Tarime na Musoma. Aidha, Wizara yangu itawezesha uanzishwaji wa vituo vya kulelea watoto katika vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kuanzia mwezi Januari, 2013 Wizara yangu ilianza kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi ambapo jumla ya wanachuo 1,173 walidahiliwa. Vyuo ambavyo vimeanza kutoa mafunzo hayo ni Rubondo, Kisangwa, Handeni, Msingi, Mwanva, Kasulu, Munguri, Chilala, Masasi, Malampaka, Mbinga, Gera, Chisalu, Kiwanda, Mputa, Newala, Njombe, Chala, Nzega, Mamtukuna, Ikwiriri, Katumba, Sengerema, Muhukuru na Sofi. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kudahili na kuimarisha utoaji mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha Wananchi kujiongezea kipato na kuwapunguzia mzigo wa kazi, Wizara yangu kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Maendeleo ya Jamii iliendelea kusambaza teknolojia sahihi kwa Wananchi. Kwa mwaka 2012/13, jumla ya matrekta sita ya kusukuma kwa mkono yalisambazwa katika Vyuo sita vya Maendeleo ya Wananchi vya Msingi, Ulembwe, Chilala, Mputa, Mbinga na Ikwiriri. Aidha, wakufunzi 12 kutoka vyuo hivyo walijengewa uwezo kuhusu matumizi sahihi ya matrekta hayo. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia sahihi kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea na juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi nchini. Katika

kutekeleza hilo, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, iliratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Katika kipindi cha mwaka 2012/13, Wizara ilitoa jumla ya shilingi 48,000,000 kwa Halmashauri sita zilizokamilisha marejesho ili ziweze kutoa mikopo kwa wanawake wajasiriamali. Halmashauri hizo ni Lushoto, Ngara, Siha, Biharamulo, Chamwino na Maswa. Katika mwaka 2013/14, Wizara yangu itaendelea kutoa fedha kwa Halmashauri kadiri zitakavyorejesha ili kuwakopesha wanawake wengi zaidi. Tunazikumbusha Halmashauri zote zinazopata mikopo hii kuchangia asilimia tano ya mapato yao ili wanawake wengi zaidi wanufaike na mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili wa kijinsia bado ni tatizo kubwa hapa nchini. Katika kukabiliana na tatizo hili, Wizara iliendelea kuratibu na kutekeleza mipango na mikakati ya kutokomeza ukatili wa kijinsia. Kwa mwaka 2012/13, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu ukatili wa kijinsia kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Manyara. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Wajumbe 163 wakiwemo wanaume 125 na wanawake 38. Mafunzo hayo yaliwezesha Kamati hizo kuandaa mikakati ya kupambana na ukatili wa kijinsia katika maeneo yao. Vilevile, Wizara iliwezesha Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana kutathmini hali halisi ya ukatili huo katika Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara. Tathmini hiyo ilibaini kuwa ukatili wa kijinsia hususan ukeketaji katika eneo hilo bado unahitaji juhudi za ziada kuweza kuutokomeza. Kwa mwaka 2013/14, Wizara yangu itawezesha shughuli za Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia na Kuondoa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto. Aidha, itazijengea uwezo kamati za kupinga ukatili wa kijinsia katika ngazi za mikoa na wilaya kwenye mikoa minne ya Mbeya, Iringa, Tabora na Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mikataba na Maazimio mbalimbali inayohusu maendeleo ya wanawake na watoto ambayo nchi yetu imesaini na kuridhia, Wizara imeendelea kushiriki katika Mikutano ya Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Hali ya Wanawake, Kikao Maalum cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Mkutano wa Maziwa Makuu

kuhusu Masuala ya Wanawake. Aidha, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Maazimio mbalimbali yanayoafikiwa katika mikutano hiyo. Mojawapo ya utekelezaji huo ni kukamilika kwa uandaaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uingizaji Masuala ya Jinsia kwenye Sera, Mipango, Programu, Mikakati na Bajeti zinazohusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Lengo la mwongozo huo ni kuzisaidia Wizara, Idara, Wakala, Halmashauri, Asasi mbalimbali za Kiraia, Sekta Binafsi na Wadau mbalimbali kupanga na kutekeleza shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia jinsia. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kushiriki mikutano hiyo na kutekeleza Maazimio yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutafakari mafanikio na changamoto zinazokabili jamii, hususan wanawake, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali huratibu Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo hufanyika tarehe 8 Machi, ya kila mwaka. Lengo la Maadhimisho hayo ni kuwakutanisha wanawake ili waweze kubadilishana uzoefu katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili. Katika mwaka 2012/13, Wizara yangu iliratibu Maadhimisho ya Siku hiyo katika ngazi ya mkoa. Kaulimbiu ilikuwa 'Uelewa wa Masuala ya Jinsia katika Jamii: Ongeza Kasi'. Kaulimbiu hii inasisitiza umuhimu wa kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia masuala ya jinsia katika kuleta maendeleo katika jamii. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kuratibu maadhimisho hayo katika ngazi ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine, Wizara ina jukumu la kuwezesha uwepo wa usawa wa jinsia katika jamii. Katika kufanikisha jukumu hilo, Wizara yangu imehimiza uanzishwaji wa Dawati la Jinsia katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, pamoja na Mikoa na Halmashauri. Dawati hilo huwezesha uingizwaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mikakati, Programu, Mipango na Bajeti za Maendeleo. Kwa mwaka 2013/14, Wizara itaendelea na juhudi za kufanikisha usawa wa jinsia katika jamii kwa kudurusu Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); kuwajengea uwezo Waratibu wa Dawati la

Jinsia; kukamilisha na kusambaza mwongozo wa Kitaifa wa Dawati la Jinsia; na kuandaa rejista na vitendea kazi vya kuwezesha uingizwaji wa masuala ya kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ni nguzo kuu katika kuhakikisha kuwa haki za mtoto zinalindwa na kuzingatiwa. Kwa kuliona hilo, mwaka 2012/13 Wizara ilianza kutafsiri Sheria hiyo katika lugha nyepesi na rafiki kwa makundi yote likiwemo la watu wasioona. Wizara yangu iliendesha mkutano kuhusu Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 kwa Makatibu Wakuu ambao ulibaini mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa Sheria hiyo kwa wadau. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Mtoto katika ngazi mbalimbali; kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa Sheria hiyo katika Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora na kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, Wizara imeandaa Mpango wa miaka mitatu wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto (2012/13 - 2015/16). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanzisha Kituo cha Huduma za Pamoja *(One Stop Centre)* kwa ajili ya kuhudumia watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili hapa nchini. Kituo hicho kimeanzishwa kwa majaribio katika Hospitali ya Amana, Manispaa ya Ilala. Aidha, Wizara imekamilisha uanzishaji wa Mtandao wa Simu wa Watoto *(Child Help Line)* Namba 116 ambao utatumika na jamii kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto.

Katika mwaka 2013/14, Wizara itaratibu kikosi kazi kinachosimamia masuala ya ukatili dhidi ya watoto na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Ukatili Dhidi ya Watoto; kufanya mikutano ya kuongeza uelewa wa ukatili dhidi ya watoto katika mikoa mitatu ya Mara, Shinyanga na Singida; kuandaa vitini vya elimu juu ya ukatili dhidi ya watoto vitakavyotumika katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na kuanzisha timu za ulinzi wa watoto katika mikoa 24 Tanzania Bara. Wizara yangu itaendelea kuwatambua na kuwapongeza wadau wanaoshiriki kikamilifu na kutoa

mchango mkubwa katika kufanikisha upatikanaji wa haki za mtoto na kuzuia ukatili wa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa watoto katika maamuzi ni jambo linalopaswa kuzingatiwa katika kuhakikisha haki na maendeleo ya mtoto yanafikiwa. Katika kuongeza ushiriki huo, mwaka 2012/13, Wizara iliwezesha kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ulipitia taarifa za utekelezaji za Mabaraza ya Watoto ya Wilaya na Mikoa pamoja na kuchagua Viongozi wa Baraza hilo. Katika mwaka 2013/14 Wizara itaendelea kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto wanaoishi mitaani ni moja ya changamoto kubwa ambazo Wizara yangu imejizatiti kupambana nazo. Katika mwaka 2012/13, Wizara yangu ilitekeleza mpango kazi wa mwaka mmoja ambao ulihusisha uundaji wa kamati za ulinzi wa watoto katika baadhi ya Halmashauri. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliandaa Mpango Kazi wa miaka mitatu wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto ambao pamoja na mambo mengine, unahusika na uelimishaji umma kwa njia mbalimbali zikiwemo redio, runinga, magazeti na vipeperushi kuhusu tatizo la watoto wanaoishi mitaani. Kwa mwaka 2013/14, Wizara kupitia Kamati za Ulinzi wa Mtoto katika ngazi ya Wilaya, Kata na Kijiji itaelimisha wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa kuhudumia na kuwapatia watoto mahitaji ya msingi kama vile elimu, chakula, mavazi na ulinzi ili kuzuia ongezeko la watoto wanaoishi au kufanya kazi mitaani. Wizara yangu pia kwa kushirikiana na wadau itaanzisha programu ya kujengea uwezo kiuchumi familia ili ziweze kujikimu na kuwahudumia watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, Wizara yangu iliendelea kuziwezesha *NGOs* kutambulika kisheria kupitia usajili chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005. Hadi kufikia Machi, 2013, Wizara ilisajili jumla ya mashirika 443.

Kati ya hayo, mashirika 423 yalipatiwa Cheti cha Usajili na mengine 20 yalipatiwa Cheti cha Ukubalifu. Mashirika haya yanafanya kazi katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa. Katika kipindi cha mwaka 2013/14, Wizara yangu itaendelea na zoezi la usajili wa mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kuratibu na kufuatilia shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini kwa lengo la kuhakikisha kwamba, huduma zinazotolewa na mashirika haya zinaboreka na kuwafikia walengwa. Katika kutekeleza hilo, Wizara iliwezesha kufanyika kwa vikao vitatu vya Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Mikoa ya Mtwara, Njombe na Mwanza. Aidha, Bodi ilikagua shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 22 katika mikoa hiyo, kukutana na wadau 220 na kujadili fursa na changamoto zinazoyakabili Mashirika hayo. Baadhi ya fursa zilizojitokeza kupitia mikutano hii ni kubadilishana uzoefu kuhusu upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Mashirika, namna bora ya uwajibikaji wa Mashirika kwa Wananchi, kuboresha mahusiano baina ya Mashirika na Serikali na kuhakikisha kuwa mipango yao inajumuishwa kwenye mipango ya kazi katika Halmashauri husika. Katika kipindi cha mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kuiwezesha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yake ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni suala muhimu katika kuongeza ushiriki, uwazi na uwajibikaji wa Mashirika hayo hapa nchini. Wizara yangu iliendelea kuboresha Benki ya Taarifa na Takwimu za Mashirika na kuziwezesha taasisi na wadau mbalimbali kupata taarifa hizo kwa ajili ya maamuzi. Wadau 250 walipata taarifa hizo kupitia Ofisi ya Msajili na wengine 3,600 kupitia Tovuti ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(http//www.tnnc.go.tz).* Miongoni mwa wadau walionufaika na taarifa hizo ni pamoja na benki mbalimbali, watafiti kutoka vyuo vikuu, Wizara mbalimbali na Wabia wa Maendeleo. Katika kipindi cha mwaka 2013/14, Wizara itaendelea na zoezi la kuboresha Benki ya Taarifa na Takwimu

za Mashirika kwa lengo la kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinapatikana kwa wakati na zinaendelea kuwa za kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Miradi ya Maendeleo inatekelezwa ipasavyo, Wizara yangu inatoa kipaumbele katika suala la ufuatiliaji na tathmini ya miradi. Katika mwaka 2012/13, Wizara yangu ilifuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika vyuo tisa vya maendeleo ya jamii na vyuo 55 vya maendeleo ya Wananchi. Tathmini hiyo imebaini kuwa miradi mingi ya ukarabati wa majengo na miundombinu haikamiliki kwa wakati kutokana na kutopatikana kwa fedha katika muda unaotakiwa. Kwa mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera na Miradi yake ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/13 Wizara yangu iliendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya haki, usawa, uadilifu, utawala bora na uwazi na kuweka mkazo katika kudhibiti vitendo vya rushwa na uzembe kazini. Masuala haya ni ya msingi katika kuiwezesha Wizara kuwa na watumishi waadilifu na wanaowajibika, wenye ari, moyo na msimamo thabiti kuhusu utumishi wa umma na walio tayari kutoa huduma bora kwa umma wakati wote. Jitihada hizi zitaendelea kusisitizwa katika mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ni muhimu katika kuongeza ujuzi na utaalamu kwa watumishi ili kuwawezesha kupata mbinu za kisasa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika mwaka 2012/13, jumla ya watumishi 152 waliwezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Kati yao, watumishi 99 kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi walipata mafunzo ya ufundishaji mahiri *(CEBET)*, yaliyotolewa katika Chuo cha *VETA* Morogoro. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi wake kupata mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwapatia motisha wafanyakazi, Wizara yangu kwa mwaka 2012/13, imewapandisha vyeo watumishi 48 na kuwabadilisha kazi

watumishi watano. Aidha, watumishi 26 walithibitishwa kazini na watumishi saba waliingizwa kwenye masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni. Kwa kipindi cha mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi wake kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sasa, Wizara yangu imekuwa ikikabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hasa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Nafarijika kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, katika mwaka 2012/13, Wizara yangu imeajiri jumla ya watumishi 58. Idadi hii imesaidia kupunguza pengo kubwa lililopo kati ya mahitaji halisi na watumishi waliopo. Katika mwaka 2013/14, Wizara inatarajia kuendelea kuajiri watumishi wengine ili kuendelea kupunguza pengo lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Wizara yangu imekamilisha ukarabati wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya ofisi kwa kutengeneza maegesho ya magari na kununua jenereta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/13, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha watumishi kuhusu umuhimu wa kupima afya zao. Aidha, iliwawezesha watumishi 11 waliojitokeza kuwa wameathirika na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI kupata viini lishe, dawa na chakula. Huduma hizi zimewawezesha watumishi hao kuboresha afya zao na kuongeza tija katika utendaji wao wa kazi. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi wajitokeze kupima afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Wizara wa mwaka 2012/13 na Malengo ya mwaka 2013/14 yanaonesha jinsi Wizara yangu ilivyo na umuhimu katika kuleta usawa wa jinsia, upatikanaji wa haki na ustawi wa watoto na ongezeko la ajira kwa vijana. Ili Wizara itekeleze vyema majukumu yake inahitaji ushirikiano mkubwa wa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kumshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mb.), kwa ushirikiano, ushauri na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu, Bibi Kijakazi Rajabu Mtengwa; Naibu Katibu Mkuu, Bibi Anna Tayari Maembe; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo; Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania, Bibi Margareth Chacha; Wakuu wa Vyuo; na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wadau wote tunaofanya nao kazi na wengine ambao kwa namna moja au nyingine tunashirikiana. Peke yetu kama Wizara tusingefikia mafanikio niliyoyataja. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Asasi ya Wanawake na Maendeleo *(WAMA);* Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF);* Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP);* Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(TAWLA);* Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania *(TAMWA)*; Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania *(FAWETA); Medical Women Association of Tanzania (MEWATA); White Ribon; Plan International;* Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Napenda pia kuyashukuru Mashirika kutoka nchi rafiki ambayo yameendelea kutusaidia na kufanya kazi na sisi. Mashirika hayo ni pamoja na *DFID; GPE; CIDA; KOICA* na *UK Education.* Aidha, nayashukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni *UNICEF; UNDP; UNFPA* na *UN WOMEN* kwa misaada yao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2013/14, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya

shilingi 23,964,170,000; kati ya hizo Shilingi 14,053,498,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 8,656,002,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 5,397,496,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 9,910,672,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi 4,500,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 5,410,672,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117 (11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niwasilishe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza wajibu wake Kamati ilikutana na watendaji wa Wizara tarehe 28 Machi, 2013 Jijini Dar es Salaam na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na kujadili bajeti iliyohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Aidha, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha unaoisha Juni 30, 2013, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali, hasa kwenye maeneo yanayohusu

kuongeza fedha za ndani kwenye Miradi ya Maendeleo, kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, kuongeza bajeti kwa ajili ya kuimarisha Vyuo vya Maeendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Benki ya Wanawake Tanzania kupanua wigo wa huduma zake hadi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa, ushauri wa Kamati umezingatiwa. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Maeneo Hayo ni pamoja na usawa wa kijinsia na maendeleo ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Tanzania katika usawa wa kijinsia na Maendeleo ya Jamii unaonekana wazi katika Katiba ya nchi yetu na katika uwekaji sahihi na uridhiaji wa mikataba mikuu ya kimataifa inayotoa haki za binadamu na usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona masuala yanayohusu usawa wa kijinsia na Maendeleo ya Kijamii ni masuala mtambuka ambayo hayajapewa uzito unaostahili kwenye mipango ya maendeleo ya Serikali kwani kwa sasa maeneo haya ni viashiria hatarishi kwa ustawi wa wanawake, watoto, amani ya nchi yetu na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Kabla ya kusoma makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, napenda kuyaainisha masuala hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa Sheria na vyombo vya kiutawala, bado matukio ya wanawake kuendelea kuteswa na kunyanyaswa ni mengi mno. Wanawake wanapigwa na kufanyiwa vitendo vya ukatili vinavyopelekea baadhi yao kupata ulemavu wa viungo na wakati mwingine kufa au kupoteza heshima na utu wao, wengine kubakwa na kunyanyaswa kijinsia wawapo kazini, shuleni ama vyuoni. Mambo haya yataendelea kuangaliwa mpaka lini na nini dawa yake? Nani anawajibika kukomesha haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mifano michache kati ya mingi iliyopo, Kamati inaitaka Serikali katika Bunge lijalo kuleta mkakati wenye fedha na rasilimali za kutosha kuondoa matatizo haya. Kamati inasikitika kuona unyanyasaji huu bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa za kijinsia mahali pa kazi na vyuo vya elimu ya juu. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kupambana na rushwa na watuhumiwa wengi kukamatwa na kuchukuliwa hatua, kama Taifa hatujapata kusikia kuwapo kwa kesi zitokanazo na rushwa inayohusu udhalilishwaji kijinsia kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa na malalamiko mengi ya chini kwa chini kuhusu rushwa za ngono hasa kwa watoto wa kike hasa mahali pa kazi na maeneo ya vyuo vinavyotoa elimu ya juu kwenye baadhi ya taasisi. Kamati inaamini Serikali ina mkono mrefu wa kuweza kufanyia kazi tuhuma hizi na kukomesha rushwa ya ngono inayolalamikiwa. Kamati inaishauri Serikali ilifanyie utafiti suala hili ili kuwaokoa watoto wa kike na wanawake waweze kuondokana na unyanyasaji huo. Kamati inashauri Serikali kutengeneza mfumo wa siri wa kutoa taarifa zinazohusu rushwa ya ngono ili kuwaokoa wanawake na watoto wa kike wanapopata matatizo ya unyanyasaji wa kijinsia mahala walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo inaajiri Watanzania takribani asilimia 75 na wengi wa wakulima wa vijijini ni wanawake. Pamoja na kuwa Serikali imeweka mkazo katika kilimo cha umwagiliaji na pembejeo, miundombinu ya kilimo bado siyo rafiki na yenye kuleta tija itakayoweza kumkomboa mwanamke wa kijijini. Wengi wa wanawake hao hali zao za maisha ni duni. Vyombo vya fedha havitoi nafasi kwa wanawake kupata mikopo kwa riba nafuu na hata kama mikopo hutolewa wanawake wa vijijini hawana rasilimali za kuweka dhamana ili kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika, *SACCOS, VICOBA* na vikundi vya kilimo na kibiashara ndiyo mkombozi wa wanawake. Hata hivyo, mifumo hiyo

haijawezeshwa kukidhi haja za wanawake. Eneo hili la kuwezesha wanawake kiuchumi ni la msingi kwani wanawake wengi ndiyo walezi wa familia. Kamati inaiagiza Serikali kupitia upya mifumo ya kuwasaidia wanawake ili wanawake wengi zaidi waweze kuvifikia vyombo mbalimbali vya kuwawezesha kiuchumi. Mpaka sasa ni asilimia tano tu ya wanawake ndiyo wameweza kukopesheka na wamefikiwa na uwezeshaji huo wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua Uzazi wa Mpango ni suala la kiuchumi na lenye kupewa kipaumbele katika juhudi za kukabiliana na umaskini. Katika Mkakati wake wa kupunguza umaskini (MKUKUTA II 2010 - 2015), Serikali imeweka lengo la kupunguza wastani wa uzazi kwa kila mwanamke aliye katika umri wa kuzaa kutoka 5.4 hadi 5.0; vifo vya akina mama vinavyohusiana na uzazi kutoka 454 hadi 265 kwa kila vizazi hai 100,000; na vifo vya watoto wachanga kutoka 26 hadi 19 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2015. Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya III, Julai 2009 na Mpango wa Taifa wa Kutekeleza Huduma za Uzazi wa Mpango *(NFP CIP 2010 - 2015)* unaonesha dhamira ya Serikali katika kuhakikisha huduma za uzazi wa mpango zinaongezeka na kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati hiyo mizuri iliyowekwa na Serikali, Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali katika kumpunguzia mwanamke wa Kitanzania adha ya uzazi wa mara kwa mara, kwani katika kipindi cha mwaka 2012 - 2015, Tanzania inahitaji shilingi bilioni 140 kusaidia kutekeleza uzazi wa mpango kwa wanawake milioni 3.2. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 huduma za bidhaa zinazosaidia uzazi wa mpango zilizopatikana zilikuwa sawa na asilimia 20 tu na huduma hizo zilizopatikana ziligharamiwa na wadau wa maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/ 2014 eneo hili halikutengewa fedha yoyote na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na utegemezi wa fedha za nje, Kamati inaitaka Serikali kusimamia kwa dhati utekelezaji wa sera inayowahakikishia wanawake maskini wa vijijini kupata huduma za uzazi wa mpango na kutoa agizo

kwa Halmashauri zote kuweka huduma za uzazi wa mpango kuwa kipaumbele katika mipango yao ya maendeleo na kutenga bajeti kwa ajili ya huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzazi usio wa mpango unahatarisha afya ya wanawake, unapunguza fursa za wanawake kupata nafasi za kisiasa, kijamii na kiuchumi pale zinapotokea. Kamati inaamini hatua hizo zitamsaidia mwanamke kujikwamua kiuchumi na kukuza Uchumi wa Taifa na kuweza kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI na Jinsia: Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupunguza kuenea kwa Virusi vya UKIMWI, wanawake kwa ajili ya maumbile ya kibailojia wamekuwa wakiathirika zaidi kuliko wanaume. Kamati inaitaka Serikali iwasaidie Wanawake wa Tanzania kupata huduma zinazohusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI katika vituo vilivyo karibu. Hatua hii itasaidia kuwapunguzia mwendo mrefu wa kufuata huduma hiyo na kushindwa kutekeleza majukumu ya kifamilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa watoto siyo tu ukiukwaji wa haki za watoto, bali pia ni ukiukwaji wa Sheria na Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Tatizo la ajira kwa watoto bado ni kubwa kwenye maeneo ya migodini, mashamba ya chai na tumabaku na sehemu za uvuvi. Watoto wadogo wamekuwa wakitumikishwa kwa kulipwa ujira kidogo huku wakikosa haki ya msingi ya kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha asilimia tano ya watoto bado wanatumikishwa katika ajira mbaya. Mbali na watoto kutumikishwa, kuna taarifa za watoto kutoroshwa na kuuzwa nje ya nchi kwa ajili ya kutumikishwa. Tatizo hili ni kubwa na linahitaji hatua za haraka zitakazosaidia kuwanusuru watoto hao. Ili kuondokana na tatizo hilo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza wajibu wake wa kulinda raia wake wakiwemo watoto wanaotumikishwa katika ajira mbaya, kuwarejesha watoto hao kwenye maisha ya kawaida, kuelimisha Jamii kuhusu kuondoa tatizo la

utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari na kuwafikisha mbele ya sheria wale wote wanaoajiri watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kuingiza masuala ya Jinsia katika Sera na Mikakati mbalimbali ya Maendeleo kwa lengo la kufikia usawa wa jinsia. Hadi sasa jumla ya Madawati ya Jinsia 188 yameanzishwa katika Wizara 26, Wakala saba za Serikali, Sekretarieti za Mikoa 21, Halmashauri 133 na Idara inayojitegemea moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuanzishwa kwa madawati hayo, bado hakuna taarifa za uhakika za jinsi madawati hayo yanavyotekeleza wajibu wake. Kamati inaitaka Wizara kuwasilisha mbele ya Kamati utekelezaji wa Dawati la Jinsia mahali pa kazi na kwa wale ambao hawajaanzisha Dawati la Jinsia kwenye maeneo yao ya kazi, Kamati inawataka kufanya hivyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, yenye lengo la kuwalinda watoto dhidi ya ukatili. Utafiti unaonesha zaidi ya watoto milioni mbili ni yatima ambao baadhi yao hulelewa na ndugu na wengine huishia mitaani. Watoto hawa wako kwenye hatari zaidi ya kuonewa, kudhalilishwa na kunyanyaswa. Mfano, hivi karibuni yameripotiwa matukio kadhaa ya watoto kubakwa na walezi, kuchomwa moto, kulishwa vinyesi na walemavu kufichwa kwa kuogopa aibu ya jamii. Kamati inaishauri Serikali kuboresha mfumo wa kuwalinda watoto kwa kuhakikisha polisi, wanasheria, mahakimu, wafanyakazi wa huduma za jamii na kadhalika, wanafunzwa vizuri kuhusu kutumia sheria za watoto na kuwaelimisha wanajamii majukumu yao. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha mara kwa mara inatoa ripoti Bungeni kuhusu takwimu zinazoonesha hali ya watoto walio katika mazingira hatarishi na hatua zilizochukuliwa kwa wote wanaovunja haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lishe bora kwa watoto na wanawake: Utafiti umeonesha kuwa katika kila watoto kumi

wa Kitanzania, watoto watatu hawafikii kiwango cha ukuaji kimwili na kiakili kwa sababu ya kukosa lishe bora (utapiamlo). Hali hii inatokana na sababu kuu mbili; moja ni akina mama kutopata lishe bora wanapokuwa wajawazito na watoto kutopata lishe bora hasa katika miaka miwili ya mwanzo ya maisha yao. Vilevile asilimia kubwa ya vifo vya watoto walioko chini ya umri wa miaka mitano hufariki dunia kwa sababu ya utapiamlo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lishe bora hupatikana kwenye vyakula vitokanavyo na mimea na wanyama kama maziwa, mayai, nyama, siagi, mboga za majani na kadhalika, ambavyo huuzwa kwa bei ghali ambayo Wananchi wengi hasa wa vijijini hawamudu gharama zake. Kamati inaitaka Serikali kukamilisha haraka mchakato wa Sheria ya Virutubishi. Sheria hii itasaidia vyakula vilivyoongezwa virutubishi kupatikana kwa wingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara inatarajia kukusanya fedha kupitia ada za Wanafunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii jumla ya Shilingi 2,093,721,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iweze kutekeleza majukumu yake, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 23,964,170,000; kati ya fedha hizo, Shilingi 14,053,498,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Shilingi 9,910,672,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na bajeti ndogo inayotengwa kwa Wizara hii kila mwaka bila kujali umuhimu wake katika kuimarisha masuala yote yanayohusu maendeleo ya jamii, usawa wa jinsia, haki za watoto na ustawi wa familia. Ni wazi bajeti hii ndogo itaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujadili Bajeti hii kwa kina, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ni ndogo, bado kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hali hii imekuwa ikiathiri Wizara katika kutekeleza majukumu yake na hasa Miradi ya Maendeleo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha uliomalizika, hadi kufikia Desemba 31, 2012, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 3.1 kati ya bilioni 15.6 ilizoidhinishiwa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 20 ya Bajeti yote iliyoidhinishwa. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Miradi ya Maendeleo iliathirika zaidi kwani katika kipindi kama hicho, Wizara ilikuwa imepokea shilingi milioni 200.4 tu kati ya shilingi bilioni 3.4 zilizoidhinishwa na Bunge, kiwango ambacho ni sawa la asilimia 6.9 ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi Miradi ya Maendeleo iliyokusudiwa haitaweza kutekelezwa ipasavyo. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha hadi kufikia tarehe 30, Juni kiasi cha fedha zilizosalia zinapatikana. Aidha, Serikali inaitaka Serikali kuainisha vyanzo vipya vya mapato na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuweza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na siyo kama ilivyo sasa ambapo fedha nyingi za Miradi ya Maendeleo zinategemea kutoka vyanzo vya nje na upatikanaji wake umekuwa siyo wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inabainisha wazi kuwa, umri unaoruhusiwa kuingia katika ndoa ni kuanzia miaka 18 kwa kijana wa kiume na miaka 15 kwa kijana wa kike. Hata hivyo, Sheria hii inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo inamtambua mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18 kama mtoto. Kwa mantiki hii, Sheria ya Ndoa ambayo imekuwepo na kutumika kwa takribani miaka 41 sasa inaruhusu watoto kuingia katika ndoa. Kwa kuwa Tume ya Marekebisho ya Sheria imekwishapeleka mapendekezo ya kurekebisha hiyo Wizara ya Katiba na

Sheria, Kamati inasisitiza kuwa marekebisho ya Sheria hii yafanywe haraka ili kuweza kuwanusuru watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu fulani umasikini na jamii kutotambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike, vimekuwa vikichagiza baadhi ya jamii kuwaozesha watoto wa kike katika umri mdogo ili kupata mali na kama njia ya kuwaondoa katika familia hasa kwa kuwa hawaoni umuhimu wa kuwasomesha. Katika baadhi ya jamii zenye utamaduni huu, wasichana wamekuwa wakifungishwa ndoa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. Kamati inashauri Serikali kuajiri wafanyakazi wa kutosha wa huduma za jamii na washauri nasaha ambao watasaidia kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike na athari za ndoa za utotoni ambazo huchangia kwa kiwango kikubwa vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini elimu ikitolewa kwa jamii husika, kutakuwa na mwamko mkubwa wa kupinga ndoa za utotoni, watoto wa kike wataelimishwa na hatimaye Taifa litakuwa na jamii iliyoelimika. Aidha, Serikali iendelee kuwaelimisha wanawake juu ya sheria mbalimbali zinazotoa fursa kwa wanawake kumiliki ardhi na mali pamoja na sheria zinazowalinda dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendelo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi: Dhana ya teknolojia na jinsia ni mpya lakini ni ya msingi katika kuleta maendeleo ya kijamii, ingawa uhusiano na uwiano wa dhana hiyo unatakiwa kulinganishwa baina ya wanaume na wanawake. Tumeshuhudia kwa kipindi kirefu sasa watoto wa kike kutopenda kusoma masomo ya sayansi na hivyo kulifanya kundi kubwa la wanawake likose upevu wa kuchangia maendeleo ya Taifa lao. Utafiti uliofanywa na Bwana Sakamoto wa Japani, mwaka 1994, ulibaini kuwa uwiano wa matumizi ya kompyuta kwa watoto wa kike na wa kiume ni 1:4. Hii ni dhahiri kuwa, uwiano katika matumizi ya teknolojia baina ya wanawake na wanaume hauridhishi. Kutokana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali iboreshe vyuo vyetu katika nyanja mbalimbali ili kuhakikisha

vinatoa mafunzo bora yanayoendana na teknolojia ya kisasa kwa vijana wetu na hasa wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti inayotengewa Wizara ni ndogo, Wizara iangalie uwezekano wa kuandaa maandiko *(proposals)*, kwa lengo la kutafuta fedha zaidi nje ya Serikali. Hata hivyo, bado Kamati inasisitiza kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha inaitengea Wizara hii bajeti ya kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, ambapo vimefanikiwa kutoa wataalamu 2,630 wa ngazi za Cheti na Stashahada kati ya hao wanawake waliohitimu ni 888 na wanaume 1,742. Kutokana na ongezeko hilo la idadi ya wahitimu itasaidia kuongeza Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo changamoto ya kukosekana kwa Watalam wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali hususan ngazi za kata, haitokani na ukosefu wa wataalam, bali kutokuwepo kwa nafasi za ajira. Kamati inaona suala la idadi ya Wataalam siyo tatizo kwa sababu kwa wastani, wanachuo waliohitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, inazidi idadi ya Kata zote zilizopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na ukosefu wa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Kamati inashauri Serikali kupitia Halmashauri zitenge bajeti kwa ajili kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao pamoja na majukumu mengine, watalazimika kuwaelimisha Wananchi umuhimu wa kushiriki katika shughuli za maendeleo na hivyo kujikwamua na hali ngumu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha utaratibu wa *retention* ambao una lengo la kuhakikisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinapata fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na

kufanyia kazi. Utaratibu huu wa *retention* umeisaidia Wizara kuongeza fedha kiasi cha shilingi 2,093,721,000 kwa mwaka 2013/2014. Hata hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kuhakikisha Bajeti inayotengwa kwa ajili ya vyuo hivi inatosha na inapatikana kwa wakati ili kuhakikisha kuwa vinakuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia pamoja kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitatengewa fedha za kutosha, vitaweza kukarabati majengo na miundombinu ambayo imekuwepo tangu kuanzishwa kwa vyuo hivi takribani miaka 36 iliyopita. Aidha, Kamati inatambua umuhimu wa kuanzishwa kwa elimu ya awali na inapongeza ujenzi wa miundombinu ya elimu hiyo. Pia Kamati inasisitiza suala la ukarabati na utoaji wa elimu ya stadi kazi upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuongeza ruzuku inayopelekwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na pia iboreshe mazingira na miundombinu katika vyuo vilivyopo pembezoni ili kuwavutia walimu na watumishi wanaopangwa kufanya kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilianzishwa mwaka 1975. Tangu kuanzishwa kwake, Vyuo hivi vilikuwa vikipata ruzuku ya Serikali na ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* hadi mwaka 1990 ufadhili wa Shirika hilo ulipositishwa. Tangu wakati huo, fedha ya ruzuku ambayo imekuwa ikitengwa na Serikali kwa ajili ya Vyuo hivi imekuwa ikipungua jambo ambalo limeathiri utendaji na ufanisi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza kukamilika kwa Mpango utakaowezesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vipatavyo 25 kutoa mafunzo ya ufundi stadi *(VETA)* kuanzia Januari, 2013 ambapo kwa kuanzia vijana 1,250 wanatarajiwa kupata udahili. Hii ni hatua muhimu ambayo itasaidia kutoa nafasi kwa vijana ya kujifunza elimu ya ufundi stadi. Hatua hii itasaidia vijana

kupata ujuzi ambao utawawezesha kujiajiri na hivyo kupunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Waziri (TAMISEMI) na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)*, kwa kuandaa Mkataba wa Makubaliano *(MoU)*, ambao unaelekeza *VETA* kutoa ruzuku kwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinavyotoa mafunzo kwa ajili ya kusaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kamati inaitaka Wizara ianzishe utaratibu wa kuwa na takwimu zitakazoonesha vijana waliohitimu katika vyuo hivyo wako wapi na wanafanya nini ili kuelewa namna ya kuwasaidia kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakiongezeka hapa nchini mwaka hadi mwaka. Hadi sasa Mashirika yanayoratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto yamefikia 675. Licha ya kuwa na Mashirika mengi kiasi hiki, ni Mashirika machache ambayo unaweza kuona mchango wake wa moja kwa moja katika kuisaidia jamii hasa katika Sekta za Afya, Elimu, Mifugo, Kilimo, Mazingira na kadhalika. Kwa upande mwingine, kumekuwa na malalamiko kwamba, baadhi ya Mashirika hayo yasiyo ya Serikali yamekuwa yakiwanufaisha walioyaanzisha badala ya kuwanufaisha walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuratibu vyema Mashirika haya, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuteua Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Wilaya na Mikoa ambao watakuwa na wajibu wa kusajili Mashirika hayo. Hatua hii itasaidia kufuatilia kazi za Mashirika hayo katika ngazi husika na hivyo kubaini mchango wake katika jamii kulingana na vibali walivyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara kufanya utafiti ili kuweza kubaini mchango unaotolewa na Mashirika hayo katika kuleta maendeleo ya jamii hususan kwa wanawake na watoto. Aidha, Kamati inatoa angalizo kwa Mashirika yote ambayo hayafanyi kazi kwa nia ya kuleta

maendeleleo na badala yake kujinufaisha wenyewe kuwa iwapo tabia hii itaendelea, Serikali italazimika kuyafunga mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulinzishwa kutokana na Azimio la Bunge lililopitishwa Agosti mwaka 1993 kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) cha Sheria ya *Exchaquer and Audit Ordinance (Cap. 439)* Na. 21 ya mwaka 1961, kama mojawapo ya mikakati ya kuwawezesha wanawake kujiimarisha na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Mfuko huu ni kuwawezesha wanawake wote walio katika Halmashauri kwa kuwakopesha fedha kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na kupambana na umaskini kwa kuunda vikundi na kupatiwa mikopo. Mwaka 2010/2011, Wizara ilianza kutoa fedha za Benki ya Wanawake Tanzania, fedha hizi zinatolewa kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 2010. Mheshimiwa Rais aliahidi kutoa shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 ili zisaidie kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake ingawa kumekuwepo na Mfuko wa Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi kiasi cha shilingi bilioni mbili zimekuwa zinaingia katika Mradi Namba 4943, Kifungu 3001. Namba hiyo ya Mradi ilikuwa ni ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(Women Development Fund - WDF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2005/2006 hadi sasa, Mfuko huu haujawahi kutengewa fedha na Serikali kupitia Hazina na hali hii inasababishwa na baadhi ya Halmashauri kutochangia kikamilifu asilimia tano ya mapato yake kama ilivyoagizwa na Waziri Mkuu mwaka 1995; na katika maeneo ambayo fedha ipo na imekopeshwa kwa vikundi vya wanawake kushindwa kurejesha fedha walizokopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile baada ya kuanza utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutoa shilingi bilioni mbili kwa Benki ya Wanawake namba ya Mradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ikachukuliwa na Mradi wa Benki ya Wanawake. Hatua zote hizi zimekuwa zikiathiri mwenendo na azma ya kuanzishwa kwa Mfuko huu, kwani iwapo hakuna fedha za kutosha na zile chache zinazokopeshwa hazirejeshwi, ni wazi Wanawake wachache tu ndiyo wamekuwa wakinufaika na Mfuko huu na hasa wa maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha malengo mazuri ya Mfuko huu yanafikiwa, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Fedha za maendeleo zilizowekwa katika Fungu Namba 3001, Mradi Namba 4943, mwaka huu ziende katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kupitia Halmashauri zote kama ilivyokuwa mwanzo na kuanzia Mwaka huu wa Fedha, Hazina waendelee kutenga fedha kwa ajili Mfuko huu kila mwaka ili kuwapa uwezo wa kiuchumi wanawake wote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa Wanawake kiuchumi, kwa kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa ajili ya kukuza mitaji ya biashara. Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kutofikiwa kikamilifu katika siku za karibuni hasa kutokana na ukweli kwamba, kiwango cha fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya benki kama sehemu ya kukuza mtaji wake ni kidogo sana ikilinganishwa na matarajio ya awali. Wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, akielezea madhumuni ya kuanzishwa kwa Benki hii alisema Serikali itatoa jumla ya shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kuiwezesha benki hii kuimarika kimtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Benki ya Wanawake kupokea mtaji wa shilingi bilioni mbili kutoka Serikalini, Benki pia inalazimika kuchukua amana toka

mashirika makubwa ili kukidhi mahitaji yake. Hata hivyo, Benki imeweza kufanikiwa katika maeneo kadhaa; mfano, imeweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 14.5 mwaka 2012 toka milioni 298 mwaka 2009. Aidha, amana za wateja zinaongezeka na kuna ongezeko la utoaji wa mafunzo kwa vikundi mbalimbali vya Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani. Benki pia inatarajia kuanzisha huduma ya *Western Union Money Transfer Bank* na mtandao wa *SWIFT Society for World Interbank Financial Telecommunication.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, Benki haijaweza kufungua Matawi katika maeneo mengi nchini, zaidi ya Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani na hivyo kuwanyima fursa wanawake wengine hasa katika miji midogo na vijijini; Tanzania Bara na Visiwani, kufikiwa na huduma hizo za kifedha iwe kupitia Benki ya Wanawake au Mfuko wa Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Benki hii na kwa kuwa Benki ya Wanawake Tanzania sasa imeshapevuka kwa kiasi cha kutosha kufikia hatua ya kujitanua nje ya nchi, Kamati inaomba Serikali itenge fedha zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais, shilingi bilioni mbili katika kifungu kitakachokuwa na namba inayojitegemea ndani ya Idara ya Jinsia ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kwa kuwa, fedha ya ahadi ya Rais shilingi bilioni mbili inaonekana katika Kifungu Namba 3001 cha Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2013/2014, Kamati inashauri fedha hizo ziende kufufua Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaitaka Serikali itafute fedha nyingine kufidia ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais. Kwa kuwa, Benki ya Wanawake imesharuhusiwa kujiendesha kibiashara na Benki Kuu, Kamati inaishauri Benki ya Wanawake Tanzania iuze hisa zake ili kuongeza mtaji utakaosaidia kuweza kufungua matawi na kutimiza azma ya Serikali ya kuwawezesha kiuchumi Wanawake wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Benki ya

Wanawake Tanzania, imeandaa Rasimu ya Mpango wa Biashara wa Miaka Mitatu (2010 hadi 2013), ambao unalenga kufungua Matawi ya Benki mikoani. Kamati inaishauri Wizara kuanza kutekeleza Mpango huo ili huduma zitolewazo na Benki hiyo ziweze kuwafikia watu wengi hasa wanawake ambao wamekuwa wakisubiri kwa hamu kupata huduma za Benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuwatumia wanahisa katika kukuza mtaji wa Benki ya Wanawake, kwani utegemezi wa fedha za Serikali pekee unaifanya Benki hiyo kuendelea kusuasua. Iwapo mazingira yataandaliwa kwa wanahisa kushirikishwa kuchangia, ni wazi kuwa mtaji wa Benki utakua kwa haraka na kuiwezesha kujiendesha kibiashara tena kwa faida. Hata hivyo, Kamati inashauri watendaji wa benki wawe wabunifu ili kukuza mtaji wa Benki badala ya kusubiri mtaji wa Serikali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA) umebainisha watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi *(Orphans and Vulnerable Children)* kuwa miongoni mwa makundi yaliyo katika hali mbaya. Aidha, Ripoti iliyozinduliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mwezi Agosti, 2011 kuhusuiana na utatafiti wa ukatili dhidi ya watoto nchini, imetoa taswira ya awali kuhusiana na ukubwa wa tatizo la ukatili wa kimwili na kiakili ambalo linawasibu watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara hii kwa kutumia matokeo hayo ya awali ya Ripoti hiyo kuandaa miongozo na kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009, kuandaa zana za ushiriki wa watoto *(Child Partcipation Toolkit)* pamoja na Rasimu ya Mkakati wa Taifa wa Ushiriki wa Watoto ambavyo vyote vinalenga kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa kumshirikisha mtoto katika mambo yanayomhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 ni kuhakikisha Watoto

wote wanastawi na kuwa na maisha bora kwa kupatiwa haki zao za msingi ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kulindwa na kushiriki katika mambo yanayowahusu bila ubaguzi wa hali yoyote. Kamati inapenda kutoa ushauri ufuatao:-

- Halmashauri zote zifuate na kuzingatia sheria ndogo zinazohusu watoto ili kuwapatia haki zao za msingi kama ilivyotajwa hapo juu ili kupunguza wimbi kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na katika Halmashauri ambazo watoto wataendelea kuonekana wanazagaa mitaani bila uangalizi wa Halmashauri husika. Halmashauri hizo zichukuliwe hatua kwani suala la kuwalinda watoto ni wajibu na si hiyari.-Wizara iendelee kuhimiza na kuweka msisitizo wa utaratibu huo ambao wameuanzisha wa kuielimisha jamii kuhusu utoaji wa chakula cha mchana shuleni ili kuwafanya watoto wapatiwe haki yao ya kusoma vizuri na kuepuka kulaghaiwa kwa kupewa chakula na vitu vingine vidogo. Maeneo ambayo utaratibu huu umeanza, yameonesha mafanikio makubwa na hata ufaulu wa watoto unaongezeka.

- Pamoja na Serikali kufanya utambuzi katika Halmashauri 95, ambapo watoto 849,051 wametambuliwa wanaishi katika mazingira hatarishi wakiwemo wasichana 407,544 (48%) na wavulana 44,507 (52%); Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kuimarisha mifumo ya kijamii ya kutunza watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi, ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuanzisha vituo vya mfano ambapo watoto watakusanywa na kupatiwa huduma za msingi kama suluhisho la muda mfupi na wakati huo familia na koo husika zipatiwe elimu kuhusu kuwahudumia watoto wanaoishi katika maeneo yao.

- Kamati inaendelea kutilia mkazo kuwa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuangalia namna nzuri ya kuhakikisha Mabaraza ya Watoto yanatambulika na kupata nguvu ya kisheria ili yaweze kutimiza wajibu wake kikamilifu. Mabaraza haya yameonesha mafanikio makubwa katika sehemu ambazo yameshaanza na hivyo kuweza kusaidia kubaini matatizo ya watoto walipo.

Hata hivyo, bado Mabaraza hayo hayana nguvu ya kutosha kisheria.

- Kwa kuwa tatizo la watoto wa mitaani linaendelea kushamiri katika miji mbalimbali hapa nchini, ni vyema Wizara ikalitambua kuwa miongoni mwa vipaumbele vyake. Wizara inaweza kukabiliana na tatizo hili kwa kushirikiana na Halmashauri husika kuanzisha vituo vya mfano ambavyo vitawakusanya na kuwatunza watoto hawa kwa kuwapatia mahitaji muhimu na kulinda haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia katika kutekeleza majukumu yako. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara kwa kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto - Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba (Mb); Naibu Waziri - Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mb); Katibu Mkuu wa Wizara – Ndugu Kijakazi T. Mtengwa; Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Anna T. Maembe na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano wao mkubwa wakati tunatekeleza majukumu ya Kamati. Ninawatakia mafanikio zaidi katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed, Mheshimiwa Nasib Suleiman Omar, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo, Mheshimiwa Capt. John

D. Komba, Mheshimiwa Salum Halfan Barwany, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Jaddy Simai Daddy, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Joshua Nasari na Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, akisaidiwa na Katibu wa Kamati, Ndugu Happiness C. Ndalu, kwa ushauri wa kitaalam kwa Kamati na pia kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na ninaomba kuwasilisha.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA (K.n.y. MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumwendeleza mwanamke ni kuiendeleza jamii. Ni wazi kuwa jamii nyingi za kiafrika, mwanamke ameendeelea kukumbana na changamoto nyingi. Kutokana na ugumu wa maisha, Wanawake wa Kitanzania wameendelea kuumia, kuteseka na kudhalilika hasa pale inapokuja suala la kutetea haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka 30 sasa imepita tangu Kongamano la Kwanza la Wanawake la Dunia lifanyike Jijini Mexico na miaka 17 tangu Mkutano wa Beijing ufanyike. Asilimia kubwa ya Wanawake wa Kitanzania wamebaki katika mapambano ya kukabiliana na changamoto za kijamii, kisiasa na kiuchumi hasa linapokuja suala la kufanya maamuzi, uwakilishi wa kisiasa, kushika nafasi za juu kitaaluma na nafasi yao ya ujumla katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, sehemu ya pili inayohusu haki na ustawi wa mtoto (a), kipengele cha 4 – 14, inataja haki za mtoto kuwa ni pamoja na kulindwa dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote, haki yake kupata chakula bora, malezi bora, huduma za afya, elimu, uhuru wa kuamua, kucheza na kupumzika. Pia, sheria hiyo inataja majukumu ya mzazi kwa mtoto kuwa ni pamoja na kuhakikisha mtoto wake anaishi, anathaminiwa, anaheshimiwa, anapata muda wa kupumzika. Nyingine ni kumlinda dhidi ya mateso, vurugu, uonevu, ukatili au kupata madhara kimwili au kisaikolojia. Pia, mtoto ana haki ya kutoa maoni, kusikilizwa na kuheshimiwa katika uamuzi unaomhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watoto wa mitaani limekuwa kubwa katika nchi hii. Jamii zetu hasa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Dodoma, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro na Mji Mkongwe Zanzibar, limekuwa likishika kasi huku kukiwa na jitihada chache za kukabiliana kwa dhati na tatizo hili. Hivi karibuni Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* lilitoa ripoti ya mwaka 2012 kuhusu hali ya watoto duniani ambayo inaonesha kuwa umaskini unazidi kukua katika miji na inaonekana hali za vijijini na mijini zinaanza kufanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa kwa Taifa ni kuhakikisha kundi hili linakuwa la manufaa kwa mwendelezo wa Taifa hili. Tatizo la watoto wa mitaani limeongezeka huku likijenga mazingira hatarishi kwa watoto hawa ambao tunasema ni hazina ya Taifa. Taarifa mbalimbali za vyombo vya habari pamoja na utafiti wa taasisi mbalimbali vinaonesha kuwa, watoto wa mitaani wanakumbwa na adha kubwa ikiwemo ukosefu wa malazi, hali inayopelekea wengi wao kubakwa na pia kulawitiwa. Zipo pia taarifa kuwa watoto hawa wanatumika katika biashara haramu ya madawa ya kulevya, hali inayowaweka watoto wenyewe kuwa watumiaji wa madawa ya kulevya, mangali na umri mdogo na hivyo kuhatarisha makuzi yao kiafya, kisaikolojia na hata kielimu. Aidha, watoto pia wanatumika katika biashara ya ngono, hali inayowaweka katika hali ya kushiriki

katika ngono zembe, kuwaweka katika nafasi kubwa ya kuambukizwa Virusi vya UKIMWI. Vitendo hivi ni hatarishi kwa afya za watoto hawa na kwa kuwa watoto wengi wanaoishi mijini wanaishi katika mazingira ya umaskini, njaa na manyanyaso ya kijinsia na kwamba wapo katika hati hati ya kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI kuliko wenzao wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira magumu *(Most Vulnerable Children)* ni la muda mrefu katika nchi yetu. Wapo ambao wapo mitaani kwa sababu tu ya kukosa malezi yanayofaa katika familia zao, aidha, kwa wazazi kutoa adhabu chungu za kuumiza zisizomfunza wala kumsaidia mtoto, wapo wasioridhika tu na maisha katika familia zao, wanaopenda kuishi maisha ya uhuru zaidi kama wanavyodai, wapo pia wanaosukumwa mtaani na hali ya mifarakano katika kaya, hasa katika mahusiano ya wazazi, yaani baba na mama, hali inayoashiria kuwa hatuwezi kuzungumzia kujenga msingi imara wa haki za mtoto bila kuhusisha kujenga msingi wa kimaadili katika mahusiano bora kwa ngazi ya familia na kusisitiza weledi katika malezi. Kundi kubwa, ni la hawa ambao hali ya uchumi katika familia zao ni ngumu na hawana uhakika wa kuishi kesho, hivyo wanaona afadhali waingie mtaani kujitafutia namna toka kwa wasamaria wema. Katika kundi hili la hali ngumu ya uchumi, wapo wanaotoka na wazazi na wapo wanaotoka peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fikra zao, mijini ndiko kuliko na maisha bora na wanapowaza kuhamia mijini, suala la makazi kwao siyo kipaumbele. Kipaumbele ni kwamba, tayari yupo mjini na atapata ahueni ya maisha. Wanafanya haya bila kujiuliza athari zitokanazo na kuwepo katika mazingira mapya usiyo na makazi na matokeo yake ni vitendo hivyo tunavyovishuhudia. Inasikitisha, lakini pia inatukumbusha kuwa tunatakiwa kuliangalia tatizo katika mizizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutafuta majibu yanayosabisha msukumo wa watoto kukimbia kutoka vijijini

na kuja mjini ni mojawapo ya nia ya dhati ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili. Kiwango cha umaskini na uduni wa huduma za kijamii maeneo ya vijijini linatakiwa liangaliwe kwa mapana yake. Aidha, uwekezaji katika elimu, ambayo si bora elimu bali elimu bora yenye uwiano wa usawa kati ya mijini na vijijini, pamoja na kuendeleza fursa ya kuinua kipato kwa rika la vijana ni baadhi ya hatua zinazoweza kupunguza nguvu ya msukumo wa kukimbilia mijini kwa watoto na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa kuna Mashirika mengi yasiyo ya Kiserikali na Vituo mbalimbali vilivyosajiliwa vinajihusisha na huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, ikiwa ni pamoja na kutoa misaada kwa watoto hawa wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kwa kupitia Wizara hii, kutueleza kama imefanya sensa na kujua idadi rasmi ya watoto wa mitaani katika Taifa hili. Pia, Serikali ituambie inawezaje kufanya mipango ya kukabiliana na tatizo la watoto wa mitaani bila ya kuwa na takwimu sahihi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali kubwa ni kuwa, huku kukiwa na ongezeko la wimbi la watoto wa mitaani pamoja na ongezeko kubwa la mashirika yasiyo ya kiserikali na vituo hivyo kila kukicha; je, ni watoto wangapi wa mitaani mpaka sasa walioweza kusaidiwa? Je, ni kweli nchi hii ni maskini wa kutupwa kiasi cha kushindwa kuwasaidia watoto hawa ambao ni hazina inayoteketea? Kukosekana kwa majibu ya maswali haya ni kielelezo cha upungufu katika mfumo wetu wa utoaji huduma, lakini pia ukusanyaji wa takwimu zinazohusu haki za Watoto Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo niliyoyaainisha juu yanaleta taswira kuwepo kwa tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira magumu, ni ajira ya watu fulani na jitihada yao kubwa ni kwamba, hili linakuwa ni tatizo la kudumu kwa nchi yetu, ili ajira yao isikome. Hawa wametumia watoto wa mitaani kama kigezo cha kuomba fedha kwa wafadhili na kujinufaisha wao na si watoto. Pia inawezekana katika Wizara

hii tatizo hili linatumika kama chambo cha kujichotea fedha kupitia bajeti kwa kuwasaidia watoto hawa, lakini kila mwaka zikaishia katika mikono ya watu wachache, wajanja wanjanja kwa kukosekana kwa takwimu rasmi. Hii ni ishara pia kuwa Sera za Serikali katika eneo hili zimeshindwa kuleta matokeo yaliyokusudiwa aidha kwa sababu ni Sera mufilisi au kuna upungufu mkubwa katika miundombinu ya utekelezaji wake au zinaimbwa tu huku kukiwa hakuna nia ya dhati ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ni suala zito la haki za binadamu, jamii na afya ya jamii nchini Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingi duniani. Vitendo hivi vinamomonyoa msingi imara ambao watoto wanahitaji ili wawe na afya bora na maisha yenye tija na vinasigana na haki ya msingi ya watoto ya kuishi salama utotoni. Tatizo la ukatili wa kijinsia, ambalo ndilo hasa linalozungumziwa na Utafiti wa 2009 juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania ni zito sana. Kuainisha aina zote za vitendo vya ukatili (kijinsia, kimwili na kiakili) na sababu zake ni hatua muhimu kuelekea kwenye kubuni mikakati na Sera za Kitaifa zinazohusisha sekta mbalimbali za kuzuia na kukabiliana na tatizo hili na kuwalinda vizuri zaidi watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili dhidi ya watoto umeendelea kila kukicha na vyombo vya habari vimekuwa mstari wa mbele kuripoti ukatili huo kila unapotokea huku Serikali ikikaa kimya bila ya kukemea hadharani na kwa nguvu vitendo hivyo mara vinapotokea. Kuna matukio mengi ya ukatili dhidi ya watoto ambayo yameripotiwa toka mwaka huu uanze vikiwemo ulawiti, ubakaji, mateso ya mwili (yenye athari kiakili). Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua watuhumiwa wa vitendo hivi vya ukatili dhidi ya watoto wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la hivi karibuni la mtoto wa miaka minane anayesoma darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Mkundi, Mkoani Morogoro, alidaiwa kubakwa na baba yake mzazi, Venance Mbui (41), baada ya kugunduliwa na mtoto wake mwingine ambaye ni mlemavu. Bado matukio

kama haya yameendelea kuripotiwa kwenye vyombo vya habari na sasa yameanza kuzoeleka kama ya kawaida. Huko Kizumbi, Manispaa ya Shinyanga, mtoto wa kike wa miaka saba alitobolewa na kuingiliwa kinyume na maumbile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ni magumu kuyatamka lakini kwa kuwa Taifa limefika hapa lilipo ni lazima tuseme wazi na hadharani, kwa kuwa yanasikitisha, yanalitia doa Taifa na yanaumiza mno. Katika Mji Mdogo wa Mbalizi, Askari Polisi aitwaye Zungu, ametuhumiwa kumbaka mtoto wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Swaya Ntokela, Wilayani Rungwe. Huko Mpwapwa, mtoto wa siku 45 alifanyiwa unyama na babu yake mwenye umri wa miaka 61 kwa kuingiliwa kimwili hivyo kuwa katika hali mbaya ya kiafya. Kama Taifa, tunaendelea kukaa kimya bila kukemea mambo haya; tunaelekea wapi? Kama Taifa, tumeshindwa kubadilisha Sheria zetu katika kusimamia na kulinda haki za watoto kwa kuweka adhabu kali hata za kifo kwa watu wanaotenda unyama na ukatili huu? Hoja ya msingi hapa ni je, Jeshi la Polisi liko wapi? Watendaji wa Wizara wako wapi? Ustawi wa Jamii uko wapi? Wajibu wetu kama Taifa umeishia wapi? Lazima Serikali, iwalinde watoto na kukemea kwa nguvu zote matukio haya ya kinyama na ya kikatili pamoja na kuwachukulia hatua kali watuhumiwa ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanaosoma shule za kutwa wamekuwa wakikumbwa na adha kubwa ya usafiri kwa watoto wa mjini na kutembea umbali mrefu kwa watoto wa vijijini na wamekuwa wakitumia muda mwingi katika vituo vya usafiri au kutembea kutoka nyumbani kwenda shuleni na kurudi. Watoto hawa hukumbwa na kadhia za utingo wa daladala kuwanyanyasa na hivyo kupoteza hata zaidi ya saa mbili katika vituo vya mabasi. Pamoja na kuwa Serikali ya CCM imeendelea kujigamba kwa kuongeza shule, mazingira anayopitia mtoto wa maskini ni ya kukatisha tamaa na yenye kuchosha, hali inayofanya watoto hawa kutokuwa na morali au tashwishi ya masomo kwa kuwa kuna siku ambazo huchelewa baadhi ya vipindi vya masomo kutokana na tatizo la usafiri. Aidha, ongezeko la nauli kwa wanafunzi toka shilingi

100 kwenda shilingi 200 limeleta changamoto kubwa katika malezi, ukizingatia kuwa familia nyingi za Kitanzania zinaishi katika mazingira magumu. Lazima Serikali ifanye utaratibu wa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanatafutiwa ufumbuzi wa usafiri ili kulinda ustawi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa mstari wa mbele katika kutetea ustawi na maendeleo ya Taifa hili. Pamoja na kubezwa tunakokushuhudia sasa, tutaendelea kuishauri Serikali katika kuleta maendeleo ya kila Mtanzania kwa sababu Tanzania ni yetu sote na ni wajibu wa kila mmoja wetu, kutetea maslahi ya Taifa letu. Hivyo, katika kutatua tatizo hilo, njia bora ya kushughulikia tatizo hili ni kuhakikisha kuwa, familia wanazotoka zinawezeshwa na kuwa na maisha ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litawezekana ikiwa Wizara husika itafanya upembuzi yakinifu na kuwa na idadi halisi ya watoto na kufanya matumizi sahihi ya fedha inayotengwa kila mwaka, kwa kujenga uwiano bora unaolenga kupunguza rasilimali kuishia kwenye michakato ya taratibu za kiutawala kama kulipana posho na warsha katika ngazi ya Taifa na kwenye Halmashauri zetu na badala yake rasilimali hizi zilenge kufikia ngazi ya kaya ambamo watoto hawa wanapatikana. Hili litawezekana iwapo Serikali kwa kushirikiana na wadau wote itajikita katika kuangalia namna bora ya kujenga mfumo wa hifadhi ya jamii yenye taswira ya haki ya mtoto Tanzania. Pili, misamaha hii ya kodi ya hovyo na ukwepaji unaofanywa, ukidhibitiwa vyema na fedha yake ikaelekezwa kuwasaidia kwa dhati Watanzania, tatizo hili litabaki kuwa ni historia. Vinginevyo, haya yasipofanyika, litakuwa ni historia kwamba ni tatizo lililoishinda Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kambi Rasmi kwenye kupunguza ukatili dhidi ya watoto. Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na ushauri wa wataalamu hasa kwa kuzingatia tafiti mbalimbali katika kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto kwa kutambulisha na kuanzisha mikakati yenye

vigezo na vipimo ya kuzuia na kukabili ukatili dhidi ya watoto ndani ya jamii, pamoja na kuanzisha na kutathmini gharama za mifumo ya ulinzi wa watoto katika Halmashauri nchini. Vilevile, kubuni na kutekeleza kampeni ya kuhabarisha umma inayowalenga watoto wakubwa na vijana ili kuwafungulia njia za kutoa taarifa na inayoonesha mikakati ya kuwasaidia watoto na vijana kupata habari na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, itenge fedha za kutosha katika bajeti kuhakikisha haki za mtoto zinaheshimiwa kikamilifu. Serikali ya Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimekuwa katika mstari wa mbele katika Ukanda wa Afrika kufikia makubaliano ya kutenga kasma ya kutosha kulingana na viwango vilivyowekwa kwa ajili ya bajeti inayoenda kuhudumia Watoto hasa katika Sekta ya Afya na Elimu. Hivyo, hamna budi kwa Serikali kujikumbusha juu wa wajibu ambao imeshiriki yenyewe kuutamka kuhusu kiwango stahili cha bajeti.

Pili, utengaji huu wa bajeti uambatane na kutengeneza mifumo na miundombinu ya kitaasisi, kisheria na kisera ya kuwezesha utekelezaji wa haki za mtoto Tanzania. Pia zitengwe rasilimali za kuandaa tafiti za maoni na uzoefu wa watoto na watu wazima katika mahusiano ya shari na amani na kuyajumuisha haya kwenye programu ya uhabarishaji jamii ili kupambana na matumizi ya ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali iandae mikakati endelevu ya kusaidia na kuyaratibu mashirika yanayoshughulika na ustawi wa watoto, ikiwa ni pamoja na kujenga ushirika wenye ulinganifu na mashirika haya pamoja na wadau wengine kama vile sekta binafsi ili kutokomeza ukatili dhidi ya watoto pamoja na kuhakikisha kwamba, watoto wenyewe wanashirikishwa katika kufuatilia na kutolea taarifa tabia na desturi zenye madhara kwenye jamii zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekuwepo na taarifa zinazojirudia rudia zihusuzo mauaji ya vikongwe hususan wanawake katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mara nyingi

mauaji haya huhusishwa na imani za kishirikina na kwa bahati mbaya, walengwa zaidi ni akina mama wenye umri mkubwa ingawa hata wanaume wazee nao pia huuawa lakini si kama ilivyo kwa akina mama vikongwe.

Mauaji kama haya yamekuwa yakisababisha huzuni kubwa kwa familia husika na kulitia aibu Taifa katika jamii ya Kimataifa. Ikumbukwe kwamba, wanaouawa ni wazee ambao bila shaka huacha familia zao zikiteseka. Takwimu zilizotolewa na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali zinaonesha kuwa zaidi ya wazee 6,000 nchini wameuawa kwa imani za ushirikina tangu mwaka 1998 hadi Juni mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezakani watu waendeshe mauaji dhidi ya vikongwe kwa miaka yote hiyo na wakaachwa wakitanua tu mitaani pasipo kukamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria. Kila binadamu anayo haki ya kuishi na kwa msingi huo, hakuna mtu yeyote mwenye haki ya kutoa uhai wa mwenzake na inapotokea hivyo, basi anapaswa ashughulikiwe kikamilifu kulingana na sheria za nchi. Tunatoa wito kwa vyombo vya usalama kujipanga ipasavyo kuhakikisha kwamba, mauaji ya vikongwe katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa yanakomeshwa haraka iwezekanavyo ili watu wanaofanya unyama huo watambue kwamba, Tanzania inajali na kuheshimu uhai wa kila mtu. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mikakati ya Wizara katika kukabiliana na ukatili dhidi ya wakongwe na hatua za kisheria ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kufuatilia na kuwatia hatiani watuhumiwa wa mauaji na udhalilishaji wa vikongwe hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mipango yake ya ushirikishaji wa jamii kwenye masuala yanayohusu maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, Serikali na wadau mbalimbali wamekuwa wakiwaacha wanaume kwa kiwango kikubwa huku nao wakiwa ni sehemu muhimu ya kuleta mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea ukatili dhidi ya watoto, ubakaji, ulawiti, unyanyasaji dhidi ya wanawake, mauaji ya watoto wenye ulemavu, utelekezwaji wa familia nchini, kwa kiasi kikubwa umechangiwa na wanaume. Wanaume wameachwa nyuma lakini kwa kiasi kikubwa wamechangia kuporomoka kwa maadili. Sasa Serikali inapoandaa mikakati yake bila kuweka mipango madhubuti kwa ajili ya kuwashirikisha wanaume katika kuleta mabadiliko ya kweli katika jamii, basi ni wazi vita ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto itakuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali kwa kupitia Wizara iweke mpango mkakati endelevu utakaokuwa na mtandao wa kuwashirikisha wanaume kama wadau muhimu wa kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Lazima Serikali iandae mpango wa kuwashirikisha wanaume katika fursa, warsha, mafunzo na nafasi mbalimbali zenye kuwaelimisha kuwa vileta mabadiliko katika jamiii yetu. Hii kwa kiasi kikubwa itapunguza miguno toka kwa wanaume kuwa wanapuuzwa linapokuja suala la kujadili changamoto za kijinsia na jinsi ya kuzikabili kwa pamoja kama Taifa. Ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa mwaka huu wa fedha, jambo hili linatiliwa mkazo kwa ajili ya mabadiliko ya kweli ya Jamii ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezuka Mashirika mengi yasiyo ya Kiserikali pamoja na vituo vingi ambavyo vimesajiliwa kwa mgongo wa kuwasaidia watoto yatima. Ila kwa ukweli halisi na tafiti zilizopo ni kuwa, baadhi ya *NGOs* na vituo hivyo, vinatumia mwanya huo ili kuweza kuepuka kulipa kodi na kujipatia misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vituo ambavyo vimeanzishwa kwa ajili ya kulea watoto yatima, vimegeuzwa kuwa chanzo cha kujipatia kipato kwa wamiliki na ndiyo maana baadhi ya vituo vimekuwa vikijikusanyia watoto wa mitaani na wasio yatima na kuwaweka vituoni mwao kwa minajili ya kupata misaada mbalimbali kwa njia ya udanganyifu. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mpaka sasa ni vituo vingapi vimesajiliwa kwa ajili ya kulelea watoto

yatima na taarifa za kiukaguzi za mara kwa mara kwa vituo hivyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka pia kufahamu idadi ya vituo na *NGOs* ambazo mpaka sasa zimefungiwa kwa kushindwa kukidhi vigezo na mahitaji na wamiliki wake wamepewa adhabu gani ili kuweza kudhibiti uanzishwaji holela wa vituo na *NGOs* kwa manufaa yao binafsi? Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ishirikiane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhakikisha kuwa taarifa hizi za uratibu wa *NGOs* na Vituo vya kulelea Watoto zinapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni mojawapo ya Sera zilizoandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali kuhakikisha kuwa wanawake kwa wanaume wanashiriki katika shughuli za maendeleo. Sera hiyo imetokana na urekebishwaji wa Sera ya awali ya Wanawake katika Maendeleo ya Mwaka 1992 inazingatia jinsia kwa kuangalia mahitaji ya wanaume na wanawake kwa kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba, kuna ushirikiano wa kutosha kati yao. Lengo kuu la Sera hiyo ilikuwa ni kusawazisha tofauti zilizopo kati ya wanaume na wanawake ili kuweka mazingira mazuri yatakayowawezesha kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kushirikiana. Asasi mbalimbali zisizo za Kiserikali zimekuwa mstari wa mbele kutoa huduma muhimu za kuleta maendeleo ya jamii kwa kuzingatia Sera hiyo. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa Sera hiyo, wanawake bado wanakabiliwa na vikwazo, matatizo na majukumu mengi ya kifamilia yanayowafanya wabaki nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa ukosefu wa elimu, mila potofu pamoja na mfumo dume, vinachangia baadhi ya wanawake kushindwa kujikwamua kiuchumi kutokana na baadhi ya jamii kuamini hawawezi kuongoza mambo mbalimbali. Kwa mfano, wanawake wengi nchini wanakosa haki zao za mirathi kutokana na kuendekeza mila na desturi potofu zikiwemo sheria za kidini ambazo zinawakandamiza. Kwa kuwa sheria za kimila na kidini zinasababisha wanawake kukosa haki zao, umefika wakati

sasa kwa Serikali ishirikishe zaidi Taasisi na Mashirika mbalimbali kuhakikisha kuwa tunaondokana na unyanyasaji huo wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu limejengwa kwa misingi ya kuthamini utu na kulinda heshima ya jamii nzima dhidi ya vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake. Siku za karibuni kumeibuka aina mbalimbali za vitendo vinavyofanyika katika sehemu za wazi za starehe ambazo zipo karibu kabisa na makazi ya watu. Baadhi ya matendo hayo ni pamoja na matamasha maarufu kama 'Kanga Moko-Laki Si Pesa', Kibao Kata na Baikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchezaji wa nyimbo ambao si tu unadhalilisha utamaduni wa Kitanzania bali pia unadhalilisha thamani ya mwanamke, ambapo wanawake wanaocheza huvaa kanga moja zilizotiwa maji bila ya kuwa na nguo nyingine za kuwasitiri. Wengi wetu ni mashahidi kuwa vitendo hivi hufanyika katika baa na sehemu za starehe ambazo zipo katika maeneo ya makazi ya watu.

Pamoja na kuwa zinadhalilisha wanawake, lakini pia inaleta taswira mbaya kwa watu wa rika mbalimbali za kijamii kutokana na aina ya uchezaji. Je, vitendo kama hivyo vinatusaidia nini? Je, kama ni ajira kwa wanawake, inamaanisha kumdhalilisha mwanamke hata kama ni kwa ridhaa yake? Je, tunafundisha nini watoto wetu na jamii yetu kwa ujumla juu ya thamani ya mwanamke na umuhimu wa watoto wengine wa kike kusoma kwa kufuata Sheria na Taratibu za nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko la kupiga marufuku uchezaji wa Kanga Moko, Kibao Kata na Bai Koko, kwa kuwa si tu vinalenga kumdhalilisha mwanamke bali pia vinahamasisha vitendo vya ngono ambavyo huchangia kwa kiasi kikubwa kuenea kwa kasi ya maambukizi ya UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si nia ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuzuia utamaduni wa Kitanzania, bali rai yetu ipo

kwa ajili ya kujenga jamii yenye misingi ya kuulinda utu, hadhi na thamani ya Mwanamke wa Kitanzania, pamoja na kulinda ustawi wa vizazi vyetu dhidi ya vitendo ambavyo havilengi kuulinda utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la maendeleo ya jamii, ni lazima jamii zihamasishwe kushiriki kwenye shughuli za maendeleo kwa manufaa yao. Changamoto kubwa iliyopo katika Jamii za Kitanzania, ni pamoja na vitendo vya baadhi ya watendaji wa Serikali kuwaacha nyuma Wananchi katika Miradi na Programu mbalimbali zinazohusu jamii zao. Hali hii imejenga tabaka kwa Wananchi ambao wanaamini kuwa shughuli za maendeleo za jamii zao ni wajibu wa Viongozi wao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija katika jamii nyingi za mijini, suala la uhamasishaji wa jamii katika shughuli mbalimbali za kijamii upo katika kiwango kidogo na hivyo kufanya hata baadhi ya shughuli kama usafi wa mazingira wa kaya na mitaa mbalimbali unaonekana kama ni kazi ya Serikali tu. Ipo haja ya kuandaa Programu Shirikishi zitakazowahamasisha Wananchi katika shughuli za maendeleo ya jamii zao na kuvunja matabaka mbalimbali yanayojijenga kutokana na Wananchi kutoshirikiana kuendeleza jamii zao. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua toka Wizarani ni mkakati upi kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014 ulioandaliwa kuhakikisha Wananchi wanahamasishwa katika shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, changamoto kubwa ipo kwa upande mwingine, Wananchi nao wako nyuma sana kwani hawataki kujihusisha na mambo muhimu ambayo Serikali inawaletea mitaani kwao; wengi husingizia kuwa na majukumu mengi sana hadi kushindwa kushiriki kikamilifu katika miradi na hata kushindwa kuishinikiza Serikali iwashirikishe au iitekeleze Miradi kwa mujibu wa mipango mikakati. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwa Serikali kufufua hamasa kwa kuajiri mama na baba maendeleo *(Social Workers)* kama ilivyokuwa zamani kwa kila kata ili

kuweza kuhamasisha jamii kushiriki kwenye Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuna Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii, hali hairidhishi katika ngazi ya Kata na Kijiji, ambako Wataalam hao wanahitajika zaidi kuwafikia Wananchi na kuwahamasisha ili kujiletea maendeleo yao.

Sera ya Maendeleo ya Jamii imeelekeza awepo angalau mtaalam mmoja wa Maendeleo ya Jamii kwenye kila Kata. Hivi sasa ni asilimia 56 tu ya Kata zote 2,637 zina Wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Hii ina maana kuna upungufu wa wataalam 1,213, sawa na asilimia 44 ya mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia idadi kubwa ya wahitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambao hawana ajira. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa nafasi za ajira kwa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ili kuweza kuziba upungufu uliopo katika Halmashauri zetu. Pia changamoto kubwa iliyopo ni kukosekana kwa nafasi za ajira kwa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika sekta mbalimbali.

Mwaka wa fedha wa wa 2012/2013, tulisema wazi kuwa, Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii huhitimu vyuo mbalimbali, lakini kuwepo kwao hakuoneshi tija kwa Taifa; hivyo, fani hii imeendelea kupuuzwa.

Wizara ituambie ni mkakati gani uliopo ambao umewekwa kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ili kuweza kuziba pengo katika Halmashauri kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014, lakini pia katika kuhakikisha kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, wanapata nafasi za ajira katika sekta mbalimbali nchini ili kuongeza tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; katika kipindi cha miaka mitano, idadi ya wananchi waliopata mafunzo katika Vyuo hivi imeongezeka kutoka washiriki 25,486 mwaka 2005/2006 hadi 31,877 mwaka 2010/ 2011. Hata hivyo, hali ya majengo na miundombinu katika vyuo bado ni chakavu kutokana na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni uhaba wa vyombo vya usafiri, upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali, nyumba za watumishi, madarasa, karakana, mabweni, vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kwa ujumla wake ni shilingi bilioni 2.1 fedha za ndani, wakati jumla ya fedha za viburudisho na vitafunwa ni shilingi 69,037,000/= ambayo ni sawa na 3.3% ya bajeti ya maendeleo ya fedha za ndani ukiondoa fedha zinazowekwa kwenye benki ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni mikakati gani ambayo Wizara imejipangia kwa mwaka huu katika kukabiliana na changamoto hizo? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuipa kipaumbele Wizara hii na kuhakikisha kuwa inapata bajeti ya kutosha ili kuweza kukabiliana na changamoto hizi ili kuweza kuleta mwamko wa maendeleo katika jamii ya Kitanzania kwa kuongeza wataalam wa kutosha wa fani hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake; kwa mujibu wa Waziri mwenye dhamana wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)*. Kati ya mwaka 2006 hadi 2010, jumla ya Sh. 1,048,000,000 zilikopeshwa kwa wanawake wajasiriamali katika Halmashauri 128 Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua mpaka sasa ni idadi gani ya wanawake ambao wameweza kunufaika na Mfuko huu kwa upande wa Tanzania Visiwani na ni kwa kiwango gani Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake umejiwekea mikakati ya kuwafikia na kuwanufaisha wanawake wa Tanzania Visiwani kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa takwimu za Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 , jumla ya Maafisa Maendeleo ya Jamii 265 kutoka ngazi za Kata, Halmashauri na Mkoa, walipatiwa mafunzo kuhusu kuhamasisha wanawake kujiunga na *SACCOS* na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali kwa kuzingatia Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua Wizara imefanya mikakati ipi ili kufuatilia matokeo ya mafunzo hayo kwa Maafisa Maendeleo ili kuweza kujua idadi halisi ya wanawake ambao mpaka sasa wamefanikiwa kujiunga na *SACCOS* na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania ilianzishwa kwa nia ya kuwapa fursa wanawake wa Tanzania katika kupata msaada wa kifedha kwa miradi mbalimbali. Changamoto kubwa ni kuwa benki hii haijafika katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na hivyo kusababisha wanawake wengi kukosa fursa ya mafunzo na mikopo ya benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, majibu ya Serikali ni kuwa ili kuwafikia watu wa vijijini imeanzisha *Umoja Switch* inayomsaidia mwananchi kupata huduma za kibenki kwa muunganiko wa mabenki mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaona kuwa changamoto hii inajenga matabaka kwa wananchi hasa wa vijijini ambao wanaona kuwa

wanawake wa mjini wanapendelewa kifikra. Hivyo, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha lazima iweke mkakati wa jumla wa kuwawezesha wanawake wa vijijini kupata fursa za kibenki, ikiwemo mikopo yenye riba na masharti nafuu kwa kuwa asilimia kubwa ya wanawake wanajihusisha na shughuli za kilimo ambazo nazo zinawapa wakati mgumu katika kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria Kandamizi dhidi ya Wanawake na Watoto; kumekuwa na matumizi ya Sheria mbalimbali katika jamii ambazo zimekuwa kandamizi kwa Watanzania, hali inayofanya jitihada za kuleta maendeleo ya kiujumla ya jamii kuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sheria kandamizi ambazo zinahitaji marekebisho ya haraka kwa sasa, zikiwemo Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sheria ya Kudhibiti Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza marekebisho ya haraka yenye tija ili kuweza kujenga Taifa letu kwa misingi ya kutunza na kulinda haki za makundi yote ya kijamii kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema, hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara hii ina wachangiaji wengi sana, lakini kutokana na bajeti yake kuwa ni ya siku moja, tunatoa nafasi kwa wachangiaji wanane.

Katika wachangiaji hao, tunaanza na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, ajiandae Mheshimiwa Titus Kamani na pia Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed ajiandae.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu. Kabla sijaendelea kuchangia hotuba hii, kwanza naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Sina matatizo na hotuba hii pamoja na kitabu hiki, isipokuwa nitaboresha tu baadhi ya mambo, kuhusu ukatili dhidi ya akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili dhidi ya akinamama ni mwingi na ni mkubwa sana na unahuzunisha. Ukatili huu siyo wa kupigwa tu, lakini ukatili huu unakuja mpaka waume zao wakifariki. Haya sisi huwa tunasema kwamba, Serikali isimamie, lakini watu wa mwanzo kabisa ni sisi Viongozi tuliomo humu ndani kuanzia Wabunge, Madiwani halafu Kijijini. Kwa bahati nzuri kila Kijiji kina viongozi wake mpaka Kata na Wilaya, tutoe taarifa haraka ili hawa akinamama wasaidiwe kwa hali na mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile watendaji wakuu au wahusika wakuu ni Jeshi la Polisi pamoja na Mahakama. Kesi kama hizi za ukatili dhidi ya akinamama na ushahidi upo, huwa nastaajabu kesi kama hizi, zinakwenda kwa muda wa miezi sita au mwaka, unasikia kwamba ushahidi haujapatikana. Hili nalo linatufanya sisi akina baba kuzidisha kuwafanyia ukatili akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile Waziri katwambia kuwa kama Mikoa saba mpaka nane ameshatoa elimu pamoja na semina, Mikoa nane ni kidogo sana, namwomba Mheshimiwa Waziri azidishe kutoa Semina kuhusu ukatili na siyo atoe kwa akinababa tu, bali wawepo akinamama, wawepo Madiwani na wote wale wanaohusika wasikie. Pia ukatili wa watoto vile vile utolewe semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wa mtaani; nadhani Serikali haijatoa hamasa kwamba, watu wazae kwa wingi, watu wanazaa kutokana na starehe zao. Sasa kila anayesimama hapa anailenga Serikali dhidi ya watoto hawa. Kwanza tujiulize watoto hawa wanasababishwa na kitu gani? Watoto hawa wahusika wakuu ni wale wale wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ninaoutoa watoto hawa waelekeze wanatoka wapi? Wazee wao wako wapi? Twende, tutazame za wazee hawa ziko vipi? Lakini hapa kila

kitu Serikali, kila kitu Serikali, Serikali haijatoa hamasa kuwa watu wafanye tendo la ngono kwa kupata watoto wengi. Mimi kama mimi Jimboni kwangu, siwezi kusema kuwa watu wasizae, ukisema hivyo tu utaambiwa kuwa hutaki watu na utakosa kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri kupitia kwako kuwa, itolewe taaluma ya uzazi wa mpangilio. Itolewe taaluma akinamama wanavyokwenda kwenye anasa zao, starehe zao za ngono, ni lazima wakati wa kutenda tendo la ngono wahakikishe kwamba, kabla kiwanja hakijatumiwa basi soksi ziwe zimevaliwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Zanzibar, sina mashaka nao lakini nataka Mheshimiwa Waziri aje atueleze kwa nini ina kigugumizi na hiki nitasimama kama kawaida ili kupata maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nakwenda kunako mashindano ya warembo; Mashindano ya warembo wote wanakuwa akinamama/wanawake na kama wanaume wataonysha mavazi yao basi watavaa *full suit* suruali mpaka chini, lakini akinamama wao mpaka hapa mapajani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natoa maelekezo yangu na ushauri, kwa hapa Tanzania mwanamke yeyote atakayekwenda kutaka kuchaguliwa awe mrembo, avae vazi la heshima, lakini akitoka hapa akienda huko nje kama lazima avae nguo fupi, mwache avae lakini kwa hapa kwetu mwanamke yeyote akienda kwenye mashindano, basi avae nguo za heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwunga mkono na nilifurahia sana ndugu yangu Mheshimiwa Shamsi, alipokuwa mgeni rasmi, akauliza hivi huyu mrembo hapatikani mpaka aje uchi? Mpaka leo hawajamwita hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto ambao bado hawana umri wa kufanya kazi, hivi sasa kuna mtindo

wafanyabiashara wote huwa wanawatumia watoto chini ya miaka 15 ili wakae madukani, wauze *chips* na wauze kila kitu ili wawape hela ndogo kwa maslahi yao. Hili ningeomba kuanzia Wadi kwa kule kwetu Zanzibar na huku Kata, Vijiji, wasimamie hili ili vijana wetu wale wadogo wadogo wasifanye kazi ambazo haziwahusu kwa kuwaneemesha wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja watoto wale wakikutwa, kwa sababu kuna Mabalozi wa CCM, kuna wanavijiji, kuna Wajumbe wa Serikali ya Mtaa, basi wawahoji kwa nini wanafanya kazi zile na kama kuna watu ambao wanawaajiri wafanye kazi, basi zile waitwe na wapewe taaluma vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa natazama *TV,* nadhani ilikuwa *channel* ya *East Africa,* baadhi ya watoto walikubali tu kuwa wanatumwa na wazee wao na ikifika saa saba watoto wanaendewa, aliyepata 2,000 anatoa, aliyepata 3,000 anatoa na aliyepata 1,000 anatoa na kama wengine hawakupata kitu wanaadhibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hivi sasa kwa wale watoto ambao wanatumwa, basi twende au Serikali ifike sehemu husika na hasa Serikali za Mitaa, wawaendee watoto wale, tuwafanyie usajili, twende tukaulize kuna kitu gani na kama ana wazee wake, basi awe anawekwa kwa wazee wake ili afaidike na matunda ya wazee wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kuhusu kuvunja mila na utamaduni wetu hasa kwa akinamama. Hivi sasa akinamama wamegeuka akinababa na akinababa wamegeuka akinamama, kwa nini basi? Kwa sababu akinababa ndiyo wanaovaa nguo za heshima, kama mama utamkuta kavaa suruali siyo vibaya, siyo ya heshima kwa sababu anavaa nguo inambana mpaka sehemu husika zote unaziona, jambo ambalo siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe kivazi kizuri kwa mama avae vizuri, apendeze ule mwili wake uwe

umevaliwavaliwa hivi, wewe mwanaume ujiulize kavaa kanzu hali hii, je, ndani yuko hali gani? Sasa yametoweka hayo, yaliyoko sasa, ukimwona mtu kavaa kila mahali unapatambua. Jambo ambalo tunatoka kwenye utu na kwenda kuwa kama wanyama na sasa linaonekana limekuwa ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hivi sasa wanaume wengi walio vijana walishaona ni jambo la kawaida, wanakaa na wasichana hivi hata hawajali, wanawaua uume wao, tumefika mahali pabaya kabisa. Hili nadhani tungelikemea, tuwape uhuru wao wavae vizuri, akiwa anavaa suruali, anavaa kitu gani, avae lakini kiende na maadili yetu ya utamaduni wa Kitanzania. Mwanaume awe katika hali nzuri na mwanamke akiwa katika hali nzuri, hili natumaini Ndugu yetu Mheshimiwa Waziri tunamwomba sana hili alizingatie na lisimamiwe na watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru Mheshimiwa kengele la pili hiyo na hawa warembo lazima wawe mwiba vile vile, wasiwe wanene. Namwita Dkt. Titus Kamani.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii. Kwanza, nianze kupongeza uongozi wa Wizara hii kwa juhudi kubwa wanazozifanya kuipatia sura Wizara hii, sura halisi inayostahili katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua; hivi karibuni tumeelezwa kuwa Serikali imeteua sekta sita ndizo ziwe katika mfumo wa *quick results now,* lakini Wizara hii haimo, lakini kati ya Wizara nyeti katika kuondoa au kumaliza umasikini wa wananchi Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni ya msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni kwa sababu wanawake ni zaidi ya nusu ya idadi ya wananchi wote na kwa hiyo, ukibadilisha hali ya maisha ya wanawake, ina maana sehemu kubwa ya jamii yetu itakuwa imebadilika kabisa kiuchumi na kifikra. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata bahati ya kutembelea China, hawa wana mpango mkubwa sana wa kuondoa umasikini katika Taifa lao na moja ya maeneo ambayo wamejielekeza ni kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vya Maendeleo ya Wananchi pamoja na Vyuo kama *VETA* katika kufundisha wananchi hawa wanawake na vijana katika stadi mbalimbali, lakini wao wanakwenda hatua zaidi wanawaunganisha na taasisi zinazowezesha kupata mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili ni suala la msingi sana kwetu, kwa sababu vituo kama hivi walivyonavyo vingekuwa ni *business incubation centers* ambazo zingeweza kuibua mawazo ambayo yatatengeneza ajira, yatawapa kazi za kufanya na shughuli za maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi wanawake wa China ni kati ya wanaoongoza katika fani mbalimbali, zikiwemo *texitiles* na *embroidery* na wanauza mpaka nchi za nje, kwa nini Tanzania tusiweze kufanya hivyo na tayari vituo vya msingi tunavyo. Nafikiri kuwa ni muhimu sana Wizara sasa ikajielekeza katika kuviimarisha Vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu ambayo Vyuo hivi haviko hata kwenye Wilaya ya Busega ambako hakuna Chuo cha namna hiyo kwa kutumia *Private Public Partinership,* tuweze kuweka miundombinu ili Vyuo hivi viwepo katika sehemu mbalimbali katika nchi yetu, lakini pia viweze kuongezewa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia bajeti kwa upande wa Vyuo hivi ni ndogo sana. Mwenyekiti wa Kamati

na hata nashukuru na upande wa Upinzani wameliona hili kwa pamoja kuwa, kwa kweli vyuo hivi vinahitaji kuongezewa mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara hii iweze kufanya vizuri nafikiri kwamba, kwa mpango ujao wa *quick result now* ni muhimu Wizara hii ikaingizwa sasa ili na yenyewe ishiriki kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni huu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Mfuko huu ni kama tunausema tu kisiasa, lakini kiutendaji ni kidogo sana. Nimeangalia takwimu hapa kwenye bajeti, milioni 168 tu ndiyo zimekopeshwa kwa wanawake kwa nchi nzima, milioni 168, kwa *population* ya zaidi ya milioni 20 ni wapi na wapi? Nilikuwa naona kiwango wanachotoa ni cha laki moja na laki moja ni biashara gani hasa yenye tija itaweza kuanzishwa na mtaji wa laki moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kuwa ni muhimu sasa Serikali idhamirie kweli kuweka fedha na kwa sababu Serikali Kuu haiweki fedha za kutosha kwenye Mfuko huu hata Halmashuri zimeupuuza sana Mfuko huu hazitengi fedha kuingiza kwenye mfuko huu. Matokeo yake unakuta ni wanawake wachache sana wanaweza kuzipata. Tangu mwaka 2005 hakuna fedha ambayo imewekwa katika Mfuko huu. Sasa tunategemea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wanawake wamedhihirisha kwamba, wana uwezo wa kukopa na kurejesha vizuri. Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu sana Serikali Serikali Kuu na Halmashauri ziweke juhudi za makusudi ziimarishe Mfuko huu ili wanawake wengi waweze kunufaika na hivyo kubadilisha hali yao ya kiuchumi. Akinamama kimsingi ndiyo wanaogharamia shughuli nyingi katika familia, kwa hiyo ukiwaimarisha hawa, hali ya umaskini katika jamii itabadilika kwa kiasi kikubwa na kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwamba, nimesikitishwa sana na maendeleo ya Benki ya Wanawake.

Benki hii ilianzishwa kwa hamasa kubwa sana, shamrashamra nyingi. Kimsingi inafanya vizuri kwa kiwango chake pale Dar es Salaam, lakini benki hii haikuanzishwa kwa ajili ya wanawake wa Dar es Salaam peke yake, benki hii ni kwa ajili ya wanawake wa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inatakiwa ifanye kazi kibiashara, ishindane na mabenki ma-*giant* kama *CRDB, NMB, NBC* ambazo Serikali iliweka fedha nyingi na kwa muda mrefu. Serikali ilitoa ahadi ya kuchangia mtaji wa benki hii, nini kinachozuia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili benki ifungue matawi inahitaji kujenga miundombinu kwenye mikoa, sheria ya Benki Kuu hairuhusu kutumia amana za wateja kutengeneza miundombinu, ni muhimu Serikali itimize ahadi yake ya kuchangia ili angalau ianze hata kwa Kanda kufungua matawi na hatimaye mikoani. Kama itakuwa inachangia kiasi kidogo basi angalau bilioni moja kila mwaka, ili benki hii iweze kupanuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nigusie kidogo kuhusu suala la ukatili wa akinamama na watoto, lakini zaidi malezi duni ya watoto. Hivi jamii yetu tutaendelea katika karne hii kutuma watoto wakafanye biashara ya kuombaomba mitaani, dunia ya sasa! Ni aibu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Wizara ingeichukua hii kama changamoto kubwa na ya haraka, haipendezi na inafedhehesha. Sasa hivi ukipita kituo chochote cha mabasi au mahali popote ambapo kuna msongamano wa magari unakuta vijana wadogo wa kike na wa kiume wanaombaomba au wanajaribu kusafisha magari ili apate chochote, hii siyo ajira. Kwa kweli ni aibu, ni muhimu sana Serikali ifanye juhudi za makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana kabisa na mzungumzaji aliyepita kwamba, hawa watoto hawaji kwa bahati mbaya, wanatokana na kazi ya makusudi inayofanywa, kwa nini sasa matokeo yake yanakuwa mateso

kwa jamii? Ni lazima kuwe na mpango wa kuwafuatilia wazazi ili wawajibike kwa kazi waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kazi waliyoifanya na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Kamani. Sasa nitamwita Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhammed, ajiandae Mheshimiwa Maulidah Anna Komu.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyowekwa hapa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujikita juu ya ukatili wa unyanyasaji wa kijinsia, hasa ulivyoathiri nchi yetu. Kuna matukio mengi ya ukatili ambayo yanajitokeza katika nchi hii au katika jamii yetu. Matukio hayo ni kama vipigo kwa wanawake na watoto ambavyo vimeshamiri sana, ukeketaji ambao naweza kusema kidogo umepungua angalau una asilimia 0.1, ubakaji umekuwa ni wa hali ya juu, kulawiti, kunajisi, kutupa watoto, ambapo mtu amebeba mimba kwa miezi tisa, ameumwa na uchungu na amezaa, lakini mtoto anamtupa. Sielewi ni kwa sababu gani, inabidi watu kama hawa watazamwe akili zao, pengine zimechafuka kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa watoto nao umeshamiri sasa hivi katika sehemu hii ya kijinsia, lugha za matusi nazo ni moja ya unyanyasaji wa kijinsia ambao unatakiwa ufanyiwe kazi ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu hizi zote zinatokana na mambo mbalimbali kama mila na desturi ambazo zinachangia kutendeka kwa ukatili wa unyanyasaji wa kijinsia. Pia mila hizi ambazo bado tunaendelea kuzitekeleza, namwomba Waziri atoe elimu ya kutosha ili watu

wasijiendekeze katika mila za namna hii na unyanyasaji huu utakuwa hauishi siku zote kwa sababu mila hizi tutakuwa tunaziendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia mbaya za baadhi ya wazazi nazo pia ni sababu mojawapo. Wazazi na walezi nao tunawalea watoto wetu katika hali mbaya sana, tunawatesa, tunawafungia ndani ya vyumba, tunawapiga, tunawachoma na moto. Hizi ni sababu mbaya ambazo zinamuathiri mtoto kisaikolojia ndiyo maana unamwona mtoto anahama katika nyumba anakwenda sehemu zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hali duni ya uchumi katika familia, nayo hii ni sababu mojawapo zinazofanya unyanyasaji wa kijinisia uwe mkubwa. Ni bora sasa hivi mume na mke wakae pamoja waweze kutazama uchumi wao uko namna gani ili waweze kuangalia watoto wao vizuri na hili wimbi la watoto lisije likawa linazidi siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo ni la talaka na kutengana. Talaka na kutengana nayo ni moja katika sababu zinazoleta machafuko katika unyanyasaji wa kijinsia. Mwanamke anapotalikiwa hana kazi, kwa sababu hana kazi na anataka kukaa na watoto, inabidi watoto hawa kwa kuwa hawawezi kutazamwa vizuri, inabidi wahame katika nyumba wakimbilie mijini, au mume anayetakiwa awatazame watoto wale, hapeleki chakula, hawashughulikii kuhusu shule. Hii pia inakuwa ni sababu ya kuwafanya watoto hawa wapate tabia isiyoridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia ya ubinafsi kwa baadhi ya wazazi na walezi, kuna tabia pia ya ubinafsi kwa baadhi ya wazazi na walezi jamani. Wewe mwenyewe umemzaa yule mtoto, lakini unamtenga, unasema, huyu bora kuliko huyu. Hili ni jambo baya kabisa, nawaomba wazazi wenzangu tuache tabia hii ya kuwatenga watoto ili tuepukane na unyanyasaji huu wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watoto kama hawa, unawaweka mbali hata huwapi elimu, wakati unao uwezo wa kuwapa elimu, una uwezo wa kuwapa malazi bora, lakini hufanyi jambo hilo, unawaacha watoto wanaathirika, watoto wanatembea halafu inakuwa ni matatizo ya Serikali. Sisi tunasema kwamba, Serikali haijafanya hivi, ingawa Serikali nayo ina wajibu wake, lakini na hili wazazi lazima tutimize wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifo vya wazazi na walezi, navyo pia ni tatizo. Mzazi ameshakufa, mlezi amekufa, basi, watoto tunawaacha wanasambaratika. Hii ni tabia mbaya na ni hali mbaya sana kwa watu wanaofanya vitu kama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizi za matatizo kadhaa niliyoyazungumza, matokeo yake ni kwamba, tukiangalia mwaka 2012, watoto waliobakwa ni 356, watoto waliolawitiwa ni 246, watoto waliotupwa ni 174, watoto walioibiwa ni 103. Haya yote yanafanywa na watoto wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi watu wazima wenye umri wa miaka 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa ambao wanafanyiwa ukatili huu wana umri wa miaka 0 mpaka miaka 18. Lakini kwa upande huo huo, utaona kwamba, watu wazima nao wanaathirika. Watu wazima waliobakwa ni 5,389, kulawitiwa ni 491, mauaji ya vikongwe ni 629 na mashambulio ni 160 na haya pia wanayafanya watoto wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni mbaya sana na haya tuliyoyazungumza ndiyo yaliyoripotiwa Polisi, lakini kuna wale ambao hawajaripoti Polisi, pengine tu kwa sababu wana hofu, wamehofishwa na wale watu ambao wanafanya vitendo vile, au mila tamaduni zetu zinamzuia mtu yule kufanya vile, anaona kwamba ni aibu au kutojua haki zetu. Wanawake bado *percent* kubwa hatujui haki zetu. Namwomba Waziri atoe elimu ya kutosha kwa kutoa mafunzo kwa wanawake ili kujua haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja katika suala la watoto wanaoishi mitaani. Watoto wanaoishi mitaani sasa hivi, asilimia kubwa sana ya watoto hawa sasa hivi wanalawitiwa na wanabakwa, japokuwa wao wenyewe hawataki, lakini wakati wa usiku wengi wao wanatafuta mahali pa kulala, wanafanyiwa vituko kama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utafiti uliofanywa na *USAID* mwaka 2013 unaitwa *Help Seeking Pathways and Barriers for Survivors of Gender base Violence* zaidi ya asilimia 75 ya watoto wa kike chini ya miaka 18 wame-*experienced physical violence* na watoto watatu kati ya kumi wanaripoti kufanyiwa *sexual violence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Wizara inajitahidi sana kwa kufanya semina, makongamano, mikutano, lakini bado tunaomba mtoe elimu ya kutosha na myashughulikie mambo haya ili Serikali iweze kutimiza shughuli zake na kutoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Thuwayba ni kengele ya pili.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa nitamwita Mheshimiwa Maulidah Komu, dakika tano.

**MHE. MAULIDAH ANNA VALERIAN KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini kabla ya yote ningeomba nikupe ujumbe wangu mmoja tu katika ukumbi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana hasa kwa upande wetu sisi akinamama, lakini kinachonishtua na kunishangaza na ndiyo maana nimekaa hapa natafakari, nikasema ndiyo maana Serikali inatupa bajeti ndogo kwa

sababu tunaonekana sisi wenyewe hatuoni umuhimu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba uangalie ukumbi huu leo, ambapo ningetegemea akinamama wangekuwa wengi na wengi tungepigania kuchangia Wizara hii muhimu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naishia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kidogo tu kwa Serikali kuhusu watoto wa mitaani. Ni kweli tunasema kwamba, hawa watoto wa mitaani mama zao ndiyo washughulike kuwalea na kuwapa matunzo. Hayo hayapo kwa sasa hivi. Kwa sababu wimbi la watoto wa mitaani linaongozeka kila siku asubuhi na ni hatari kwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo Kigamboni na naona watoto wa mitaani wengine wamejikusanya wao wenyewe, wamekodisha nyumba sisi wengine ndiyo tunawasaidia, lakini walioko mitaani ni wengi hatari!

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa naambiwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam wapo 5,800, nikasikia tena Mkoa wa Kilimanjaro wapo 5,600. Ninachoiomba Serikali, isaidie Wizara hii kwa dharura na kwa kuangalia umuhimu wa watoto walioko mitaani. Leo tuna mwaka mmoja watoto hao wana miaka kuanzia minne, mitano mpaka miaka 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watoto watakua, watafika umri wa miaka 18 na miaka 20, watoto hawa wanaishi kwenye mazingira magumu, wanalawitiwa, wanalawitiana wao wenyewe kwa wenyewe, wanachukuliwa kufanywa au kufundishwa kama wezi usiku, wanaishi kwenye maisha ya ajabu ya kikatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi zilizoendelea tunaposikia watoto wamepigana risasi kwenye mashule, wanaangalia historia ya yule mtoto alikuwaje mpaka akafikia kupata akili ya kupiga risasi wenzake. Sasa sisi tunaacha hili wimbi tukisema kwamba, akinamama wajitokeze kuwachukua, wako wapi hao akinamama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri kwamba, tujitahidi kutafuta hizo pesa, wakusanywe hao watoto sasa hivi, waulizwe wanatokea wapi, kama vile alivyofanya Mheshimiwa Makamba wakati alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, aliwakusanya ombaomba wote wakarudishwa makwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuwakusanye hao watoto, waulizwe wanatokea wapi, Serikali imsaidie Waziri na Naibu wake na Wizara kuwarudisha hawa watoto kabla hawajakua, Jiji la Dar es Salaam halitakalika, hao mnaowaita watalii hawatakuja, kwa sababu kutakuwa na majambazi na watu waliokua kwenye hali ya kutisha kabisa, fikra za kutisha kabisa, watakuwa hawana woga wa kufanya jambo lolote lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, iache hii dharau ya kusema, watakuja wenyewe akinamama wawachukue watoto wao wakawalee. Samaki mkunje akiwa bado mbichi, tukisema tunaliacha hili leo, tusubiri miaka mitano au sita ijayo, kesho na keshokutwa majambazi wamezidi Dar es Salaam, tunapishana na akinamama Komu na watoto wao, ahaa babu tupishe! Itakuwa hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kapt. John Komba atafuatiwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere. Mheshimiwa Komba kaa kwanza, Mheshimiwa Nyerere dakika tano.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naanza kuchangia kuhusu mauaji ya vikongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda gereza la Ngudu leo limefurika watuhumiwa wa mauaji ya vikongwe, hii ni kwa sababu ya kukosa elimu. Vikongwe wanauawa eti kwa sababu ya macho mekundu. Macho mekundu yanatokea kwa sababu hawa akinamama wamekuwa wakipikia kuni maisha yao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wanauawa eti kwa sababu ameonekana ameingia zizi la mtu la ng'ombe. Ni kwa sababu ya hali halisi mwanamke anapozeeka au mwanaume, kuna tatizo linaitwa *Alzheimer* au *dimentia***,** husahau, hupoteza kumbukumbu ya sasa hivi, lakini anaweza akakumbuka mambo ya miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kikongwe anaweza akatoka nyumbani anapoishi akaenda kwa jirani, akaona zizi la ng'ombe, akakumbuka alivyokuwa anakamua ng'ombe wakati wa usichana wake, akaingia kwenye zizi la mtu akaanza kukamua ng'ombe, matokeo yake anapigwa mapanga anauawa. Elimu itolewe na Watanzania waelimishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie kuhusu mfumo dume. Tanzania tumekuwa mahiri kwa mfumo dume, kuna watu wanafikiri kwamba uwezo wa mtu unapimwa kutokana na jinsia, siyo. Naomba niwape mfano, kuna mtaalam mmoja alichukua vyumba viwili akaweka matangazo kwenye mlango mmoja aliandika *Intelligent Men Only*, mlango wa pili akaandika *Ordinary Men Only*,

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza wanaume wengi waliingia kwenye *Ordinary Men Only* na ni mmoja tu aliingia kwenye *Intelligent Men Only*. Lakini tangazo hilo hilo lilivyotumika kwa wanawake; mlango mmoja uliandikwa *Intelligent Women Only*, huku mlango wa pili uliandikwa *Ordinary Women Only,* kwa upande wa akina mama wanawake wote waliingia kwenye *Intelligent Women Only.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii inaashiria kwamba, wanawake tunajiamini na siyo kujiamini tu, wanawake tuna akili, wanawake tuna uwezo, wanawake tumesoma, wanawake tuna uwezo wa kuwa viongozi. Wale wote ambao wanafikiri watatushusha chini eti kwa kujaribu kutusema vibaya wanawake hasa wanasiasa, wasahau, *we are strong, we are powerful*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mkalale tu kama hamna uwezo wa kushindana na sisi, *so* hii ndiyo meseji ya mwaka. Kwa wale wote wanaodhani kwamba mwanamke atashushwa uwezo wake eti kwa maneno tu ya kipuuzi ya kihuni, *hell no*, hakuna tunaendelea kusonga mbele, tuna uwezo, tuna uwezo wa kuwa viongozi kwa sababu nia tunayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu suala la mavazi. Suala la mavazi kila eneo lina mavazi yake, ukienda kwenye mkutano unavaa mavazi husika, ukienda Kanisani unavaa mavazi husika, ukienda Msikitini utavaa mavazi husika, ukienda kulala unavaa mavazi husika, ndiyo maana watu huwa hawalali wamevaa suti. Jambo la kufanya tuwaelimishe wananchi wafuatilie, wazingatie hali hii kwamba kila sehemu ina vazi lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu mauaji ya wanawake wa Butiama. Hii inasikitisha! Hii ni aibu! Wanawake wa Butiama wanauawa kwa sababu ambazo mpaka sasa hivi hazieleweki. Hii ni aibu ya hali ya juu kuona kwamba, Wilaya ya kihistoria, Wilaya ambayo ni makazi ya Baba wa Taifa wanawake wamekuwa *victim*, wanachinjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nasema mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, ichukuliwe hatua mara moja, kwa sababu suala hili limetudhalilisha Taifa zima. Nashangaa sijawahi kusikia hatua madhubuti zimechukuliwa kuweza kudhibiti vitendo hivi vya kinyama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijagongewa kengele, nina imani bado nina dakika kidogo pale. Naomba nizungumzie suala la watu kutumia lugha chafu kuchafua wanawake kwenye mitandao; nasema waache mara moja kwa sababu, haiwasaidii. Ukitaka kushindana na mwanamke, ambaye unadhani anakuzidi, ana uwezo kielimu, kiuwezo, kifikra, ana hekima, jiimarishe na wewe ili uweze kumkaribia hata robo badala ya kukaa kwenye mitandao umekunja mgongo siku nzima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Kapt. John Komba.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichangie kuhusu Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwanza nimpongeze Waziri mwenyewe, anafanya vizuri na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara muhimu sana, ni Wizara mtandao, kubwa kabisa. Serikali, yenyewe imeunda Wizara hii, lakini nashangaa Serikali, inainyanyasa hii Wizara, inainyanyapaa hii Wizara. Ina mambo mengi, lakini ni Wizara ambayo ina bajeti ndogo kuliko Wizara zote, lakini imepewa jukumu kubwa kuliko Wizara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vinakwenda vitu vinakuwa tofauti; jukumu kubwa, lakini uendeshaji unakuwa ni mdogo. Kwa hiyo, naomba Serikali, iangalie upya jinsi ya kuisaidia Wizara hii, ili iweze kufanya mambo makubwa zaidi. Tukumbuke usemi unaosema, "Ukimsomesha mtoto wa kike, umesomesha Taifa zima na ukimsomesha mwanaume umesomesha mtu mmoja tu." Kwa hiyo, naomba Serikali, iweze kutoa pesa nyingi katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu Sheria ambazo zinawakandamiza wanawake. Ziko Sheria nyingi, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi, Sheria ya Ardhi, Sheria za Kimila zinzomkandamiza mwanamke ziko nyingi sana. Naomba leo Serikali, iniambie ni lini itaandaa Miswada ya kuleta Sheria hizi hapa Bungeni, ili tuzitungie Sheria, ili wanawake hawa waache kukandamizwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamwona Mama Nyerere pale analalamika tu, analalamika kwa sababu, kwa kweli, wanawake wana uwezo, wana upeo, lakini wananyanyaswa

bila sababu yoyote ya msingi. Leteni Sheria hizi hapa tuzirekebishe, ili mwanamke awe kama mwanaume alivyo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa hata leo wanaume nao wawe Wabunge wa Viti Maalum, halafu wanawake wawe ndio Wabunge wa Majimbo. Ikija Sheria kama hii itakuwa nzuri zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mmomonyoko wa maadili. Taifa letu limeshuhudia wakati wote, sasa maadili yanazidi kumomonyoka miongoni mwa watu wetu na wanaoongoza kumomonyoa maadili ni sisi Wanasiasa, ambao tunazungumza maneno ya hovyo, tunapenda kuzomea, tunapenda kupiga mayowe, hatuna heshima, na watoto wanatuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge, ndio mfano, ndio kioo cha jamii katika nchi yetu; sisi ndio Viongozi, lakini kazi yetu kuzomea, kusema maneno ya hovyo, sasa unamlaumu mtoto amemomonyoka maadili, unashangaa, unalaumu ulikoangukia, kumbe umesahau umejikwaa wapi? Tunajikwaa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu utakuta ni aibu sana Mbunge mwanaume au mwanasiasa mwanaume kumtukana mwanamke. Uone aibu ni kama unamtukana mama yako mzazi. Ni aibu sana, wako Wabunge kabisa. Najua Mikoa kama Iringa huko, wapi, Wabunge wanawanyanyasa Wabunge wa kike; mimi sipendi hata kidogo, rekebisheni tabia hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto wa mitaani. Bado naendelea kusema kwamba, wanaosababisha tatizo la watoto wa mitaani ni sisi wanaume. Sisi ndio wa kulaumu, ukiwaona watoto wako pale mitaani wanaombaomba chanzo chake ni sisi. Tunaandaa ngono za *deal,* yaani unamkuta mwanamke unampa tayari kitu chake, pesa yake,

unakwenda naye, unasahau, baadaye mtoto hana baba na ukimuuliza wewe baba yako nani anasema mimi sina baba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kafanye utafiti Dar-es-Salaam, wale watoto wote wa mitaani ukiwauliza baba yako yuko wapi? Watakwambia simjui; hizo ni ngono za *deal* ambazo tunazifanya sisi wanaume. Tena wengine tuna vyeo, tukiacha hii watoto wa mitaani watapungua. Fanya ngono stahili wewe na mke wako na nini kwenye ndoa na nini, lakini hizi ngono za mitaani mitaani hizi ndio zinaongeza watoto wa mitaani, tuache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Mfuko wa Maendeleo. Tangu 2005 Mfuko huu umeshakufa, fedha zake zote zinapelekwa ile Benki ya Maendeleo ya Wanawake; sasa Mfuko huu ni wa Maendeleo ya Wanawake wote Tanzania, wakiwa wako Mbamba Bay, wakiwa Tabora, Iringa, Manyoni, Arusha au Moshi, lakini leo Mfuko huu hauna pesa hata moja. Halafu tunasema tunataka kuwainua, kuwawezesha wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema mwanamke anaweza, lakini akiwezeshwa; kuwezeshwa ni pamoja na Mfuko kama huu upewe pesa kila wakati, ili wanawake waweze kukopa, waweze kusaidiwa kufanya mambo yao. Naomba sana Serikali, iurudishe Mfuko huu tena kwa nguvu kubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake; ni lazima nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuamua kutoa fedha za kuanzisha Benki hii. Hiyo ndio *credit* sasa ya CCM katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni *credit* kwa CCM, lakini pesa hizi hazitoshi. Pamoja na kwamba, Serikali, inatoa pesa kupitia bajeti hii, lakini ni vizuri itafute tena pesa nyingine

kwa Wafadhili ili Benki ile badala ya kusaidia Dar-es-Salaam na Pwani tu, iende kila Wilaya ili hasa iwasadie wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi unakuta ni Wilaya za Dar-es-Salaam na Wilaya kidogo chache za pale Pwani. Lakini pesa zile zingekwenda, Benki ile ingekwenda sehemu zote kama Tabora, Arusha, Mwanza, Iringa, Rukwa, sijui wapi huko na wapi na wapi, tungeweza kufanya mambo, kuwainua sana wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kapt. John Komba na sasa namwita Mheshimiwa Leadiana Mng'ong'o.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu, ambayo imefanya wanawake wengi tukapata nafasi za uongozi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Mfuko huu uliweza kusaidia miradi mbalimbali ya wanawake nchini, lakini sasa umeachwa kama ulivyo. Naomba wenzangu wote waniunge mkono hapa leo, naomba fedha bilioni mbili zilizopelekwa Benki ya Wanawake, zirudishwe kwenye sehemu yake na fedha za Benki ya Wanawake ziongezwe na fedha hizo zipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukubali namna hii, wanawake ndio sehemu kubwa ya wananchi hapa Tanzania, idadi kubwa ya watu ni wanawake. Wakulima hapa nchini wanaozalisha chakula ni wanawake, wanaohudumia wagonjwa ni wanawake, wanaokumbwa na majanga ni wanawake na watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kamati ya Bajeti, ikatafute fedha kwingine, bilioni mbili zirudishwe na Mheshimiwa Rais wetu, amefanya kazi nzuri, ameahidi; miradi mingi Rais anaahidi, lakini huwa hawanyofoi sehemu. Kwa nini, alipoahidi Rais wetu kwa heshima kubwa ya kuwajali wanawake wa nchi hii, halafu mtunyofolee zile hela nyingine? Naomba wenzangu mniunge mkono, fedha zikatafutwe leo hii na bajeti ipite, tutakuwa tumewajali wanawake wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja kabisa, fedha hizo zitolewe. Bilioni mbili zirudishwe mahali pake na bilioni mbili zikatafutwe na ziongezwe Benki ya Wanawake ipate bilioni nne, ili iweze kufika sehemu nyingi zaidi. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mniunge mkono kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na tuunge mkono Wabunge wenzangu, ili tuweze kupata fedha hizo.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu imeungwa mkono. Bilioni mbili zirudishwe mahali pake, bilioni nne zitafutwe kwa ajili ya Benki ya Wanawake hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea hapo hapo, Benki ya Wanawake inafanya kazi nzuri na naomba nimpongeze Mkurugenzi Mkuu, Mama Magreth Chacha, kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kuhakikisha kwamba, Benki hii inafika kila sehemu. Lakini haiwezi kufika kila sehemu kama ina bajeti ndogo ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka ifike Njombe, Iringa, Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Lindi, Mikoa ya Tanga, Singida na Mikoa ya Mara, Shinyanga, Geita, Simiyu na Mikoa

yote hapa nchini; hiyo ndio itakuwa Benki ya Wanawake ambayo imemfikia kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kama tulikuwa hatuikubali kwa nini tumeiweka? Matokeo yake Watendaji wanaonekana kama hawana kazi maalum ya kufanya. Naomba sasa ibadilike, hii ndio iwe Wizara ambayo inapewa fedha na kujaliwa, lakini naomba kwanza hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Baraza la *NGOs* hapa nchini. Serikali, imefanya kazi nzuri, imeanzisha Baraza la Kuratibu Masuala ya Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali; naomba nianze kwa ku-*declare interest* kwamba na mimi ni mwana-*NGOs* wa siku nyingi. Baraza hili kama halipewi fedha za uratibu hivi litawezaje kuratibu *NGOs* ambazo tunasema, ni za mifukoni, *NGOs* ambazo zipo sijui hazieleweki zinafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Baraza litengewe fedha, ili liweze kuratibu shughuli hizi na tujue kwamba, kweli Wizara imeweka Kitengo cha *NGOs* na Baraza lile linawezeshwa kufanya kazi. La sivyo, watategemea fedha za Wafadhili na Wafadhili watasema wanalotaka kwa sababu, huwezi kupewa fedha ambazo hazina masharti. Kwa hiyo, Baraza la *NGOs* nalo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya watoto; wenzangu wamezungumza, kila siku tunasikiliza kesi za watoto, watoto wamebakwa, watoto wamenyanyasika, watoto wameumizwa, ikiwa ni mashuleni, iwe ni nyumbani, iwe ni kila sehemu. Hebu hili tatizo tuliangalie kwa undani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kutoa hoja hapa kwamba, naomba ianzishwe Kamisheni ya Kuratibu Masuala ya Watoto. Kamisheni ya Kuangalia Masuala ya Watoto ili tujue kwa sababu wana matatizo mengi. Wana ajenda zao, ajenda 10 ambazo wanatembea nazo wanaelezea ajenda zetu ni hizi, sauti ya watoto inatumika kwenye Baraza la Wototo. Wizara inafanya kazi nzuri ya kuratibu na kuangalia hili Baraza la Watoto kama linafanya kazi, lakini kama

hatuweki chombo maalum cha kuangalia masuala ya watoto, matatizo ya watoto yataendelea kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watoto yatima, tumewapeleka mpaka Vyuo Vikuu. Serikali, imefanya kazi nzuri katika kila Halmashauri, fedha zinatengwa kwa kuhudumia watoto wenye matatizo, yaani watoto wa mazingira hatarishi kusomeshwa shuleni. Hivi naomba niulize ni watoto wa mazingira hatarishi wangapi waliomaliza Vyuo Vikuu tuliowasomesha, waliopewa ajira au wanaangaliwa kutafutiwa ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu na hili tuliangalie, kama tunawasomesha, tunawapeleka kwenye Vyuo vya Ufundi, tunawapeleka Vyuoni, halafu wakimaliza hatuwasaidii kupata ajira wakati wengine ni Wakuu wa Kaya. Naomba na hili nalo tuliangalie zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la mauaji. Mauaji ya vikongwe, wameshazungumza wenzangu, yalikuwepo mauaji ya vikongwe wanaosaidikiwa ni wachawi kwa sababu tu ya kupikia kuni na kuwa na macho mekundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezuka mauaji katika Wilaya ya Butiama, imezungumzwa pale. Kwa nini, wanawake wauawe, hivi ni hatua gani zimechukuliwa wanawake wa Butiama wanauawa hivi? Wanawake wa umri fulani, hivi wanawake wa Butiama wana nini ambacho watu wanatafutia utajiri kwenye vichwa vyao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali, itueleze ni tatizo gani liko Butiama tu? Ni tatizo gani hili? Hili nalo liangaliwe kwa undani, tuone kuna kitu gani? Uchunguzi ufanywe, tusichukulie juu juu tu kwamba, hawa ni wauaji na nini, hebu twende kwa undani tuchunguze, ni kitu gani hiki kinachofanya tatizo litokee, wanawake wa Butiama wauawe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kuwawezesha wanawake kiuchumi. Tuwawezeshe

wanawake kiuchumi na hili ndio tumezungumzia pamoja na miradi hiyo na *VICOBA* na *SACCOs* na nini, lakini hilo lingine nililokwishalizungumzia ni muhimu zaidi, lakini sio kiuchumi tu, tuwape elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku napingana na hoja inayosema eti wanawake wanaweza bila kuwezeshwa; kuwezeshwa sio mitaji tu, kuwezeshwa ni pamoja na kupewa taarifa sahihi. Wanawake wako vijijini huko hawajui hata mahali pa kupata mitaji. Taarifa sahihi ndio inayotakiwa na huko tuanzishe kama walivyoanzisha Dirisha la Wanawake la kuwapa elimu, lilishaanzishwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba, Mkoa wa Iringa pale Rungemba kipo, lakini vituo vya namna hii viwe vingi zaidi, ili liwepo dirisha ambalo linawapa taarifa mbalimbali likiwa na nia njema ya kupata elimu na mitaji. Watoto wetu wa kike wanamaliza shule, wako vijijini, hawajui mahali popote pa kwenda; naomba hili nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nalizungumzia kwa nguvu zote, ni ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana. Kama hatutapambana nalo na nawapongeza wanaume waliozungumza humu kwamba, ukatili huu wanaume wanaweza; kama wanaume wakisema leo tunaacha kufanya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wa kike utakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo ni kubwa na linaleta madhara makubwa sana na kuwafanya watoto wahamie mitaani. Ni lazima lipingwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tunatakiwa tuliangalie, ni suala ambalo tafiti zimeonesha viashiria vya masuala ya UKIMWI, wanawake na watoto wa kike wameathirika zaidi na tatizo la UKIMWI. Hivi ni mkakati gani ambao umewekwa kwa ajili, ya watoto wa kike na wanawake? Na tunajua kwamba, Wizara inayoratibu ndio hii, lakini ndio Wizara inayopewa fedha kidogo, kama vile fedha inayobaki, ndio ile Wizara inagawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba na hili pia liangaliwe na litiliwe umuhimu. Elimu ifike kwa watu wote wanaume na wanawake; tunajua hii Wizara inashughulikia jamii nzima. Wizara inayoshughulikia jamii nzima, sio wanawake tu, inashughulikia wanaume na wanawake, wazee na watoto na kila mtu na kama ni Wizara ya jamii nzima kwa nini, ndio ipate kile kidogo kinachokuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa ipate fedha za kutosha kwa sababu, jamii yote itafikiwa. Maafisa Maendeleo ya Jamii watahamasishaje wananchi wakati hawana vitendea kazi, hawana hata nyenzo za kuwafanya wafike kwa wananchi? Wengine wanafanya kazi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, nizungumzie suala zima la watoto wa mazingira magumu. Vituo vinavyowasaidia hawa watoto, kama *SOS* kilichoko Dar-es-Salaam na vingine vya Ma-*sister* kikiwemo cha Kipengele na vituo vingine vya dini vinasaidia, lakini havipewi ruzuku. Hebu tuanze kuviangalia vile vinavyofanya kazi vikiwepo vile vya Njombe na Iringa, vinavyofanya kazi nzuri na vyote vya Tanzania nzima, vipewe ruzuku kama ruzuku ya vitanda inayotolewa kwa hospitali binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ile hoja yangu niliyosema ijibiwe na fedha hizo zipite. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Mkosamali, dakika tano; atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyogera, naye dakika tano na ndio wachangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili name nichangie katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nataka kuchangia juu ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* na ningeshauri tu kwamba, Wizara hii ili iweze kuwa na kazi

za kufanya, ili iwe na majukumu ya kufanya, mambo ya elimu ya ufundi, bora tuwaachie hawa watu wa Wizara hii; Wizara ya Elimu ibaki inashughulika na elimu ambayo pia ni mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii vimekuwa na hali mbaya, havina huduma, ni vyuo ambavyo tunavitegemea visaidie watoto hawa wanaomaliza shule za Kata kwa sababu, viko kwenye Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mfano Chuo cha Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* Kibondo, kina zaidi ya miaka kumi hakijapata fedha za maendeleo. Mwaka jana kimepewa fedha za matumizi ya kawaida 400,000/= ambazo wanapaswa kuzifuata Mkoani Kigoma. Kutoka Kibondo kwenda Kigoma kufuata hizo fedha, kwenda na kuzifuatilia ni zaidi ya hiyo 400,000/= ambayo mmekuwa mnapeleka kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtupe majibu, mtapeleka fedha za kutosha lini? Tunataka tuwashauri, tuwasaidie, Vyuo hivi vya Maendeleo vya Wananchi, kila Wilaya vibadilishwe viwe Vyuo vya *VETA,* ili kuweza kusaidia nchi yetu kuendelea. Msione hawa Wachina wanakuja wanazungukazunguka kutengeneza mitaro hapa Tanzania, hawa hawajasoma mpaka Vyuo Vikuu wala hawana Shahada, huwa nawauliza, wana *Certificate* na *Diploma*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumieni vyuo hivi, viwe *VETA,* vifundushe na *SIDO* na watu wengine wawe na matawi yao pale, waende kufundisha viwanda vidogo na kadhalika. Vyuo hivi vifundishe elimu za kilimo na mifugo kwa maeneo ya kilimo na kwa maeneo ya mifugo, lakini mkiviacha vikakaa hoihoi tu namna hii kwamba, ndio mnaendeleza elimu ya ufundi, haitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote ambayo haitawekeza kwenye elimu ya ufundi, wananchi wake hawataendelea kwa sababu, viwanda vidogo ndio vinasaidia kwenye uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi. Lakini naomba fedha hizo ambazo mmekuwa mnatuletea Kibondo 400,000/= kwa mwaka jana, Januari mpaka Disemba, 400,000/=, tena mnawaambia wazifuate Kigoma Mjini, nipewe majibu sahihi. Ningewashauri tu fedha hizi kama ni 400,000/= bora mpeleke hata kwenye akaunti za vyuo zenyewe kuliko mnakopitishia, Hazina na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba, mmevitelekeza hivi vyuo, hamjaona umuhimu wake; mjitahidi, tafuteni fedha hizi maana Wizara inatengewa bilioni 23, yenye vyuo vyote hivi, huu ni utani kwa wananchi. Hebu kwa kweli, mjitahidi kwa kweli, hii *no.* Tena nadhani ingeweza kuwa hata Idara tu kwenye Wizara nyingine, kama mnapewa fedha hizi, bilioni 23, fedha kidogo sana hizi. Kwa mambo ya vyuo hivi na mambo yenu ya akinamama, fedha gani hizi? Ingekuwa Idara kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba nichangie kuhusu watoto wa mitaani. Tusipambane wala tusishinde tunashawishi watu kwenye kuwabaini watoto wa mitaani, tutafute vyanzo, kinachosababisha ni nini? Hawa watoto wanakuwa wengi kila mahali watoto wa mitaani? Ukipita hapo nje, nadhani na Waziri huwa na wewe ukipita pale wanakuombaomba fedha? Ni Wizara yako hiyo na wewe unawaona wanakuombaomba fedha na mabakuli yao, watoto wako hapo nje; sasa tuangalie vyanzo, lakini pia Serikali, iwe *strict.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ieleze wazi, mtu anazaa watoto 40, hakuna kusomeshewa watoto wote, hiyo ni kuwanyima fursa watoto wengine. Lazima tuwe na utaratibu kama Serikali, tunasaidia watoto wangapi. Huwezi kuacha watu wanazaa tu, wanazaazaa hovyo, wanatupa watoto nje huko, wanaombaomba, badala ya kupambana na chanzo, watu wanajiuza huko Dar-es-Salaam mitaani usiku, kila mtu anawaona; tumeshindwa kudhibiti kweli suala hili? Tumeshindwa kudhibiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kumekuwa na utitiri wa *NGOs,* kila mtu anasajili *NGO.* Nadhani kila mtu huko Tanzania ni mwanachama wa *NGO* fulani. Kila mtu, inawezekana hata humu Bungeni, kila Mbunge ni mwanachama wa *NGO* fulani, zimetusaidia nini? Mbona hamzitathmini kama wanavyofanya *CRB? CRB* wanaita, muwe mnafuta *NGOs* ambazo zimekaakaa hazifanyi kazi yoyote.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mkosamali. Sasa namwita Mheshimiwa Agripina Buyogera kwa dakika tano.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nimpe pole Mheshimiwa Waziri, kwa kazi ngumu anayoifanya kuisimamia Wizara hii. Naamini kama Wizara hii ingeongozwa na mwanaume angekuwa ameshajiuzulu, lakini kwa kuwa akinamama tumeumbwa na moyo wa huruma na tunaweza, ameendelea kuiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite Kasulu. Kasulu tuna Chuo cha Maendeleo; Wizara, Serikali mnaelewa, Chuo cha *FDC,* ambacho ni chuo kikubwa katika Mkoa wa Kigoma. Chuo kile kimefanya kazi nzuri sana kwa miaka ya nyuma, ambapo kilizalisha vijana wengi na wakapata nafasi ya kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua umahiri na ubora wa kazi nzuri iliyofanywa katika chuo kile, angalia katika Mkoa wa Kigoma, ubora katika Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma, ukiangalia nyumba bora kwa Mkoa wa Kigoma, namba moja ni Wilaya ya Kasulu, lakini yote yale ni matunda mazuri yaliyopatikana kutokana na chuo cha *FDC* Kasulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu kwamba, ni wakati sasa Wizara iangalie kwa makini,

kuhakikisha Chuo cha *FDC* Kasulu, kinarudi barabarani kwa maslahi ya Taifa la Tanzania. Naomba Wizara katika hili, itekeleze mambo matatu muhimu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ihakikishe inatafuta vitendea kazi katika chuo cha *FDC* Kasulu. La pili, ihakikishe wale vijana wanaopata elimu katika chuo cha *FDC* Kasulu, Wizara inawawezesha kuwatengenezea utaratibu wa kuweza kuwasajilia makampuni ambayo yatawasaidia vijana wale wanaohitimu katika chuo kile, waweze kupata kazi mbalimbali katika Halmashauri zetu. Tunajua tunatoa tenda mbalimbali, tunajenga shule na tuna miradi mbalimbali inayofanyika katika Halmashauri, lakini leo tunatafuta wajenzi kutoka maeneo mengine kabisa, wakati tumeandaa vijana ambao tunawafundisha katika vyuo vyetu.

La tatu, naomba Wizara ijipange; Mheshimiwa Waziri, naomba hili alisikilize na kwa kweli, nitaomba wakati anafanya majumuisho anipe jibu la uhakika. Wizara ijipange kufanya ziara kwenda Wilaya ya Kasulu, kutembelea Chuo cha *FDC,* ili kubaini upungufu uliopo pale na kuweza kuhakikisha chuo kinapata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna wakufunzi wetu pale, tuna Walimu wanaojitolea pale, lakini hawana vitendea kazi. Kwa hiyo, ili kulisaidia Taifa, pamoja na hali ngumu, pamoja na kukupa pole, naomba hili uniahidi ni lini Wizara itakuja Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala linguine kuhusu hii Mikopo ya akinamama. Naiomba Serikali, ihakikishe inaziagiza Halmashauri, Wakurugenzi, zile asilimia ambazo zinahitajika kuweka katika Idara ya Maendeleo ya Jamii wahakikishe zinatolewa. Leo mpaka Maafisa wetu Maendeleo ya Jamii unawaonea huruma, mtu amesoma, ana elimu yake nzuri, anaitwa Afisa, lakini mtu hata usafiri hana, Afisa gani huyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake katika Halmashauri, anaonekana tu kama na yeye utafikiria ni

Mtendaji wa Kata, ni Mratibu Elimu Kata, yaani haeleweki, thamani yake imeshuka. Naomba Wizara iliangalie hili na naamini yote hayo mtayabaini kama mtatembelea Chuo cha *FDC,* Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi na sioni sababu ya kujazia maneno mengi, naomba kukushukuru kwa nafasi hii, nasubiri majibu ya Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wote wamekwisha. Jioni Mheshimiwa Waziri, utahitimisha hoja yako. Ataanza Naibu Waziri kwa dakika 20 na wewe utamalizia kwa dakika 40.

Nichukue nafasi hii kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Kafumu na Mheshimiwa Aeshi, kwa kurudi tena Bungeni, kupitia Chama cha Mapinduzi. Tunawatakia Bunge jema na Uwakilishi mwema kwa wale waliowachagua.

Baada ya maneno hayo, nasitisha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.48 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE.KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na ibara ya 204 na 205 za ilani ya uchaguzi ya CCM, inayoelekeza mikataba iliyoridhiwa ya Haki za Wanawake na watoto itekelezwe kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya malengo ya utekelezaji wa mikataba hii ni jambo jema ingawaje utekelezaji wake umekuwa mgumu sana. Serikai inatambua kwamba haki za watoto zimekuwa zikiendelea kuvunjwa kwa makusudi kana kwamba hakuna sheria zinazowalinda watoto na wanawake.

Mheshimwia Mwenyekiti, naiomba Serikali iweke mkazo katika kufuatilia udhaifu unaoonekana unadumaza malengo mazuri ambayo kama utekelezaji wake utatekelezwa, basi tunaweza kutokomeza matendo yote yanayodhalilisha wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa na linalohitaji nguvu zaidi kulishughulikia ni suala la ajira kwa watoto, jambo ambalo pamoja na jitihada za kukomesha ajira kwa watoto lakini bado inaonekana linazidi kukua badala ya kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya uchimbaji wa madini na utumikishwaji majumbani ni miongoni mwa maeneo yanayoendelea kuchukua nafasi kubwa katika kuwatumikisha watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ianzishe Idara maalum ya kushughulikia wale wote wanaovunja sheria ya kuwatumikisha watoto wadogo ambao kwa mujibu wa sheria hawaruhusiwi kuajiriwa katika hali yoyote itakayokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali katika kushughulikia juu ya mikakati ya kupambana na ukatili dhidi ya watoto. Ni jambo lisilo na shaka kwamba ukatili dhidi ya watoto katika nchi yetu limekuwa likiongezeka siku hadi siku. Hivyo, ni jukumu la jamii kutoa ushirikiano kwa Serikali juu ya jambo hili ambalo ni la aibu kwa Taifa lolote linalojali haki za binadamu. Naishauri Serikali kuchukua hatua kali kwa wale wote watakaobainika kufanya ukatili kwa watoto, kwani ukatili kwa watoto haukubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Serikali iwatazame kwa macho ya huruma watoto wa Mitaani, kwani ongezeko la watoto wa Mitaani haionyeshi kama Serikali inajali au inachukua hatua stahiki juu ya kudhibiti watoto wa Mtaani.

Mheshimwia Mwenyekiti, pia naiomba Serikali iwashughulikie wazee ambao sambamba na watoto wa Mitaani wametapakaa katika Mji Mikuu katika nchi yetu. Siyo

jambo jema na linatia aibu Taifa kuonekana kama ni Taifa lililoshindwa kuwatunza wazee ambao hawana au wametelekezwa na familia zao.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yangu ni kuomba Serikali itueleze ni njia gani tutafika 50/50 katika ngazi za uongozi hasa Ubunge? Tujifunze kwa wenzetu wa nchi za jirani, wamefikaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri *Bank* za wanawake zifike vijijini pia, au hata Mikoani, lakini waanze kupeleka Mikoa ya pembezoni kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipi tutapata mgao wa Hisa za *Bank* ya wanawake iliyoundwa na mimi nikiwa mwana-Hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGO* nyingi zinazoundwa hazifiki Vijijini, huishia Mijini tu. Nasi tunahitaji huduma za *NGO;* walazimisheni waje Mikoani pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGO* ziache kushabikia maandamano ya wanaharakati. Baadhi za *NGO* hawana mipango, kazi yao ni kushambulia Serikali. Waaswe ili waache lengo la *NGO* ni kusaidia Serikali na siyo kupinga Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho 50/50 iharakishwe katika uongozi.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo matatu katika hotuba hii ya Mheshimiwa Sofia Simba - Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendo vya ukatili kwa watoto, ni kweli Wizara imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na hasa watoto wale ambao hawawezi kujitetea vinadhibitiwa. Pamoja na juhudi za Wizara, bado tabia hizi zipo.

Mheshimwia Mwenyekiti, mara nyingi tumekuwa tukisikia na kushuhudia jinsi watoto wasioweza kujitetea wanavyofanyiwa vitendo vya kikatili ama na mama zao wa kambo ama na baba zao wa kambo ama watu wengine wa kawaida ambao hawako katika kundi la wazazi wala walezi. Sasa Wizara inatumia mikakati gani ya kufuatilia vitendo hivi vya ukatili na hasa kwa familia ambazo siyo rahisi siri zao za kifamilia kutoka nje? Ama Wizara mpaka iambiwe na wadaku wanaozunguka familia hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naishauri Serikali kutengeneza utaratibu maalum wa kupata habari za unyanyasaji na vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto hasa wale wanaolelewa na walezi kwa maana ya mama wa kambo au baba wa kambo.

Mheshimwia Mwenyekiti, sambamba na ufuatiliaji wa vitendo vya ukatili kwa watoto, vitendo vya ukatili kwa akina mama pia vifuatiliwe vyema, bado shida iko. Wanawake wengi wanaendelea kupata mateso makubwa kutokana na mfumo dume uliopo! Wanawake bado wanafanyiwa vitendo vibaya na vya kikatili mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie kuhusu wanawake kuhusishwa katika vyombo vya maamuzi na vyombo vya utawala vya ngazi za juu. Tunaishukuru Serikali kwamba imeanza kutekeleza azima ya 50 kwa 50. Naendelea kuiomba Serikali iendelee kutekeleza azma yake njema ya kuwahusisha wanawake katika vyombo vya juu vya maamuzi. Bado tunaendelea kuomba asilimia 50 kwa 50 ndani ya Bunge. Nategemea pia mwaka 2015 Waziri Mkuu ama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya wanawake Tanzania, naishukuru Serikali kwa kuanzisha Benki ya wanawake Tanzania na nafikiri Serikali ilikuwa na nia njema kabisa ya kuanzisha Benki hii, wanawake wapate mikopo waweze kuinuka kupitia huduma na mikopo kutoka katika Benki hii.

Mheshimwia Mwenyekiti, sasa swali: Je, Benki hii inahudumia na kuwapa walengwa huduma inayostahili? Kuna malalamiko na maswali mengi juu ya huduma ya Benki hii. Hivi ni nani hasa wanafaidika na Benki hii ya wanawake kwa kiasi gani? Ni kweli Benki hii imeshafanya vizuri *so far* katika kuwahudumia akina mama wa kitanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ama Serikali kwa ujumla kuangalia na kupata majibu ya maswali hayo hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ambayo yamepatikana katika kuwakomboa wanawake wa Tanzania toka tupate uhuru, bado kuna wanawake wengi hasa wa vijijini na maeneo mengi ya Mijini ambao wanaendelea kuteseka na kunyanyaswa. Mateso na manyanyaso hayo yanatokana na sababu zifuatazo: athari za mfumo dume, elimu duni, umasikini wa kipato na mila potofu ambazo zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa hapa ni elimu. Wanawake wengi bado hawafahamu haki zao za msingi kwa kuwa hawana elimu ya kutosha. Mahali pengi wanapambana na uonevu, ukatili wa aina mbalimbali unaolelewa na mfumo dume na mila potofu. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kueneza elimu ya haki za wanawake ili kuwawezesha wanawake kuendesha mapambano yao kwa misingi thabiti ya kikatiba na kisheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kubwa inayowakabili wanawake katika mapambano yao dhidi ya mfumo dume ni umasikini unaowakabili wanawake wengi vijijini. Kuhusu hili, bado wanawake wengi vijijini hawana haki ya kurithi mali. Je, Serikali ina mpango gani wa

kupunguza umasikini kwa wanawake wengi vijijini ambao hawawezi kupata mikopo ya aina yoyote kutokana na kutokidhi vigezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea haki za watoto. Hatua ya Wizara kutafsiri Sheria ya Mtoto Na. 21 (2009) ni nzuri na mpango wa miaka mitatu (2012/2013 – 2015/2016) wa kuzuia ukatili dhidi ya watoto ni hatua nzuri pia. Jambo lingine jema ni uanzishaji wa Baraza la Watoto ambalo lilifanya Mkutano mwaka 2012/2013, (ukurasa wa 29 wa hotuba ya Waziri unaonyesha).

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa na mpango huu wa miaka mitatu, ni dhahiri kuwa kuna tatizo katika utekelezaji wa mpango huo kutokana na ufinyu wa bajeti. Mathalan suala la kueneza elimu kuhusu uelewa wa ukatili dhidi ya watoto lilitekelezwa tu katika Mikoa mitatu: Mara, Shinyanga na Singida (ukurasa 28 hotuba ya Waziri).

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sheria ya Mtoto (2009) bado haujapangiwa mpango endelevu ambao utashughulikia changamoto zinazowakabili watoto kikamilifu. Watoto wengi vijijini na mijini (pamoja na watoto yatima na watoto wa mitaani) hawana hakika ya kupata haki zao za msingi (haki ya elimu, afya, chakula bora, malezi na kadhalika) hasa kwa sababu ya umaskini ambao ni changamoto ya msingi katika maeneo mengi. Kama Serikali inataka kwa dhati kutekeleza kikamilifu Sheria ya Mtoto, lazima iandae mpango endelevu ambao utatengewa fedha ya kutosha. Bila kutoa fedha ya kutosha, Sheria ya Mtoto haiwezi kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kumwendeleza mwanamke ili kufikia hatua ya kuwepo usawa wa kijinsia na suala la kutekeleza Sheria ya Mtoto ni suala mtambuka linahusisha mahitaji ya kielimu (jamii kuelewa tatizo) mahitaji ya kiuchumi, mahitaji ya huduma za kiafya na kadhalika. Serikali ina mkakati gani wa kitaifa ili kutimiza mahitaji haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la maendeleo ya jamii ni kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya wananchi ambao wako nyuma kimaendeleo. Kutokana na fungu la fedha kuwa dogo, Wizara haijafaulu kuleta mabadiliko hayo katika sehemu nyingi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maendeleo ya jamii vijijini ni hafifu ama kwa kuwa fungu ni dogo ama maofisa maendeleo hawatimizi majukumu yao kikamilifu: Serikali ina kauli gani kuhusu jambo hili?

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa Wizara hii ikawa na watumishi ambao watatoa mafunzo kwa wananchi ili wananchi waweze kujipatia maendeleo kwa maendeleo ya jamii. Ni muhimu ili kuondoa vijana tegemezi ndani ya familia. Nguvu kazi tunayo, lakini wakipata elimu ya kuhusu maendeleo yao ni ukweli usiopingika watabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuuliza kwa Mheshimiwa Waziri, ikiwa kuna mtu katenda kitendo cha kikatili ambacho kinamdhalilisha mwanamke au motto, yeye kama kiongozi wa Wizara hii anamsaidiaje mwathirika kisheria kama kesi iko Mahakamani? Mfano yule baba aliyemnajisi akamlawiti na kumlazimisha mtoto kula manii yake, mtoto huyo ni wa mkewe tena ana umri wa miaka sita tu. Mtu huyo alisababisha maumbile ya huyo mtoto kuungana yaani alimchana vibaya vibaya. Ni vyema Waziri atakapojibu (majumuisho) atufahamishe hili. Kwani huyu mtu ni mnyama na wanaume wengi wamekuwa na unyama huo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vyema akina mama sasa hivi ndiyo walezi wa familia na ni waaminifu sana, lakini akina mama hawa hawana uwezo wa kujiendesha na wanapokwenda kwenye mikopo, riba ni kubwa ambapo haimsaidii huyo mama na wengi wao huishia kunyang'anywa

vitanda, viti, meza na hata akina mama wengine kushindwa kurejesha na kuzikimbia familia zao. Ni vyema kama mfuko wa mikopo wa wanawake utanenepa na kuweza kukopesha wanawake wengi, kuepuka riba kubwa wanayotozwa akina mama huko kwenye mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wa mitaani, kwa sasa wanazidi kuongezeka kwa kasi. Nini mpango wa Wizara wa muda mrefu na muda mfupi ili kujipanga na kuondokana na ongezeko hilo la watoto wa mitaani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inasimama vipi kuwahamasisha wanawake kukopa na kulipa mikopo hiyo? Kwani mfuko wa 5% huko katika Halmashauri wakopaji wengi hawarejeshi, sababu kubwa ni kuwa watumishi wa Halmashauri hutoa mikopo hiyo kikada na kindugu na kwa kuwa mkopaji hatalipa mkopo huo, hakuna sheria ya kumfikisha Mahakamani. Ni lini basi sheria au kanuni ya mfuko huu itabadilika ili tuendane na kopa urejeshe na mwingine akope? Ni vyema Wizara ikapata pesa ya kutosha katika Wizara hii; majukumu ni mengi, lakini pesa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri katika kazi zenu. Ahsante.

**MHE. HAMOUD ABUU JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ya mwaka 2013/2014. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa bajei nzuri na yenye mikakati ya kutatua matatizo yanayozikabili sekta hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu limekuwa likikabiliwa na tatizo la watoto wa mitaani. Watoto hao hutokana na kwamba, baada ya kuzaliwa na mama zao na kushindwa kuwalea huwatelekeza. Tatizo hili limekuwa sugu kiasi ambacho ukienda kila kona ya Miji yetu lazima utakutana na watoto hawa.

Mheshimwia Mwenyekiti, Serikali kushirikiana na Taasisi za kiraia, naomba iweke mikakati madhubuti ya kuwatengea fungu watoto hawa kuwatunza na kuwasomesha, kwani ndio viongozi wa Taifa la kesho. Watoto hawa wengi wao waliopo Mijini huombaomba mitaani na sehemu mbalimbali nyakati za usiku na mchana wakiwa peku, nguo chakavu na hulala vibarazani. Mbaya zaidi, watoto hawa hujichanganya kati ya wakike na wakiume kitu ambacho ni hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kutatua tatizo hili, lazima tuanze kuwajengea njia nzuri wanawake, kwani ndiyo chanzo ukiachia mbali mwanaume ambaye anahusika pia katika tatizo hili, ila mama ambaye ndio huchukua jukumu zima la malezi na makuzi ya watoto hawa, wamekuwa wakitelekezwa pindi wapatapo ujauzito na kujifungua.

Mheshimwia Mwenyekiti, hali hiyo hutokana na mwanamke huyu kutokuwa na uwezo wa kujiendesha kimaisha na kuwa tegemezi na kutokuwa na uwezo wa kujitimizia mahitaji yake ya kila siku pamoja na familia ambayo ameachiwa. Lakini wanawake hawa wangewezeshwa kielimu ama kwa kupewa mitaji midogo midogo ili waanzishe biashara ambazo zingewasaidia katika majukumu yao ya kila siku na hivyo kuweza kumudu kulea watoto na siyo kufikiria kuwatelekeza mitaani.

Mheshimwia Mwenyekiti, Mkakati huo utasaidia hata pindi atakapokimbiwa na mwanaume ataendelea kulea watoto wake vizuri na hata kuweza kusomesha kwa uwezo mdogo aliowezeshwa, kwani akina mama ni walezi wazuri wa familia pale wanapokuwa na uwezo huo. Hilo lingesaidia sana kupunguza tatizo hili la kuwa na watoto wa mitaani.

Vile vile Serikali kupitia Wizara, ingeboresha uelimishaji akina mama katika kukuza biashara zao, kwani hivi sasa kwa akina mama wengi ambao wako katika maisha ya chini hufanya biashara ndogo ndogo ambazo haziwezi kuwakwamua kiuchumi na kubadilisha maisha yao.

Mheshimwia Mwenyekiti, hali hiyo husababishwa na mitaji yao, kwani ni midogo sana na kukosa elimu ya kutosha ya ujasiriamali. Napenda kuishauri Serikali kutillia mkazo kwenye hili kwa kuwajengea uwezo akina mama kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali ili waanzishe biashara kukidhi mahitaji yao pamoja na familia kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuendelea kutoa elimu kwa jamii ya wafugaji ili na wao wabadilike na waendane na karne hii, kwani jamii hiyo bado ina mila potofu za ukeketaji watoto wa kike na kuwaozesha watoto hao wakiwa katika umri mdogo kwa kuwaachisha shule.

Mheshimwia Mwenyekiti, pia watoto wa kiume huachishwa shule ili wakachunge ng'ombe. Tatizo hili hurudisha nyuma maendeleo ya jamii za wafugaji. Yahitajika elimu ya kutosha kutolewa kwa wananchi wa jamii ya wafugaji ili kuondokana na mila hizo potofu na taratibu zilizopitwa na wakati. Hali hiyo itasaidia sana kuleta mabadiliko katika jamii hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Serikali kuendelea kuanzisha Vyuo vya Maendeleo ni jambo muhimu sana ukizingatia idadi ya wanaojiunga na masomo kwenye Vyuo hivyo bado haitoshi. Kufanya hivyo kutaisaidia kupata wataalam wengi katika sekta hiyo, kwani tumekuwa na upungufu wa wataalam wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii ambayo kimsingi ni muhimu katika Taifa letu. Wakipatikana wataalam wa kutosha watatawanywa karibu nchi nzima na kusaidia kuondokana na changamoto zilizopo ambazo baadhi zimekuwa sugu na hazina budi kutafutiwa ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kibaha Vijijini tunakabiliwa na matatizo mengi yanayohusu Maendeleo ya Jamii, Jinsia pamoja na Watoto. Tumekuwa na watoto wengi wasiokuwa na wazazi ambao wametokana na kufiwa na wazazi wao na kukosa ndugu wa kuwalea na hivyo kuanza kujitegemea katika umri mdogo na baadhi imetokea watoto kulea watoto wenzao.

Mheshimwia Mwenyekiti, Hali hii inasikitisha sana, lakini wamekosa msaada wowote kutoka kwa jamii iliyowazunguka na hata Serikalini. Hii inaonyesha Serikali kuwasahau ama Wizara kutokuwa na takwimu za kutosha za watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu wako maeneo gani, Vijiji gani na Kata gani.

Mheshimwia Mwenyekiti, watoto hawa hupata shida, inafikia kujiingiza katika biashara ndogo ndogo ambazo hufikia kudanganyika na kuanza kushiriki biashara za ngono wakiwa na umri mdogo. Hufanya hivyo ili kujipatia riziki ilhali kujiingiza katika matatizo makubwa ya maambukizi ya Ukimwi na magonjwa ya zinaa na wengine hupata mimba zisizotarajiwa na kuzidi kukua kwa tatizo hili.

Mheshimwia Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia Wizara husika, kuwajengea uwezo watoto hawa kulingana na umri wao ama kwa kuwaendeleza kielimu, kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali kwa wale wanaofaa kupewa elimu hiyo na kuwapa mikopo midogo midogo ili kuanzisha biashara ndogo ziweze kuwasaidia.

Mheshimwia Mwenyekiti, Wale ambao bado wako kwenye umri mdogo kabisa, basi naiomba Serikali kupitia Wizara kujenga hata kituo kimoja katika Jimbo letu la Kibaha Vijijini cha kulelea watoto yatima ili kuepukana na hizi athari wazipatazo watoto hawa sasa katika Jimbo letu. Kukamilika kwa kituo hicho kutasaidia kuwakusanya watoto wote waishio katika mazingira magumu na kupata msaada moja kwa moja kutoka Serikalini na kwa wafadhili ikibidi, wakipatikana.

Hata hivyo, napenda kuiomba Serikali kuweka utaratibu pale Wizarani wa kuwatawanya wataalam katika sekta hii maeneo mbalimbali nchini ili kufanya tathmini na kujua ukubwa wa tatizo. Pia nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri aje afanye ziara katika Jimbo la Kibaha Vijijini ili kujionea hali halisi katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii katika vipengele muhimu vitatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu wimbi kubwa la watoto wa mitaani na ombaomba. Hii sasa imekuwa ni biashara ya watu, lakini Serikali imekaa kimya na kando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukaa kimya kwa Serikali kunaruhusu na kupelekea Miji yote kujaa ombaomba na watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumaliza hili tatizo, ninashauri kila Halmashauri ianze kutenga fungu kwenye mapato yao, kisha wajenge kituo cha kisasa ambacho kitatumika kuwahifadhi ombaomba na watoto wa mitaani kwa nguvu. Ila katika kutekeleza hili, lazima sera iletwe na itamkwe rasmi kuwa watakaokuwa wanaombaomba na kukaa mitaani watapelekwa kwenye vituo hivyo ambavyo lazima viwe na huduma zote za kijamii kama vile elimu, afya, maji, umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vituo hivyo viwe vyenye tija, naishauri Serikali iwe bunifu na kuanzisha miradi midogo kama vile shughuli za ufugaji, kilimo na kuwepo na zana mbalimbali za kujifunzia ufundi. Hili litasaidia sana na kuwafanya wawe wawajibikaji kwenye Taifa lao, huku likiwaongezea kipato na baadaye watakuwa wakiondoka kituoni na kwenda kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika vituo hivyo kuwepo na utaratibu wa kufanyiwa *counseling* yaani ushauri nasaha; itolewe elimu mbadala ambayo itawasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni juu ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii kilichopo Wilayani Tarime. Chuo kile kimetelekezwa kwa muda mrefu na hadhi yake imeshuka wala huwezi kuamini kama ndiyo chuo ambacho Wizara ya Elimu imekuwa mara kadhaa ikijinasibu kuwa ndiyo mbadala

wa Chuo cha Ufundi *(VETA)* kwa Wilaya inazozunguka, kitu ambacho ni cha uongo kabisa, kwani Chuo hicho hata Shule ya Msingi zinakizidi hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo hakina zana za kujifunzia, hakina Maabara, hakina miundombinu ya maji, hakina jiko, hakina Maktaba, hakina vifaa maalum vya kujifunzia kama vile *computer*, cherehani, *mechanical equipments, electronical equipments, carpentry equipments etc*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Chuo hiki kina madeni mengi na makubwa ya umeme na maji hata Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia Simba alipotembelea Chuo hicho aliweza kuainishiwa matatizo na maombi ya fedha za bili ya maji na umeme, na aliahidi kulipa deni hilo. Lakini cha ajabu, tangu mwaka 2011 hadi leo deni halijaweza kulipwa. Tuomba Serikali iweze kupeleka fedha mapema katika Vyuo hivi hasa hiki cha Tarime *(TFDC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika chuo hiki kuna uhaba wa watumishi kama vile wakufunzi, walinzi, wapishi wote kwa ujumla wao, kuna upungufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni juu ya Benki ya Maendeleo ya Wanawake na Mfuko wa Maendeleo unaopelekwa kwenye Halmashauri zetu. Benki hii inatakiwa kusambazwa hadi kwenye Wilaya zetu ili lengo kuu likamilike na siyo kwa watu wachache tu. Kuhusu fedha za Mfuko wa Maendeleo kwa wanawake, ni chache mno na huwafikia wasio walengwa.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuhakikisha usawa wa kijinsia katika nyanja zote unaendelea kuwepo pamoja na haki za Binadamu kufuatia mikataba mbalimbali ya Kimataifa – Hongera Waziri na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la unyanyasaji wa kijinsia ambapo wanawake wengi wanapigwa ua kuuwawa. Pia hata wengine kutumia lugha za udhalilishaji kwa wanawake na watoto. Hili ni tatizo na hupelekea baadhi ya familia kutengana na mwishowe watoto wanakuwa hawana mwelekeo na kuingia Mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wahusika wachukuliwe hatua kali ili kutokomeza tatizo hili. Pia elimu ya jinsia izidi kutolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, vikundi vya Sanaa/Ngoma za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za Wizara hii za kushirikiana na baadhi ya asasi zisizokuwa za Kiserikali, ni budi zipongezwe kwani zimeleta mafanikio kwa baadhi ya jamii na kuanza kutokomeza mila potofu zilizopitwa na wakati kama ukeketaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, naomba Serikali ifikirie kuanza kuongeza bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa Mitaani au wanaoishi katika mazingira magumu ni tatizo sugu chini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri miongoni mwa hotuba zake katika kupambana na tatizo hili, alisema kwa kuiomba Serikali kwamba kuna haja ya kuandaa/kutenga bajeti maalum ya ziada kwa ajili ya kuwarejesha watoto hao wa Mitaani kwa familia zao. Hiki ni kilio cha Taifa. Ni vipi Serikali itasaidia hii Wizara? Watoto hawa wanaathirika Kisaikologia, kielimu, kiafya na hata wengine kubakwa au kupata mimba za utotoni na pia kukosa kujiendeleza wakati Taifa tunawategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini jukumu la Mikoa katika kusimamia uondoaji wa watoto wa Mitaani ambao wamejaa kwenye Makao Makuu ya Mikoa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa na Mikoa mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa watoto wa Mkoa wa Dar es Salaam ambao wanazagaa na Mkoa haujachukua hatua zozote? Wizara haina fungu la kutosha. Sasa juhudi zipi zitakazochukuliwa ili kuondoa tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza bajeti ya Wizara hii kutokana na majukumu yake kwa Jamii ambapo sote ni mashahidi kutokana na utendaji wao mzuri pamoja na fedha chache wanazopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iangalie uwezekano wa kurudisha fungu la fedha za Maendeleo kwa wanawake kwenye Wizara hii badala ya utaratibu unaotumika sasa. Fedha hizi zikipitia Wizarani, wanawake watazipata kwa urahisi kupitia kwenye maeneo yao na pia Wizara itaweza kubaini maendeleo yao na hata kama kutakuwa na upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate majibu, ni lini Serikali itarudisha fungu hilo la fedha za Maendeleo kwa wanawake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia naomba majibu.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Jinsia na Watoto kwa kazi nzuri anayofanya. Serikali ina Sera nzuri sana ya kutaka kuinua hali za wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali imezitaka Halmashauri za Wilaya kutenga 10% ya fedha wanazokusanya kusaidia miradi ya wanawake na vijana, lakini upo ushahidi kwamba Halmashauri nyingi hazitengi fedha hizo kwa ajili ya kusaidia makundi hayo. Hata kama fedha hizo zinatengwa haziwafikii akina mama na vijana. Naomba kujua Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inachukua hatua gani kurekebisha kasoro hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Halmashauri nyingi zina fikra hasi kuhusu kusaidia miradi ya wanawake. Katika Jimbo langu la Vunjo, nilijaribu kutenga fedha kutoka mfuko wa Jimbo ili kuwawezesha wanawake wanufaike na fedha hizo kwa kusaidia vikundi vyao. Lakini jambo hili lilikabiliwa na upinzani kwa madai kwamba fedha hizo ni kwa ajili ya kutengeneza barabara, shule, maji na kadhalika, na siyo kwa ajili ya kuwawezesha wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua msimamo wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejionea kwa muda mrefu ukiukwaji wa usawa wa kijinsia, unyanywasaji, ubaguzi na ukatili unaofanywa dhidi ya wanawake. Imefikia wakati ianzishwe Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Usawa *(National Gender & Equality)* ili ifanye Kaguzi za Kijinsia *(Gender Audit)* yaani:-

-Kusimamia kutathmini, kuchunguza na kuchukua hatua dhahiri za kukosa pale ubaguzi wa wanawake kisheria na katika misingi ya haki za kijamii unapodhihirika na katika kufanya hivyo, kupiga vita aina zote za ubaguzi dhidi ya Wananchi.

-Itasaidia kuhakikisha kutekelezwa kwa mikataba inayopinga ubaguzi.

-Kuhusisha kikamilifu maono ya haki za kijinsia katika maamuzi yanayohusu Sera zote za Kitaifa, utungaji wa Sheria, Mipango ya Kimaendeleo katika nyanja zote za maisha na kuhakikisha utekelezaji wa Kikatiba wenye matokeo. Ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu anieleze kama kuna mpango wowote wa uundwaji wa Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kazi inayofanywa na Maafisa wanaoshughulikia masuala ya Kijinsia katika Wizara. Ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze wanapatikanaje na wanatakiwa kuwa na vigezo vipi kwani wako Maafisa ambao hawana utashi wa masuala ya kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wanawake wengi wanafanyiwa ukatili wa kijinsia au kingono; je, kuna nyumba zilizotengwa kwa ajili ya wanawake hao ili wahifadhiwe na kupewa ushauri nasaha na msaada wa Kisheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mashirika mengi yasiyokuwa ya Kiserikali yanayoanzishwa kwa nia ya kusaidia wanawake na watoto waishio katika mazingira magumu. Baadhi ya Mashirika haya yanafanya kazi zake kwa ufasaha kwa lengo hasa la kumkomboa mwanamke na watoto waishio katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Mashirika haya vilevile hayafanyi kazi zake kwa kuzingatia madhumuni ya uanzishwaji wake, badala yake yananufaisha wahusika walioyaanzisha. Mashirika haya pia yanajikita Mijini tu na kusahau kuwa wahitaji wakubwa na huduma zao ni Wananchi wa Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *NGO* ya mwaka 2002 inatoa utaratibu na kusimamia kifungu cha 7(1)(a), kinachoeleza jukumu la kuondoa na kuratibu *NGO* zote zilizotanguliwa na kupitia ripoti za kila mwaka za *NGO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kumuwezesha Mwanamke na kuanzisha Benki ya Wanawake, lakini sisi Wanasiasa, Wanawake wa Vijijini hawatuelewi siku zote wanapoona huduma haziwafikii hasa akina mama wa Mkoa wangu wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu ni lini Wanawake wa Iringa wataanza kuona Tawi la Benki hiyo linafunguliwa au hata *Mobile Bank* tu kwa kuwa sasa hivi kuna muungano wa Benki nyingi (Umoja), maana kuna baadhi ya Taasisi za Fedha zinawadhalilisha wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo, ukurasa wa 96 wa Kitabu cha Maendeleo, zimetengwa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa vyuo. Pesa hii ni kidogo

sana ukilinganisha na uhitaji na ukarabati wa vyuo hivyo. Vipo katika hali mbaya sana, *OC* hazifiki kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa sasa Madawati ya Kijinsia yapo karibu kila Mkoa ukiwepo Mkoa wa Iringa, japokuwa yanahitaji maboresho. Madawati haya yanatakiwa kuhamasishwa ili yafunguliwe katika ngazi ya Wilaya, Kata na Kijiji. Wanawake wengi sana wa vijijini hawana Elimu ya kutosha na wana uhitaji mkubwa wa msaada wa Kisheria hasa kutokana na Sheria kandamizi zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utaona hizi Taasisi zinazowasaidia wanawake msaada wa Kisheria, ofisi zake zipo mijini tu. Tunaomba Wizara hii itueleze jinsi itakavyoweza kusaidia ili akina mama wa vijijini waweze kufikiwa. Ushauri wangu pengine kila Shirika lingepewa Kanda yake ili tuweze kupima utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iongezewe pesa ya kutosha kwa ajili ya kukabiliana na changamoto nyingi zilizopo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Chuo cha Maendeleo cha Malya inaonekana kama vile ni mzigo kwa Wizara; je, Serikali itakubaliana nami kama ambavyo nimekuwa nikipendekeza na kuiomba Serikali ikubali kukiachia Chuo hicho ili kitumike kama Chuo cha Ufundi au kitumike kama mabweni kwa ajili ya wasichana wa sekondari wa kidato cha tano na sita na majengo mengine yatumike kama madarasa kwa ajili hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Wizara imekitelekeza Chuo hicho hadi inapelekea Mbunge kulisha wanafunzi. Pia Chuo kinadaiwa na Wazabuni na Wakandarasi waliotoa huduma katika Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nawasiliana mara kwa mara na ofisi yako kuhusu Watumishi au Walimu wa chuo hicho, lakini kila mara jibu limekuwa ni ufinyu wa bajeti. *OC* kwa chuo hicho imekuwa ni historia na ndiyo maana kwenye kitabu chako cha bajeti kuanzia ukurasa wa kwanza hadi ukurasa wa 46 au kwenye *cover* ya kitabu, hakuna sehemu Chuo cha Malya kimetajwa na hata kwenye *cover* ya nyuma mnajionesha wenyewe tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niambiwe ni kwa nini Chuo hiki hakikutajwa kwenye Kitabu cha Hotuba au ndiyo kimehamishiwa Wizara ya Elimu kitumike kama Chuo cha Ufundi? Naomba majibu. Nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ustawi wa Jamii kilichopo Mufindi cha Rungemba, kinatoa Stashahada na kinasomesha wanawake tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa Serikali ikakipandisha hadhi na kuanza kutoa Shahada na sasa Wananchi wa Kijiji cha Rungemba wamekubali kukiachia ardhi Chuo, sehemu iliyokuwa na mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Mheshimiwa Waziri na Naibu wake watakitembelea Chuo hiki ili kujua changamoto zilizopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mufindi ina Watoto 18,000 wanaoishi katika mazingira hatarishi na uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kuwasaidia watoto hawa ni mdogo. Je, ni lini Serikali itaongeza nguvu kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kuweza kuwasaidia watoto hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wengi wanaopoteza wazazi wao wote wawili kutokana na UKIMWI, wanaishi katika mazingira magumu sana na hatarishi. Waliopo vijijini hujaribu kukimbilia mijini wakitegemea kupata hali nzuri na unafuu kimaisha. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha watoto wa aina hiyo wanapatiwa elimu bure kwani elimu ni nguvu na ndiyo njia pekee ya kujiwezesha maishani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ya Maendeleo ya Jamii inawasaidiaje watoto wanaofiwa na wazazi wao, ambapo mirathi husimamiwa na ndugu na jamaa na kuna baadhi ya watoto ambao hukosa kabisa mali zilizoachwa na wazazi wao na hubakia maskini hata pale ambapo wazazi walikuwa na uwezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Watoto ambayo yanafanya kazi nzuri katika kutetea haki za watoto; Wizara inashiriki vipi katika kuwapa *support* Viongozi wa Mabaraza ya Watoto ambao wengi hukutana na vikwazo vingi hasa kutoka kwa Wananchi na Viongozi ambao hawana uelewa wa Mabaraza hayo ya Watoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa ajenda ya watoto ni jambo zuri lililoanzishwa ili kutetea haki za watoto hapa nchini. Kwa kuwa kama tafiti zinavyoonesha zaidi ya nusu ya Watanzania ni watoto. Imeonekana ni jambo muhimu kuwekeza kwa watoto ili kuwanufaisha watoto pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo kumi ya kipaumbele kwa ajenda ya watoto, je, Wizara imetenga kiasi gani cha fedha ili kufanikisha ajenda za watoto pamoja na vipaumbele vilivyowekwa ambavyo ni kuokoa maisha ya watoto na wanawake, lishe bora, udhibiti wa miundombinu na majitaka katika shule, kumwendeleza mtoto akiwa bado mdogo, elimu bora kwa watoto na pia kuzifanya shule kuwa mahali pa usalama, lakini pia kuwalinda watoto wachanga

na wasichana dhidi ya VVU, kupunguza mimba za utotoni, kuwanusuru watoto na vurugu, udhalilishaji na unyonyaji na pia kuweka kwa watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imepunguza kwa kiwango kikubwa umaskini na hivyo kuwa na Taifa linalostawi na la usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa lishe bora kwa watoto walio wengi na hasa waishio vijijini. Inakadiriwa kwamba zaidi ya theluthi moja ya watoto wa Tanzania wamedumaa na hawafiki kiwango chao cha ukuaji kimwili na kiakili kutokana na utapiamlo ambao unasababisha vifo kwa watoto walio wengi katika umri mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu zaidi itolewe kwa familia zinazoishi mijini na vijijini kwa njia ya redio kuhusu umuhimu wa kula au kuwapatia watoto na familia chakula bora yakiwemo matunda ya kila aina ambayo yanapatikana katika maeneo mengi ya nchi yetu. Tatizo lililopo ni kwamba, wananchi wengi hawaoni umuhimu wa kula matunda. Zipo mila na desturi za baadhi ya makabila ambayo wanaume hawapaswi kula matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma katika redio Tanzania ambayo ndio ilikuwa redio pekee hapa nchini, ilitumiwa sana na viongozi wetu chini ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kutoa elimu ya umuhimu wa kula chakula bora kwa kuwatumia wasanii wa muziki. “Kuleni kuku, mayai, mboga, samaki, maziwa,” hicho ni kibwagizo kilichosikika sana redioni wakati huo. Serikali ione umuhimu wa kuwatumia wasanii wetu kutoa elimu ya umuhimu wa kula matunda na vyakula bora vinavyopatikana katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2007, zaidi ya wasichana 8,000 waliacha shule kutokana na mimba za utotoni. Hii ni idadi kubwa sana na imeonekana kwamba idadi imeongezeka karibu kila mwaka ya wasichana wanaokatiza masomo kutokana na mimba wakiwa mashule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi wanaowapa mimba wasichana hawachukuliwi hatua zozote na wengine humaliza tatizo hili kimila nyumbani. Anayeathirika ni msichana kwani maisha yake huwa yamekwishaharibiwa. Endapo ni mwanafunzi mwenzake kampa mimba, mvulana huendelea na masomo huku msichana akirudi nyumbani kulea mtoto mwenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke Sheria ya kumlinda mtoto wa kike, endapo kwa bahati mbaya amepata mimba akiwa shuleni, basi, uwekwe utaratibu wa kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Aidha, elimu ya uzazi itolewe mashuleni kote ili wanafunzi wajue mimba zinatungwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake ambayo inaendesha shughuli zake Jijini Dar es Salaam, imekuwa msaada mkubwa kwa wanawake wachache waishio Jijini Dar es Salaam. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Benki kama hiyo ya Wanawake inaanzishwa vijijini ili kuwanufaisha wajasiriamali wanawake wanaoendesha shughuli zao za kujipatia kipato vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni ndogo sana na inapungua mwaka hadi mwaka. Naishauri Serikali iongeze bajeti itakayoendana na hali halisi ya mazingira yanayowakuta watoto na akina mama. Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vina uchakavu mkubwa kiasi kwamba, hata wanachuo wanaosoma kwenye vyuo hivyo, vinawakatisha tama. Naomba Serikali ije na mpango mkakati wa kuviboresha vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa kwa akina mama walio wengi kutokupata mikopo hiyo ya ujasiriamali, kwani walio wengi wanapopata mikopo hiyo kwa kununulia mavazi, jambo ambalo siyo lengwa kwa mikopo hiyo. Ni vizuri Serikali ikaandaa semina kwa Wanaushirika na

Vikundi ambavyo vinaundwa kuhakikisha wanapata elimu ya ujasiriamali ambao utawasaidia kusimamia Miradi ambayo imeibuliwa na kupewa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa mitaji ni tatizo kubwa sana kwa akina mama hasa wanaoishi vijijini, hawapati fursa za mikopo. Mikopo mingi inayotolewa inaelekezwa maeneo ya Mjini, jambo ambalo siyo sahihi. Akina mama walio wengi na wazalishaji wanaishi maeneo ya vijijini. Naiomba Serikali ihakikishe Halmashauri za Wilaya zinapeleka fedha za mikopo kwa akina mama wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri au Wilaya ni wachache sana na kufanya washindwe kusimamia shughuli za Maendeleo katika Halmashauri za Wilaya. Naishauri Serikali iongeze Wataalamu hasa katika Halmashauri ya Mpanda ambako kuna uhaba mkubwa wa Wataalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja hii kama yatafanyika marekebisho ya nyongeza ya bajeti ambayo inastahili kwa ajili ya Maendeleo ya Taifa letu.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii, kwa kadiri ilivyoainisha mikakati ya kupambana na changamoto zinazowakabili watoto na akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ipo katika kujenga uwezo wa akina mama ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Katika Jimbo langu la Bukene, akina mama wengi hujishughulisha na kilimo kwa kipindi cha miezi mitatu ya masika, baada ya hapo hukaa miezi tisa kila mwaka bila kuwa na shughuli mahususi ya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba, ni lazima tuwe na mikakati na mipango ya makusudi itakayowapa uwezo hawa akina mama ili kwa kupitia katika vikundi vyao, waelimishwe na wapatiwe

mikopo waweze kuwa na shughuli za kiuchumi katika kipindi cha miezi tisa kila mwaka, kipindi ambacho hakuna shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyingine ni Mfuko wa Mikopo kwa Akina Mama katika Halmashauri za Wilaya hauleti matokeo yaliyokusudiwa. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ina vikundi vichache sana ambavyo vimefaida na Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu ni ufuatiliaji wa Idara za Maendeleo ya Jamii ya Halmashauri; hoja hapa ni kwamba, suala la muhimu siyo tu kuwapa fedha hawa akina mama, bali ni kuwafuatilia kwa karibu ili kuona kuwa uwezeshwaji walioupata unabadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni ombi kwamba, Benki ya Wanawake ifungue mikopo Mikoa yote, angalau Tawi moja kwa kila Makao Makuu ya Mikoa na pia wanaweza kufanya mazungumzo na mtandao wa Benki za *NMB* au Benki ya Posta ili Benki ya Wanawake iwe na dirisha kupitia Benki hizi ili akina mama wa maeneo ya vijijini wapate fursa ya mikopo na mafunzo ya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu nchi imekuwa katika hali mbaya juu ya unyanyasaji wa watoto. Kutokana na kadhia hiyo, naitaka Serikali iondoe tatizo hilo na kuweka adhabu kali kwa wafanyaji pamoja na kuondoa tatizo hilo kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamko makubwa ya vijana kukosa ajira zinazotolewa na Serikali au Taasisi. Hivyo, kutokana kadhia hiyo, naitaka Serikali kulisimamia suala hilo ili vijana wapate ajira kama inavyohitajika.

**MHE. BETY E. MACHANGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inapaswa kuwa muhimu kwa sababu inabeba

asilimia 51 ya Wakazi wa Tanzania, wanawake na watoto wana matatizo mengi. *Welfare* mbaya ya wanawake inapelekea kutelekeza watoto na hivyo kuzalisha watoto wa mtaani. Kuna haja Serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii, ili iwape nafasi Viongozi kuwaendea wanawake vijijini na hasa kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa hawa wapewe mafunzo, waunde Vikundi vya Wanawake katika Kata, wawafundishe mambo ya lishe bora, malezi bora ya watoto, ya famila na yote yanayoambatana na fani yao. Zamani waliitwa Bibi Maendeleo na waliwafundisha mama zetu kupika, kufuma, miradi midogo midogo ya ujasiriamali na kadhalika. Sasa hivi Bibi Maendeleo wanaonekana kuwa *idle* na wakati mwingine wanaonekana kutokufahamu majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vingi vimedorora na havifanyi ukufunzi wa kozi zinazolengwa. Uhaba wa fedha na *management* umevifanya vikadorora. Nashauri Serikali irekebishe vyuo hivi ili vifundishe masomo ya Cheti na Stashahada na walengwa wanaweza kuwa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne. Wananchi inawezekana wakafurahia Cheti cha Wizara hii kuliko Cheti cha *VETA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo muhimu la *adoption* ya watoto yatima ambalo linafanywa na Idara ya Ustawi wa Jamii, Wizara ya Afya. Kumekuwepo na malalamiko mengi nchini ya urasimu mkubwa wa kuasili watoto. Maafisa wa Ustawi wa Jamii Mikoani wamekuwa chanzo cha urasimu na hata Viongozi wachache katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linafanya watoto yatima ambao wangekuwa na mama na baba na kupata mapenzi ya wazazi hawa, kukosa fursa hii na badala yake kubaki na kukulia katika vituo vya watoto yatima nchini ambavyo matunzo yake ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii ya Wanawake walifuatilie jambo hili na ikiwezekana kuitaka Serikali iihamishe Idara hiyo ya Ustawi wa Jamii ihamie Wizara ya Mama na Mtoto ili kuondoa urasimu huu. Wizara ya Wanawake pia inaweza kufanya kampeni ili watoto wengi zaidi ambao ni yatima wawe *adopted* na familia ambazo zipo tayari kufanya hivyo. Watanzania asilimia kubwa hawafahamu kuwa wapo watoto wadogo katika vituo ambao wanaweza kuasiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye Wizara hii kama Hotuba ya mtoa hoja ilivyowasilishwa. Naomba nizungumzie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bunge kutunga Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, ikiwa na lengo la kuwalinda watoto dhidi ya ukatili, lakini bado kuna matukio mengi sana tena mengine ya kutisha na kusikitisha wanayofanyiwa watoto; wananyanyaswa, kuonewa na kudhalilishwa. Asilimia kubwa matokeo ya utafiti wangu binafsi ni watoto ambao wazazi wao walishafariki au kutengana, lakini kuna watoto ambao wanafanyiwa ukatili na wazazi wao wa kibailojia kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ihakikishe wote wanahusika katika matendo ambayo yanaonea, kudhalilisha au kunyanyasa watoto, Sheria kali zichukuliwe tena haraka sana. Kuna tukio lilitokea hivi karibuni Manispaa ya Shinyanga, Kata ya Ndala, mtoto mdogo wa kike alibakwa na mwendesha baiskeli na kutobolewa macho na hivyo kumsababishia upofu mtoto huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa mwanaume aliyefanya unyama huo inavyosemekana ameshakamatwa, ninaomba Serikali ifuatilie suala hili kwa ukaribu ili tabia hizo

zikomeshwe. Naomba kujua mtuhumiwa huyo apewe adhabu kali ambayo itakuwa fundisho kwa wanaume wengine wenye tabia hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ambayo inaruhusu msichana ambaye yuko chini ya miaka 18 kuolewa. Sheria hii inamhusu msichana kuolewa akiwa na miaka 15, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi miaka 15 ni mtoto bado. Ninaomba Serikali iangalie upya Sheria hii ambayo inamnyima haki mtoto huyo na iongeze umri hadi kufikia miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii inakinzana hata na ile ya kupiga kura kwani msichana huyo anaruhusiwa kuolewa lakini haruhusiwi kupiga kura. Ninaomba Sheria hii kandamizi ifanyiwe marekebisho haraka. Kibaya zaidi, imeegemea upande mmoja tu wa mtoto wa kike na si mtoto wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa wanawake hasa kwenye ndoa. Kuna malalamiko mengi sana wanayopata wanawake katika nyanja zote, kijamii, kisiasa na pia kiuchumi. Nikianza na kijamii; wanawake wengi wananyanyaswa sana ndani ya familia zao, wawe wameolewa au kufiwa (wajane). Tatizo kubwa ni pale mwanamke anapofiwa na mumewe, wanawake wengi wananyanyasika sana na kukosa haki ya kurithi mali za waume zao. Naomba Serikali ilinde Sheria ambayo itamlinda huyu mama mara anapofiwa na mumewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu ambacho kimekuwa kikiwafanya wanawake wengi ndani ya ndoa kudhalilishwa na waume zao. Wanawake wengi wamekuwa wakibakwa na waume zao. Nazungumza hivyo kwa sababu tendo la ndoa bila ridhaa yako ni kubakwa, lakini wanawake hawa hawatambui kama ni udhalilishwaji. Naiomba Serikali iangalie namna ya kutoa semina kwa makundi husika ili mambo haya yasitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kesi nyingi nchini ambazo zinaonesha kabisa ukatili dhidi ya wanawake. Wengi wamekuwa wakipigwa na pengine kupata ulemavu wa kudumu na hata wakimwagiwa tindikali na waume zao, lakini sijaona kesi ngapi tayari zimeshasikilizwa na hukumu kutolewa. Hivyo, naomba kujua ni kesi ngapi zipo Mahakamani za wanaweke walioonewa na waume zao na wanaume wangapi tayari wameshachukuliwa Sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la watoto wa mtaani, ninaomba Serikali ione kuna umuhimu sasa wa kujenga vituo vya kulelea watoto hawa ambao wamezagaa kila kona ya miji yetu. Vituo vikiwa vingi tatizo hili linaweza kupungua kwa asilimia kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania bado haijafanya kazi vizuri kwani hadi sasa haijatanua wigo wake hadi katika mikoa au wilaya nyingine nchini isipokuwa Dar es Salaam tu. Pia ni vyema kuangalia upya mtaji ilionao Benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anajumuisha Hotuba yake ni vyema atupatie ufafanuzi wa kina ni sababu zipi zinazopelekea Benki hii kubaki Dar es Salaam pekee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mwenendo mzima wa Mashindano ya Warembo Tanzania, bado suala zima la mila na desturi zetu za Kitanzania linapuuzwa. Kuna warembo ambao hupenda kuvaa mavazi yasiyo na staha na pia wanashindwa hata kuongea Lugha yetu ya Taifa (Kiswahili).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tuliweza kuuona hapa Bungeni wakati *Miss Tanzania* aliposhindwa kuongea Kiswahili mbele ya Wabunge wakati wa Semina ya *Albinism.* Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Sheria mpya ambazo zitalinda

mila, silka na desturi ya Taifa letu wakati wa mashindano haya ili pale atapopatikana mshindi ieleweke vyema kwamba huyu ni mwakilishi wa Tanzania?

Je ni kwa namna gani vigezo vya kumpata *Miss Tanzania* vizingatie wanawake wembamba tu na kuwaondoa wale wote ambao ni wanene; huu siyo ubaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hali ni mbaya sana kutokana na ukatili unaondelea kufanyiwa wanawake kwa kunajisiwa, kunyimwa haki zao za kimsingi pia kulawitiwa kinyume cha maumbile. Kutokana na taarifa za Kipolisi, bado hali inatisha. Watoto wa mitaani wanaendelea kuongezeka mijini. Ni vyema kupitia na kuangalia upya Sheria zetu na kama zina upungufu, ziletwe Bungeni ili hatua kali zaidi za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, kuunda vikosi kazi katika Halmashauri zetu ili kudhibiti wimbi la watoto kukimbia vijijini na kuja mjini kwa ajili ya kuwa ombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vyema kutoa mafunzo na semina nyingi katika Halmashauri zetu ili kuelezea haki na wajibu wa wazazi kwa watoto wao katika masuala mazima ya kulinda na kudumisha mila na desturi zetu za hapa nchini. Unyanyaswaji wa watoto wa kike katika shule zetu ni tatizo ambalo limeanza kujitokeza. Naiomba Wizara kuangalia upya unyanyasaji huu ambao hufanywa na walimu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kwa kusema kwamba, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wamepewa jukumu zito ambalo kukabiliana nalo ni vigumu kutokana na kutengewa Bajeti isiyokidhi mahitaji. Nawapa pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali kupitia Wizara ya Afya ihakikishe inasimamia ipasavyo suala la uzazi wa mpango, kwani hata hizo nyenzo kama kondomu

hazipatikani katika maeneo yote ya nchi; hivyo, wanawake na wanaume walio wengi wanakosa hiyo huduma ya uzazi wa mpango.

Kukosekana kwa huduma hii kunachangia ongezeko la watoto wa mitaani, kwani watu kuingia kwenye starehe bila kinga yoyote hapo hupatikana maambukizo ya UKIMWI na hatimaye wazazi kufariki na kuacha yatima wasio na huduma na matokeo ni kupata watoto wa mitaani. Bahati mbaya sana ni kwamba, upendo umeondoka hakuna tena ndugu anayeweza kulea yatima wa ndugu yake. Familia zijajiishwe kurejesha upendo kama zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubakaji na udhalilishaji wa watoto ni jambo ambalo linazidi kila siku, hii ni kwa sababu kesi za ubakaji hazishughulikiwi ipasavyo. Kwa nini mara linapotokea suala la ubakaji na kuthibitika kwa vipimo mhusika asichukuliwe hatua za kisheria haraka sana; ni ushahidi gani unaongojwa wakati mbakaji na aliyebaka tayari yupo? Kesi hizi zinadharauliwa na ndiyo maana vitendeo hivi vinaendelea kushamiri siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa mitaani; kila mtoto ana mzazi wake, Serikali iandae mipango madhubuti kukomesha mambo haya ili kila mzazi atekeleze wajibu wake na ikiwa mzazi hataki kulea, basi ajizuie asizae. Serikali isijibebeshe mzigo wa kulea watoto wa mtu ambao mwisho wa siku jua likitua wanarudi kwa wazazi wao. Hata hapa nje ya Bunge wapigwe marufuku wale akina mama wanaojipanga pale kusubiri kuomba, tunajenga Taifa lenye ombaomba.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara hii, iendelee kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF)* kuwawezesha wanawake wa vijijini hususan katika mikoa mipya kama Katavi. Zoezi hili linaweza kufanyika kupitia Benki ya Posta ambazo zipo karibu nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Katavi, ninapenda kuomba mashine angalau tatu za *Hand Looms,* tupewe katika Chuo cha Msaginya ambacho kimekwisha karabatiwa kwa kiasi kikubwa. Chuo hicho kikipata mashine hizo, zitaweza kuwasaidia akina mama kujiunga katika vikundi na kutengeneza nguo na hivyo kuweza kujiongezea kipato na kukuza uchumi. Pamoja na hilo, Wizara ifikirie pia kuanzisha somo la upishi katika vyuo hivyo, yaani somo la *Domestic Science* ni vyema likafundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana katika maendeleo na Ustawi wa Jamii, lakini ajabu ni kwamba, imekuwa ikitengewa pesa kidogo sana ukilinganisha na majukumu mengi iliyonayo. Kutokana na pesa ya kutosha Wizara hii imekuwa kama haipo; je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuipatia pesa za kutosha ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu; kwa kuzingatia changamoto zilizopo na pia Taifa lolote ili liendelee ni vyema likatoa kipaumbele katika maendeleo na Ustawi wa Jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi ya kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunilinda hadi siku hii ya leo nikiwa mzima. Pia napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na jopo zima linalosaidia Wizara kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu, nilielewa ya kuwa maendeleo ni kusonga mbele kutoka kwenye hali duni kwenda maisha bora. Kwa bahati mbaya, baadhi yetu tunafikiri maendeleo ni kupata mambo au tamaduni za kigeni na kuziiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na utamaduni katika mavazi, watoto wetu hasa wa kike, kwa upande wa mavazi hali ni mbaya sana. Mavazi yavaliwayo ni mabaya

mno. Nguo fupi, suruali za kubana na nyepesi za kuonesha viungo vya mwili. Ukienda kwenye miziki ni balaa.

Yote haya wazazi wao wanawaona ila hawana sauti, kwani baadhi ya hao vijana majibu hayawi mazuri. Vijana wa kiume nao wavaaa suruali za "Kata K" na kunyoa mitindo ya ajabu na wengine marasta. Naiomba Wizara hii na Serikali kwa pamoja, ione haja ya kukomesha mavazi haya ya kudhalilisha hasa kwa wanawake, maana wakati mwingine hupelekea ajali ya kubakwa kwa wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kubwa sana na muhimu sana. Mara nyingi wanawake tunajidharau wenyewe. Wakati wa chaguzi, wanawake kwa vile ndiyo tulio wengi, badala ya kumpigia kura mwenzetu tunawapigia wanaume. Hii inapelekea wanaume kutudharau na kutuona hatustahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu itolewe kwa wanawake ili wajue nafasi yao katika nchi hii, majukumu, wajibu wao na kadhalika. Mambo ya mirathi mara nyingi katika maeneo mengi inapotokea waume kufariki dunia wanawake huwa wanasumbuliwa sana na familia za marehemu. Naiomba Serikali isimamie haki itendeke kuhakikisha wanapata stahili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. SALUM KHALFANI BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto wa mitaani ni kubwa sana, pamoja na jitihada mbalimbali za kupunguza tatizo hili, ndiyo kwanza linaongezeka na kukua kwa kasi kadiri miji inavyokua. Ili kushughulikia tatizo hili kwa ufanisi, mambo haya lazima yazingatiwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujua chanzo cha tatizo ambapo tafiti zinaonesha Miji Mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya ndiyo inayoathirika zaidi kwa kupokea watoto wengi na miji inayoongoza kwa watoto

kuhamia miji mikubwa ni Dodoma na Lindi. Serikali inatafuta suluhisho gani kwa kutafuta undani wake, sababu zinazowasukuma watoke na vivutio vya kule waendako badala ya kuwa na majibu mepesi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha kuwa watoto wa mitaani wako wa aina tofauti; wapo wa kudumu; wapo wa muda; na wapo wa msimu. Ni vyema basi wakati wa kutafuta suluhisho la tatizo hili ili kutambua makundi haya kushughulikia kila tatizo kwa usahihi badala ya kujumuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tafsiri mbalimbali za majina, wengine huwaita watoto wa mitaani, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wengine ombaomba, wengine wahuni, machokoraa; ni vyema Watunga Sera, Wanasiasa, Serikali na Watu wa Mipango, kuketi kitako na kutafuta mwafaka wa jina sahihi. Hii itasaidia kuleta uelewa wa pamoja katika kushughulikia hili tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo wa jambo la msingi katika maisha ya binadamu ambapo mtazamo chanya huleta maendeleo na kinyume chake ni sahihi. Tatizo kunaonekana kuna mtazamo hasi wa wadau hasa Serikali na watoto hawa na hivyo kushindwa kupata uelewa wa ndani wa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo hasi ni kutokana na Serikali kuamini kuwa hawa watoto wahuni, washari au wagomvi, walevi, wavuta bangi na kadhalika. Bila Serikali kubadili mtazamo juu yao, ufanisi hautapatikana kamwe.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuienzi Wizara hii na nawapa pongezi Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote.

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri; kama vile ambavyo hakuna mtu anaondoka nyumbani kwenda safari bila kujua watoto watakula nini, vivyo hivyo Serikali iweke mkazo kwa watoto kabla ya kufikiria Wizara zingine ili tuwape nafasi ya kuja kupata Taifa la baadaye.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Miji mikubwa kama Dar es Salaam kuna akina dada au watoto wa kike wanakaa barabarani wakiwa nusu uchi na kusimamisha magari kwa lengo la kutaka kufanya ngono. Jambo hili linakera, linadhalilisha, linaudhi na kwa kweli sio la kistaarabu na la kiutamaduni wa Tanzania. Naomba maelezo juu ya jambo hili mna mpango gani ili kuondokana na kero hii kwa Watanzania.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili ya jamii mitaani wa jinsia zote, wanakunywa pombe tangu asubuhi hadi usiku wa manane, je, kwa nini hatusikii Wizara ikitoa tamko kudhibiti uanzishaji wa baa/vioski vya vinywaji katika maeneo ya makazi na watoto wetu ku-*adapt* tabia mbaya. Je, ni lini Serikali itakomesha tabia hii?

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kujua kwa nini Serikali haipeleki fedha kwenye Halmashauri kama ilivyo katika Sekta ya Afya, *Basket Fund*, Kilimo – TASAF. Kwa nini maendeleo ya Jamii hayana Mfuko maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo Halmashauri hazina fedha na hazikusanyi mapato ya kutosha, vijana na wanawake hawapati fedha za kutosha za kukopeshwa kwa ajili ya ujasiriamali, Serikali ina mpango gani na changamoto hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa la *training* ya Maafisa Maendeleo ya Jamii, ni muda mrefu Maafisa Maendeleo ya Jamii wamekuwa hawapati *training* za mara kwa mara.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Simba; Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Ummy

Mwalimu; Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye mikakati mizuri sana ya kuendeleza jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; ni jambo la ajabu sana Serikali kuipuuza Wizara hii wakati ndiyo Wizara inayoshughulikia Maendeleo ya Jamii ya Watanzania. Zamani Bibi Maendeleo na Bwana Maendeleo walikuwa na thamani kubwa ndiyo hasa waliokuwa wanapita majumbani kuhimiza maendeleo vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wizara haipewi fedha za kutosha, ndio sababu watumishi hawana vitendea kazi mfano, pikipiki ili kuwafikia wananchi waliko. Naomba maelezo yenye kutia moyo kwa Watanzania ambao sasa hivi hawapati huduma ya wataalam ni jinsi gani wataondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Mirathi na Ndoa kurekebishwa; ndani ya Bunge tumeimba sana Sheria ambazo zimepitwa na wakati kuletwa Muswada hapa Bungeni ili kujadiliwa na kufanyiwa marekebisho, nakumbuka tangu nilipoingia Bungeni mwaka 2001 – 2005, tuliomba Serikali kuleta Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Mirathi na Sheria ya Ndoa lakini hadi sasa hakuna Muswada ulioletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kuna kigugumizi gani au ndiyo wanawake kuendelea kugandamizwa ili tuzidi kuwa wanyonge. Ama na sisi tuandamane kama wanavyofanya Chama cha CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka majibu ya Mheshimiwa Waziri, kabla hajaanza kufanya majumuisho akutane na Waziri Mkuu waeleze Serikali itakusaidiaje ili mikakati yako ifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake; ni ukweli usiofichika kuwa fedha za kiasi cha asilimia kumi kwa ajili ya wanawake

zinazopelekwa Halmashauri na asilimia tano kwa ajili ya Mfuko wa Vijana kwenda Halmashauri hazitoshi kabisa, ni lini Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake utaanza ili kukomboa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Watoto wa Mazingira Magumu, Kititimo kitachukuliwa na Serikali; napenda kukumbusha kuwa Kituo cha Kititimo hakina mlezi sasa hivi, je, ni lini Serikali itakichukua ili wapate huduma inayostahili kama watoto wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Singida *(FDC)* kupatiwa gari; chuo hiki ni kikubwa na kinatoa huduma bora sana kwa ubunifu wao wenyewe, naomba kipongezwe. Lakini kinapata fedha ndogo sana na gari limekufa. Lini Serikali itawapa gari ili kuwarahisisishia kazi zao ambazo zinatakiwa kuigwa. Nasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono mia kwa mia nikitazamia mambo yote niliyoyasema yatajibiwa na vile vile kuongezwa fedha.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhalilishaji wa wanawake na watoto; pamoja na jitihada ya Serikali lakini bado wanawake wengi wanadhalilishwa na watoto na hii hutokana na wanaume kutokuwa na huruma na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kufunga ndoa hawa kwa hiyari yao, lakini baada kutokea hitilifu ndogo tu huyo mwanamke anaachika na mwanaume huamua kumtoroka huyu mwanamke ambaye tayari amezaa naye watoto pengine zaidi ya wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali imsimamie huyu mwanamke ili aweze kupata haki yake na bila kupata usumbufu mkubwa. Kuna wanawake wengi tu wameleta malalamiko yao kwenye Wizara ya Wanawake na Watoto, lakini hadi leo hawajapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe adhabu kubwa kwa wanaume hao ili iwe fundisho kubwa kwa wengine kufanya udhalilishaji wa watoto na mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto wa mitaani watoto wengi wako mitaani wanaomba hasa kwenye Jiji la Dar es Salaam. Kuna watu wengine badala ya kuwasaidia hawa watoto, wanawaadhibu huwa wanawafanyia mambo machafu. Wengine pia huwa wanawaingilia kinyume cha maumbile, badala kujenga Taifa lililo imara, lakini tunajenga Taifa ambalo halina mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilishughulikie tatizo hili ili liweze kupungua.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwahamasisha vijana na akinamama katika Benki ya Maendeleo ya Wanawake. Ni kweli Benki hiyo imefunguliwa hapa nchini kwetu Tanzania, lakini bado uelewa wa makundi hayo haupo, yaani hawana taarifa, au hawaarifiwi na watendaji na kadhalika. Hivyo ili lengo la Serikali liweze kutekelezeka ni vyema Wizara hii iweke mpango mkakati wa makusudi ili kutoa elimu kwa wanawake wote wa Tanzania mpaka vijijini ili kupata fursa ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watoto ombaomba mitaani, hasa hasa Jijini Dar es Salaam, imekuwa ni jambo la kawaida kuwaona watoto wakiranda mitaani kwa kuombaomba, kwa kufanya kazi hatarishi katika mageto na biashara haramu. Aidha, naamini Serikali inaliona na inalijua suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naitaka Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuandaa utaratibu mzuri wa kuwaondoa, au kuondoa kadhia hii ili kuliondoshea aibu Taifa letu, naamini uwezo tunao, ikiwa tutaweka uzalendo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uzazi/kuzaa watoto na kuwatelekeza, kusema kweli hili ni janga kubwa na likiachiwa linaweza kutuharibia sifa ya nchi yetu, yaani mzazi anapata mimba na mimba hiyo ina baba yake, la kushangaza mtoto akizaliwa huwa anatelekezwa mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naitaka Serikali kuweka sheria kali dhidi ya vitendo hivyo vya wazazi, kwani wote ni wahusika, sheria hiyo iwe kila mzazi anayetupa au kutelekeza mtoto afungwe jela na apigwe faini kubwa na sheria ianze kutoka Vijijini, Kata, Jimbo, Wilaya, Mikoa na kadhalika.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ile dhana ya haki za kibinadamu, lakini tuna jambo ambalo lazima katika nchi yetu tulipe nafasi stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania wala siamini kwamba na maeneo mengine duniani ndio wanafanya hivi kwamba mwanamke ni kila jambo anafanywa yeye ndio jaa la kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania wanawake tumewaachia kazi za kilimo, ulezi wa watoto na jamii kwa jumla, ufugaji, kuwatumia katika shughuli za kujipatia fedha katika mahoteli makubwa kwa kuonesha shoo za kukaa uchi, wanatumiwa katika maeneo maalum ya kuonesha wanawake wako vipi maumbile yao, wanawake ndio ambao wanavaa mavazi nusu uchi tena hadharani na huku wakifurahia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwelimisha mwanamke umeielimisha jamii, lakini pia akipotoka mwanamke pia imepotoka jamii yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania kwa hali ilivyo sasa, Watanzania tunaelekea kubaya na jamii au kizazi kijacho katika miaka ya huko mbeleni tutakuwa na Taifa lisilo na mwelekeo wa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ije na mkakati maalum wa kudhibiti hali hii na naomba katika jambo hili tuanze na jambo la mavazi. Mavazi yawe ya heshima na tutangaze adhabu kwa watakaovaa vazi la nusu uchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Zanzibar miaka ya nyuma wakati wa Mzee Karume, tulipiga marufuku kuvaa nguo za juu nibanie chini nibwagie (Mabuga) na viatu vya raizoni na hili liliwezekana. Hivyo basi, Serikali ikiamua hakuna litakaloshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na dharau kubwa inayofanywa na Serikali hii kutopeleka fedha zilizopitishwa na Bunge hili Tukufu kwa ajili ya matumizi ya Wizara hii ambayo inaweza kumkomboa mwanamke mnyonge wa Kitanzania na watoto katika vitendo vya kikatili, unyanyasaji wa kijinsia na kuongeza kipato kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF)*; kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu juu wa watumishi wa Halmashauri hususan Wakurugenzi kutochangia fedha asilimia tano katika Mfuko wa Wanawake na Vijana. Hivyo kusababisha Halmashauri nyingi kukosa fedha katika Mfuko wa Wanawake. Je, Wizara ina mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha kuwa Halmashauri zinachangia hii asilimia tano ya mapato yao kwenye Mfuko wa *WDF*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 23 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imefanikiwa kutoa takribani 48,000,000 kwa Halmashauri sita tu nchi nzima. Je, azma ya

Serikali kutaka kumkomboa mwanamke mnyonge wa Kitanzania kwa kumpatia mtaji kwa mkopo wa riba nafuu itafikiwa au imefanikiwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na umahiri wa kuanzisha Mifuko mingi ya uwezeshaji, lakini ufanisi hakuna. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonesha kuwa tangu mwaka 2005/2006 hadi 2013/2014 Serikali haijaweka pesa katika Mfuko huu. Je, Serikali ina dhamira ya kweli kutaka kumkomboa mwanamke wa kKtanzania hususan wa kijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu; kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira magumu/hatarishi. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka/makusudi kuhakikisha kuwa tatizo hili linapungua kwa sababu asilimia kubwa ya watoto hawa wana familia zao? Je, Serikali lini itatoa fedha za kutosha ili hawa watoto warudi kwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hakuna mtoto wa mitaani kwani kila mtoto ana familia yake ama ukoo wake. Je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu kwa Watanzania wajue wajibu wao kwa familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa mitaani imekuwa ni suala gumu ambalo imefikia kwa Mji wa Dar es Salaam tu imefikia elfu 5,800 hali hii mbaya na hatutarajii kuwa watoto hawa walioko mitaani kuwa watakuwa raia wema, bila shaka watakuwa majambazi, vibaka, maambukizi na vizalia vya UKIMWI na madawa ya kulevya, baada ya miaka ya mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali iandae kwa makusudi mikakati na mipango madhubuti ambayo itatengewa bajeti ya kutosha ya kukabiliana na wimbi hili la watoto wa mitaani.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi Tanzania kuna wimbi kubwa la watoto wa mitaani, moja ya sababu kubwa ni udhaifu wa sheria inayopelekea tumeishia kusema ni utamaduni wetu. Ninachomaanisha hapa ni kuwabana wanaume wanaowazalisha wanawake kisha kuwatelekeza wote mama na mtoto bila kujali watakavyoishi au maisha ya mama yatakuwaje na atamlea vipi huyo mtoto. Kwa nini tusiwe na sheria kali ili baba mtoto ashiriki kikamilifu katika kumlea, kumtunza na kumsomesha mtoto wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia imeendelea sana, kumtambua baba mtoto si kazi ngumu, hata kipimo cha *DNA* kinaweza kutumika, lakini ni lazima Wizara ijipange sasa kuwa na Timu kwa kushirikiana na Polisi kufuatilia mpaka kwenye maeneo wanayoishi watoto hao na kujiridhisha kwamba, wazazi ambao wamegundulika kuwa na matatizo ya kindoa au baba ambaye amejulikana kumkana mtoto na kubanwa kisheria wanawafuatilia na kuhakikisha wanawalea watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatari kwa Taifa ambapo watoto wa mitaani hawawajui mababa zao. Sheria kali iundwe ili kila baba awajibike kumtunza mtoto wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza hotuba hii ambayo imesheheni mipango mizuri sana, basi naomba Wizara iongezewe pesa ili kufikia malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kidogo baadhi ya mambo kama:-

(1) Wizara kwa nini imeachia vijana wadogo wadogo kuwa ombaomba mijini?

(2) Kwa nini Serikali isichukue hatua kali kwa wazazi ambao wanatesa watoto na kuwafukuza nyumbani, matokeo yake watoto wanakwenda ovyo?

(3) Akinamama wengine wanadhalilishwa kwa sababu zao za kuvaa nguo fupi sana na zenye kubana. Naiomba Wizara itoe pia adhabu kwa wote wahusika yaani aliyebakwa na mbakaji.

(4) Pia naiomba Serikali iongeze adhabu kwa wabakaji na walawiti ili kukomesha uovu huo ambao umekithiri kufikia baadhi ya wanaume kubaka hadi kuku na wanyama na watoto wachanga hivi Serikali haioni?

(5) Pia naishauri Serikali ichukue hatua za haraka kuwarudisha watoto wa mtaani kwa wazazi wao ili kuishi na wazazi wao na kupata elimu na kuepusha wimbi la majambazi na makahaba kwa wingi hapo baadaye.

(6) Mwisho, hivi Serikali haioni aibu kwa kuachia watoto kuzagaa mitaani na kuombaomba kila kona ya nchi? Je, wageni wetu wanapeleka sifa gani kwenye nchi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Wizara kwa hotuba nzuri inayoeleweka kwa umma. Mchango wangu utahusu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili dhidi ya watoto ambao sasa unatendeka na wazazi, walezi kwa wanawake na wanaume. Vitendo husika ni kama ubakaji, kupiga watoto mpaka wanapata ulemavu, kulawiti na kadhalika. Nashauri kasi ya kushughulikia masuala haya iongezwe kwa Wizara hii kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ya kijinsia katika maeneo ya kazi na katika Taasisi za elimu yaelekea kuvuta

kasi na kuathiri zaidi wanafunzi wa kike na wanawake. Rushwa hii huwa ni ile ya ngono ambayo matokeo yake ni udhalilishaji wa kisaikolojia, kutoa wataalam ambao hawatatoa tija katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawatatoa tija kwa sababu yawezekana watakapoajiriwa wakiwa hawana umahiri katika taaluma zao ambazo wamezipata kutokana na upendeleo utokanao na ngono kwa ahadi za kupewa alama nyingi katika masomo yao, au ahadi za kupewa ajira. Hii ni hatari sana kwa vile licha ya kukosa wataalam mahiri pia inaweza ikawa moja ya njia ya kueneza UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kurekebisha sheria zetu ambazo ni potofu au kandamizi sana. Sheria hizi ni kama Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi na kadhalika. Ni muda mrefu sana ushauri umetolewa wa kurekebisha sheria hizi, hivi kigugumizi kiko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania. Napongeza kazi nzuri inayofanywa na Watendaji wa Benki hii, lakini wakati umefika sasa Benki hii ifungue matawi angalau Kikanda kwanza ndipo baadaye ijitandaze katika Mikoa yote na Wilaya zake. Vinginevyo kwa sasa inatafsiriwa kuwa Benki hii inafaidisha wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia wizara hii ya Maendeleo ya jamii ambayo ni muhimu yenye majukumu mengi ikiwemo kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa mikakati, miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la unyanyasaji wa kijinsia; suala hili pamoja na Serikali kupitia

Wizara hii imejitahidi kutoa elimu kwa umma kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, bado wanawake wengi hasa vijijini wamekuwa wakinyanyaswa kwa vipigo kutoka kwa waume zao na kuwasababishia ulemavu, hasa pale mwanamke anapotaka kuhoji kuhusu kipato cha shughuli za kilimo wanapovuna mazao yao waliyolima kwa pamoja mume na mke na wakaamua kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mume huamua peke yake kupanga bajeti na wakati mwingine kupeleka katika nyumba ndogo huku mke aliyeshiriki kulima na kuvuna akiambulia patupu. Hivyo, anapohoji kujua matumizi ya pesa hupigwa na kuachiwa ulemavu.

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara hii yenye Mawaziri hodari waendelee kutoa elimu kwa umma ili waendelee kuelimika na hasa vijijini na kuzijua haki zao.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia Wizara ili ujumbe usambae kwa wanawake kuhusu masuala ya jinsia katika jamii. Siku ya Wanawake Duniani isiendeshwe kisiasa bali iwahusishe akinamama wote kama wanawake duniani kwani kuna baadhi ya viongozi wamekuwa wakitoa picha mbaya ya sikukuu hii muhimu ya tarehe 8, Machi ya kila mwaka na kuiweka katika muonekano wa chama kimoja cha siasa.

Hivyo kusababisha wanawake wengi kuzira sherehe yao na kusababisha isherehekewe na watoto wa Shule za Msingi zaidi huku wahusika ambao ni wanawake kutosherehekea siku yao na kukosa ujumbe wa muhimu kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akihitimisha anijibu ushauri huu kama ameupokea kwani Siku ya Wanawake Duniani ni sikukuu ya wanawake na siyo ya watoto wa shule kupata ujumbe wa mama zao. Viongozi wasiingize usiasa katika sherehe hii ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya Watoto. Mtoto ana haki ya kupata afya, kupata elimu na uhuru wa kuamua, lakini bado kuna sheria kandamizi hasa katika makabila, bado kuna makabila yanaendeleza sheria hizi. Mkoa wa Katavi Kabila la (Wabende) hasa vijijini bado kuna tabia ya kuwachumbisha watoto wa kike wa umri wa miaka tisa kwa mwanaume mzee wa miaka 50 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anasoma mtoto huyo anapofikia darasa la nne na umri wa miaka 12 au 13 huachishwa shule na kupelekwa kwa mumewe. Hii ni hatari na aibu mila kama hizi. Naiomba Wizara ipige marufuku uonevu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoelewa mtoto ana haki zote za kutunzwa na kulelewa. Ningeomba Wizara hii itembee vijijini kuona ni jinsi gani watoto wananyimwa haki yao ya kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watoto wengi ambao mama zao wamewazaa kutokana na wageni wa Mataifa mengine wanaokuja Tanzania kufanya kazi za mikataba kama vile utengenezaji wa barabara na uchimbaji wa madini. Wanaume hawa wageni wamekuwa wakiajiri wanawake wa Kitanzania barabarani kusomba zege au kuwapikia vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ujira mdogo, huwadanganya wanawake wa Kitanzania kuwaoa na ndipo mimba hutokea na kuzaa na wanawake wa Kitanzania na wanapomaliza mikataba yao, wanaume hao huondoka na kuwaacha watoto hawa wakiishi maisha yasiyo na heshima wakiwa na wajihi wa Kichina au Uingereza yaani weupe wasio na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akihitimisha anieleze watoto kama hawa waliozagaa vijijini na kukosa huduma kama afya, elimu na kutegemea misaada ya kupasiana mara kwa Mkuu wa Wilaya, mara nendeni kwa Mbunge, mara misaada ya kidini.

Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kuwatambua na kuwasaidia watoto hawa wanaoachwa na mababa wa kigeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nawasilisha.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri na wasaidizi wake wote kwa kuandaa randama ya makadirio ya mapato na matumizi mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika kutoa ushauri katika mambo machache niliyoyachagua kuyatilia mkazo:-

(1) Sekta ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto ni sekta mtambuko, ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa, Wizara hii wamekuwa hawatekelezi majukumu yao sawasawa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Naiomba Serikali iione Wizara hii kama Wizara nyingine na kuitengea na fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake tofauti na ilivyo sasa.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria zinazowakandamiza wanawake: Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi, Sheria ya Ardhi na Sheria za Kimila zinazomkandamiza mwanamke. Naomba nipate majawabu, je, ni lini sheria hizi zitaletwa hapa Bungeni ili ziweze kufanyiwa marekebisho na Bunge.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, mmomonyoko wa maadili katika jamii ya Kitanzania umeendelea kuongezeka siku hadi siku na sasa tunashuhudia wanasiasa wanawafundisha vijana kutukana ovyo, kuzomea, kupiga mayowe, kutokuwa na heshima na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba na ndoa za utotoni, kuuza dawa ya kulevya, Naishauri Serikali iongeze kasi kuhakikisha inadhibiti vitendo hivi na vile vile wazazi hasa

wanawake kutekeleza wajibu wetu kikamilifu kwa kutenga muda wa kukaa na watoto wetu, vijana wetu, waume zetu na jamii kwa ujumla kuwafundisha maadili yaliyo mema.

(4) Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto, vijana na wanawake wa mitaani limezidi kushamiri katika miji mikubwa katika nchi yetu na mkakati gani walionao kwa kudhibiti vitendo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kuwakumbusha akinamama wenzangu kutekeleza wajibu wetu kikamilifu kuwafundisha maadili watoto wetu na familia zetu ili kuwa na Taifa la watu wasiovuta madawa ya kulevya, wasiojiingiza katika biashara ya madawa ya kulevya na mimba za utotoni.

(5) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na ukombozi wa wanawake kupitia vikundi vya kiuchumi katika miaka ya karibuni, Mfuko huu umekuwa haupati fedha ambazo matumizi yake yameelekezwa katika Benki ya Wanawake badala ya kwenye Halmashauri zetu ili kusaidia juhudi za wanawake katika kujiondolea umaskini.

Naishauri Serikali iendelee kutenga fedha kwa shughuli za vikundi vya wanawake badala ya ilivyo sasa fedha zote zinapelekwa Benki ya Wanawake ambayo iko Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

(6) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake: Nawapongeza watendaji wa Benki ya Wanawake chini ya Mtendaji wake Mama Margreth Chacha kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kuhakikisha Benki ya Wanawake inakuwa siku hadi siku na kuweza kufungua matawi Dodoma na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, naiomba Serikali iendelee kuongeza fedha kwa ajili ya Benki hii, tena fedha hizi zenyewe zisiwe za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kiongezeke kifungu kingine ambacho

kitakuwa na fedha ili kufungua matawi yake Kanda zote Nyanda za Juu Kusini, Mbeya, Kanda ya Kusini, Lindi; Kanda ya Kaskazini, Arusha. Vile vile ningependa kupata majibu ni jinsi gani Benki ya Wanawake imejipanga kukopesha vikundi vya wanawake vilivyoko mikoa ambayo benki haijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita mtoa hoja ili aweze kuhitimisha hoja yake. Tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 20!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yao imetupa moyo, ari na hamasa ya kufanya vizuri katika kuhakikisha tunajenga jamii ya Watanzania inayojali usawa, haki na maendeleo ya wanawake na wanaume wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nitamke rasmi kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuchangia hoja hii kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo makuu manne. Eneo la kwanza ni suala la Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, nitachangia kuhusu sheria kandamizi dhidi ya wanawake na eneo la tatu nitazungumzia ukatili dhidi ya wanawake na kama muda utatosha nitazungumzia suala zima la usawa wa jinsia na mkakati wa kuhakikisha tunafikia hamsini kwa hamsini katika nafasi zote za kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Michango yote kwa kweli iliyotolewa na Wabunge leo ilikuwa na lengo la kuboresha na kujenga Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi na niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Serikali inatambua umuhimu na mchango mkubwa wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika maendeleo ya jamii hasa maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika Ilani ya Uchaguzi, aya ya 78 inaitaka Serikali kukiimarisha na kupanua mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili vipokee vijana wengi zaidi na kuwapatia mafunzo ya maarifa ya kisasa katika fani za kilimo, biashara, ufundi stadi na ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 inatekelezwa kivitendo na kitu cha kwanza cha kuthibitisha *commitment* ya Serikali katika kuboresha Vyuo vyetu ni Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2011/2012 - 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza mpango unatambua rasmi umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika eneo zima la *human capital development* katika kukuza rasilimali watu. Kwa hiyo, huo ndiyo ushahidi wetu wa kwanza, lakini mwingine anaweza akasema mmeuweka tu kwenye mpango wa Mheshimiwa Wasira, tuonesheni dhamira ya dhati ya Serikali iko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka bajeti yetu leo na randama zetu, katika bajeti ambayo mtaipitisha leo 43% ya bajeti ya matumizi mengineyo, imekwenda katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Pia katika fedha za maendeleo zilizotengwa bilioni mbili kati ya bilioni nne za fedha za ndani, 50% ya fedha za ndani za maendeleo zimetengwa kwa ajili ya kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya si maneno tu ya kwenye makaratasi. Pia tunawashukuru wenzetu wadau wa maendeleo wametupatia bilioni 4.4 kwa mwaka huu wa fedha kutoka *Global Partneship For Education* kwa ajili ya kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, natambua changamoto zote zilizokuwepo katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu ya umuhimu mkubwa wa vyuo hivi katika kutoa *skills,* katika kutoa utaalam, fani na elimu ya ujasiriamali na elimu ya ufundi tumedhamiria kuviboresha. Ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha tumeanza awamu ya kwanza ya maboresho ya vyuo vyetu katika vyuo 25. Anayetaka kutambua atasoma iko katika kiambatanisho cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, pia tunaomba Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono kwa sababu Vyuo hivi vinatakiwa kukidhi mahitaji ya jamii husika na ndiyo maana tumemfanya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Vyuo vya *FDC* awe ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya au Mkurugenzi wa Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pale ambapo Halmashauri au Wilaya inataka kuhakikisha vijana wao wanaomaliza darasa la saba, wanaomaliza *form four* na hawana shughuli zozote za kufanya, Halmashauri inaweza ikaingiza mpango maalum wa kuhakikisha kwamba Vijana hawa wanapata mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dokta Titus Kamani ametueleza wenzetu Wachina walivyofanikiwa na Vyuo vya aina kama hii, lakini pia Mheshimiwa Zaituni Buyogera ametuonesha jinsi gani vijana wa Kasulu walivyonufaika na kupata ujuzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize moja katika eneo hili ambalo pia limeulizwa, je, Halmashauri au Wilaya zinawezaje kuanzisha Vyuo vya Maendeleo ya Wanachi.

Niwape mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, wao walitupa majengo baada ya kwamba tumekifanya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Monduli kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo wakaamua sasa kutupa majengo pale Mto wa Mbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanza kutoa mafunzo ya ufundi stadi, mafunzo ya maarifa, mafunzo ya kujua mambo mbalimbali ya kimaisha kwa vijana wao. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ni changamoto tunaiweka kwenu kuhakikisha kwamba, mnaanzisha vyuo hivi kadiri matarajio yenu yanavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika hoja ya pili ambayo ilihusu suala la Sheria kandamizi. Tunakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge juu ya umuhimu wa kufanyia marekebisho sheria zote kandamizi dhidi ya wanawake. Kama tutakataa, wanawake wa Tanzania walikiamini Chama cha Mapinduzi kukipa kura kwa kuamini kitaweza kusimamia haki, ustawi na maendeleo yao. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, aya ya 187 (f), inatuelekeza kuzifanyia marekebisho Sheria za mirathi na Sheria zote zinazoonekana kuwakandamiza wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii haiwezi kusita kwa sababu hili tumeliombea kura kwa wanawake wa Tanzania na tutakaporudi 2015 watatuuliza. Naomba niwathibitishie wanawake wote wa Tanzania na wasichana kwamba, Serikali itafanyia marekebisho sheria zote kandamizi dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato ulishaanza, tatizo lililojitokeza, kwa mfano, Sheria ya Ndoa kipengele kinacholalamikiwa kwa kiasi kikubwa ni kile kinachoruhusu mtoto wa kike wa chini ya umri wa miaka 18 kufunga ndoa. Kinasema miaka 15 mtoto wa kike kwa mtoto wa kiume ni miaka 18, lakini Sheria katika kifungu 13(2) cha Sheria ya Ndoa

Namba tano (5) cha mwaka 1971, kinaruhusu wasichana waliofikia umri wa miaka 14 kuolewa kwa kibali cha Mahakama kutokana na sababu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Sheria ya Ndoa yote siyo mbaya, kuna mambo mazuri, kwa mfano, inakataza vipigo kwa wanandoa Kifungu cha 66, lakini pia inatoa fursa kwa mjane kurithi mali za mumewe, inatoa fursa kwa watu kugawanya mali pale ambapo kutakuwa na talaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu sheria hizi za ndoa zinagusa imani za watu mbalimbali, dini na tamaduni za watu mbalimbali, ni lazima tukusanye mawazo ya wadau wote kuhakikisha kwamba tunapotengeneza Sheria haitaleta misuguano katika jamii. Kwa hiyo, mchakato ulianza, Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tulishapeleka mapendekezo kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba, Sheria hizi zinafanyiwa marekebisho na *white paper* ulishakuwa umeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na Waheshimiwa Wabunge, naomba mnielewe tulisimamisha huu mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria kandamizi kwa sababu nchi yetu sasa hivi ipo katika mchakato mkubwa sana wa kutengeneza Katiba Mpya. Kwa hiyo, tunapokwenda kwa wananchi unamuuliza Katiba mpya, *at the same time* unamuuliza kuhusu Sheria ya Ndoa, unamuuliza kuhusu Sheria za Mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria za Mirathi kinacholalamikiwa ni Sheria za Mirathi za kimila ambapo tuna Sheria ya Hali za Watu inayoruhusu kutumika kwa Sheria za Kimila na Sheria za Kiislam katika Mashauri ya madai. Kwa hiyo, kuna kitu kinaitwa *Judicature and Application of Laws Act* ya mwaka 1963.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mirathi ya Kiislam, huwezi kuibadilisha. Sheria ya Mirathi ya Kimila ndiyo inapigiwa kelele kwa sababu inaweka madaraja matatu;

urithi daraja la kwanza, mtoto wa kiume mkubwa, daraja la pili watoto wa kiume wanaofuatia, watoto wa kike wanawekwa daraja la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunakubali Sheria hizi ni kandamizi, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge tutakapokuja kuijadili Katiba mpya ni lazima tuhakikishe Katiba mpya inaweka msingi mzuri zaidi wa kulinda haki za wanawake. Tayari Katiba si mbaya hivyo, lakini ni lazima tuhakikishe kwa mfano, Katiba ya Uganda imekwenda mbali na kusema Sheria zote kandamizi dhidi ya wanawake na watoto ni *null and void,* ni batili hazitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini Mheshimiwa Warioba anatusikia na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tutakaa katika Bunge la Katiba na Waheshimiwa Wabunge tukawahamasishe wanawake wengine na wanaume wahakikishe kwamba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunayoitengeneza au tunayotaka kuianzisha inaweka msingi imara wa kulinda haki, ustawi, utu wa mwanamke na watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika eneo la tatu ambalo ni suala la unyanyasaji wa kijinsia na hili limeongelewa na watu wengi, tena kwa hasira sana. Nimefurahi kwa sababu wanaonesha ni jinsi gani wanaudhika na vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa ukatili dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba, Tanzania ina kiwango kikubwa sana cha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake. Takwimu zetu wenyewe; Tanzania *Demographic and Households Survey* ya 2010, inaonesha karibu 39% ya wanawake wa Tanzania wenye umri wa miaka 15 mpaka 49 wameshafanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia (*physical violence)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunazungumza kwamba, katika kila wanawake 100 wanawake 39 wameshawahi kupata vipigo vya kila aina ya unyanyasaji, lakini tunapozungumzia *sexual violence,* ukatili wa kingono,

katika kila wanawake watano, mwanamke mmoja wa Tanzania ameshawahi kudhalilishwa kingono. Kwa hiyo, hatukubali kama Serikali na hatutakubali kuona vitendo hivi vinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali linakuja, tumefanya nini? Katika Bunge lako hili, mwaka 1998 lilipitisha Sheria ya Makosa ya Kujamiiana inaitwa *SOSPA* maarufu sana na sasa hivi imo ndani ya Sheria za Kanuni za Adhabu Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania. Adhabu zilizowekwa za ubakaji, kujaribu kumdhalilisha mwanamke kwa matusi, maneno ya hovyo ni adhabu kali kweli, lakini ni kwa nini bado vitendo hivi vinaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako Tukufu kusema kwamba, hatutamaliza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kutumia Sheria peke yake. Ni lazima tushirikiane na jamii, wanawake, wanaume kuhakikisha kwamba vitendo hivi vinatokomea. La kwanza, nalirudisha suala hili kwa wanawake wenyewe, *TDHS* yenyewe inasema wanawake wanaulizwa, je, ni sahihi mwanamke kupigwa na mume wake kwa sababu tu ameunguza chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya 20% ya wanawake wanasema ndiyo. Je, ni sahihi kwa mwanaume akupige kwa sababu eti umeondoka nyumbani bila kuaga, wanasema ndiyo. Kwa hiyo, narudisha mzigo kwa wanawake wote wa Tanzania, sisi ndiyo tuwe chachu ya kukataa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema pia kuwa vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia vinatokea ndani ya ndoa. Tuna takwimu za Kiserikali zinaonesha kwamba, kwa Tanzania bara 45% ya wanawake wanandoa wamepitia manyanyaso ya kijinsia toka kwa wenzi wao, lakini kwa Zanzibar ni 9%. Kwa hiyo, mnaona vitendo vingi vinatokea ndani ya ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema kwamba, Sheria ya Ndoa inakataza vipigo kwa wanandoa, hivi ni

mapenzi gani ya watu kupigana? Hamwezi kurekebishana, hamuwezi kukaa mkaongea kama kumetokea tofauti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa changamoto kwa wanawake wote kuhakikisha kwamba, wanaripoti vitendo vyote vya ukatili dhidi ya jinsia. Tumeanzisha Madawati ya Jinsia katika Vituo vya Polisi tuyatumie. Tatizo letu hatutaki kutoa taarifa kwa vyombo husika na navipongeza sana vyombo vya habari vya Tanzania, vimetusaidia sana sana katika kuibua matatizo ya ukatili dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hili suala siyo la wanawake peke yao, ukatili wa kijinsia na wanaume. Pale wanaume mnapopigwa msigugumie, nendeni mkatoe taarifa, badala ya kuugulia nyumbani, pale mnapopata vipigo kutoka kwa wenza wenu na nyie mkatoe taarifa yanaitwa Madawati ya Jinsia na Watoto hayaitwi madawati ya wanawake peke yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika tano, nimalize suala la mwisho ambalo nataka kuliongea, nalo ni suala la usawa wa jinsia na haki za wanawake, je, tuna mkakati gani wa kufikia hamsini kwa hamsini. Hili limeongelewa na Waheshimiwa wengi; Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Amina Makilagi na majina mengine hapa sina. Nikubali kwamba ni kweli wanawake Tanzania ni zaidi ya 51% na hii ni kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, wanaume ni 49%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapoona Watanzania 100 maana yake wanawake ni 51. Kwa hiyo, tunaamini kama Wizara, Tanzania haitapiga maendeleo ya kweli kama tutawaacha wanawake nyuma na hawatakuwa na fursa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize fursa sawa ya wanawake kushiriki katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Msingi mzuri umewekwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13 inatamka usawa wa binadamu wote mbele ya sheria na Ibara ya 13(5) ya Katiba inakataza ubaguzi wa aina yoyote ikiwemo ubaguzi wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumefanya kitu gani kuhakikisha tunafikia hamsini kwa hamsini. Tumeridhia mikataba na maazimio mbalimbali juu ya haki za wanawake. Baada ya kuridhia mikataba na maazimio mbalimbali juu ya haki za wanawake ndiyo maana tulifanya marekebisho ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 66 (b), imeweka nafasi maalum kwa ajili ya wanawake. Hivyo, ni mategemeo yetu kwamba, Katiba hii mpya tunayotengeneza itakwenda mbali zaidi zaidi na kuweka msingi mzuri wa kulinda haki na utu wa wanawake na watoto wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie mfano wa Katiba ya Kenya ambayo wameipitisha mwaka 2010. Katiba ya Kenya licha ya kwamba inatambua usawa wa wanawake na wanaume Ibara ya 27(3) ya Katiba ya Kenya inasema: *"Women and men have the right to equal treatment including the right to equal opportunities in political, economic, cultural and social spheres".* Imesema wote wana haki sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Katiba ya Kenya imekwenda mbali, inapozungumzia masuala ya *electoral system and process,* masuala ya uchaguzi inasema haitaruhusiwa kwa jinsia moja kuzidi mbili ya tatu ya jinsia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mategemeo yetu ni kwamba, katika Katiba ya Tanzania nayo kuna mambo

mazuri ya kuiga kutoka Katiba ya Kenya, kwamba, hatutaruhusu Katiba yetu watu wa jinsia moja watawale, unakuta kati ya watu 10 wanaume wako sita, haiwekezekani wanawake ni 51% ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna suala hili namalizia ambalo limejitokeza katika mchakato mzima wa mabadiliko ya Katiba kwamba, tumeji-*commit* kwenye *SADC Protocol,* kwenye *Africa Union Protocal on the Rights of Women* kwamba, lazima tutafikia hamsini kwa hamsini *by* 2015, tutafikiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema tufute Viti Maalum, Wizara haina tatizo na kufuta Viti Maalum, msimamo wetu, Katiba iweke msingi mzuri wa kuhakikisha wanawake wanashiriki katika nafasi za uongozi. Tunahitaji kuona wanawake Wenyeviti wa Vijiji 50%, tunahitaji kuona wanawake Madiwani 50%, tunahitaji kuona Wabunge wanawake 50%, sasa tunawapataje? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnafuta Viti Maalum, futeni, lakini nitoe tahadhari ya uchaguzi wa Kenya, uchaguzi wa Kenya Katiba imesema katika ile *National Assembly* kutakuwa na Wabunge 290 na ikasema kutakuwa na wanawake 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanawake waliogombea Majimbo ni wanawake 16 tu ndio wamepita, ina maana wasingekuwa na nafasi maalum za wanawake, Bunge la Kenya leo lingekuwa na wanaume 274 wanawake 16 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye useneta, Katiba ya Kenya imekwenda mbali, ikasema kutakuwa na maseneta *whatever*, wanawake na wanaume 47. Wanawake waliogombea useneta katika *counties* zile wote wameanguka. Bahati nzuri *Alhamdulillah* Katiba ya Kenya imekwenda mbali ikasema kutakuwa na Maseneta wanawake 16 watakaokuwa *nominated* na *political parties* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo msimamo wa Wizara. Tuna majukumu ya Kimataifa na Kikanda kuhakikisha kwamba tunafikia 50 kwa 50 katika nafasi zote za uongozi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake wajitokeze katika nafasi zote za kugombea Uwenyekiti wa Kijiji, Ujumbe wa Serikali ya Kijiji na Udiwani. Lakini Katiba ni lazima iweke msingi mzuri wa kuhakikisha kunakuwa na ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu masuala ya unyanyasaji hasa rushwa ya ngono katika ajira na Vyuo Vikuu. Bahati nzuri nilishafanya maongezi na *NGO* moja, kwamba hebu tuanzishe Waziri wa Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu kwa ajili ya kuhakikisha watoto wa kike walioko katika Vyuo wanapata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizozinduliwa juzi kuhusu hali ya UKIMWI na Malaria na Mheshimiwa Rais zinaonyesha wasichana miaka 23 mpaka 24 maambukizi ya UKIMWI ni asilimia 6.6, wakati wavulana ni asilimia 2.6. Kwa hiyo, ni changamoto. Ni lazima tuhakikishe tunadhibiti hali hiyo. Tuna Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sheria ya Kuzuia na Makosa ya Rushwa, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, zote zinakataza uzalilishaji ikiwemo rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda katika Vyuo Vikuu vyote kuhamasisha wasichana watambue utu wao na wawe tayari kutoa taarifa pale ambapo haki zao zinavunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo moja la Chuo cha Maendelo ya Jamii Rungemba kwamba Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa aliomba kiwe Chuo kinachotoa Shahada. Hilo limeshapita Mheshimiwa Mgimwa, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba sasa hivi kitatoa shahada ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Hiyo ndiyo inaitwa *Best Results Now! (Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge leo asubuhi Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o katika kuchangia alitoa hoja na baadhi ya Wabunge walimuunga mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o kwa uchungu wako, na natambua namna unavyopenda akina mama na wanawake. Akina mama wamekusikia kilio chako. Lakini kwa bahati mbaya utaratibu uliotumia hauko katika Kanuni za Bunge letu. Imekuwa ni *very* very *unfortunate*. Unaweza ukatumia utaratibu huo katika Kamati ya Matumizi. Lakini vilevile hicho kifungu kimekuwa *ring-fenced* kwamba huwezi kubadilisha maudhui ya kifungu hicho. Hivyo, bado hutaweza kufanikisha azma hiyo. Nakuomba utumie utaratibu mwingine. Kama unaweza ku-*lobby* na Kamati ya Mzee Chenge, unaweza ukazungumza nao na wakakusaidia.

Sasa namwita mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyowasilisha hapa Bungeni leo asubuhi, pia na wale kuwepo na kusikiliza. Nashukuru sana kwa michango mizuri iliyotolewa leo, michango ambayo karibu yote imekuwa inaonyesha *concern* kuhusu ufinyu wa bajeti wa Wizara yangu. Nawashukuru sana, naamini Serikali tumesikia na mambo mazuri yataendelea kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 45 wamechangia hoja yangu ambapo Waheshimiwa Wabunge 11 wamechangia kwa kauli na 34 wamechangia kwa maandishi na wengine pia walichangia kupitia hotuba ya Waziri Mkuu. Michango hiyo ipo ambayo inatoa ushauri mwingi na ina maswali mengi ambayo nitajaribu kujibu na mengine Mheshimiwa Naibu Waziri ameshajibu, nami nitajaribu kuyajibu yale yaliyobaki kama muda utaniruhusu na lakini tutatoa kitabu ambacho kitaonyesha majibu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetiwa Moyo sana kwa pongezi za Waheshimiwa Wabunge. Tunathamini michango yote iliyotolewa na tunaahidi kufanyia kazi. Napenda kuriarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara inathamini sana michango yenu. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa hotuba iliyotolewa na Kambi ya Upinzani. Hotuba ile imesheheni mambo mengi ambayo Wizara itayafanyia kazi. Ilikuwa ni hotuba ya kujenga na siyo ya kunung'unika. Kwa hiyo, mimi nasema ahsanteni sana. Kama tunavyojua masuala ya wanawake hayana pande yoyote; tuko pamoja *together we stand*. Kwa hiyo, ndiyo maana hata *speech* ya Upinzani imefanana sana na *speech* ya upande wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru na kuipongeza Kamati Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuisimamia Wizara yangu kwa umakini na umahiri mkubwa. Hiyo imedhihirishwa kwenye Hotuba yao iliyosomwa hapa Bungeni asubuhi. Kamati imezungumzia sana suala la ufinyu wa Bajeti ya Wizara, lakini imetambua na kupongeza jitihada za Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufinyu wa bajeti ni kweli ukilinganisha na majukumu ya Wizara, Bajeti tunayopewa ni ndogo. Wizara hii ina Vyuo 64, ambavyo 55 ni vya Maendelo ya Wananchi na tisa ni vya Maendelo ya

Jamii. Aidha, Wizara ina jumla ya Watumishi 1,121 ambao wanastahili huduma zote za kuitumishi kama Wizara nyingine na ukilinganisha, bajeti ya Wizara yetu ni ndogo kuliko Idara nyingine za Serikali. Kwa hiyo, ni kweli hicho mnachokisema. Majukumu yetu mengi ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii zidi ya mila potofu na kuhamasisha jamii kuhusu maendeleo yao.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi kuwa watumishi wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri wanashindwa kutekeleza majikumu yao, hususan kuhamasisha Jamii kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti na ukosefu wa vitendea kazi.

Waheshimiwa Wabunge, katika hili, naomba sana tushirikiane kwani Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wako kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, tunapopanga masuala ya bajeti katika Halmashauri, sisi kama Madiwani tukumbuke kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii wanastahili kupewa vitendea kazi ili waweze kuwafikia wananchi na kuwabadilisha mitazamo hasi ili wakubali maendelo kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na tatizo la ufinyu wa Bajeti, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliwasilisha Serikalini Mapendekezo ya kuimarisha Sekta ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 2007, mapendekezo hayo yalijumuisha gharama za utekelezaji wake. Pia Wizara ilijenga hoja ya kuingiza vyuo vinavyosimamiwa na Wizara katika vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa maendeleo wa miaka mitano, hilo limetendeka. Kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, Wizara imeandaa utaratibu wa pamoja utakaowawezesha wadau hao kuchangia bajeti ya Wizara, yaani *Gender Basket Fund.* Pamoja na jitihada zote hizo bado bajeti haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati, yaani kutenga fedha kwa Mfuko wa *WDF.* Pamoja

na kukubaliana na ushauri huo, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani wa Halmashauri zao, tuaomba na ninyi pia huko kwenye Halmashauri mhakikishe ile asilimia tano ya makusanyo yao ya Halmashauri yanaingizwa katika mfuko huu ili kuuimarisha. Jitihada zinaendelea kufanywa ili tuweze kupata fedha kama ilivyozungumzwa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Serikali limeanzishwa Kisheria katika Fungu 25 la Sheria ya Na. 24 mwaka 2012. Huko mbele nitajibu Maswali ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao walizungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tatizo kubwa lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusu watoto wa Mitaani. Ni kweli lipo tatizo kubwa zaidi, na tatizo hilo ni tatizo la ukatili zidi ya watoto ambalo nimelizungumzia na nimefafanua vizuri katika ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa wengi wamezungumza kuhusu UKIMWI; ni kweli UKIMWI bado ni janga la Taifa. Mara zote Takwimu zinaonyesha wanaoathirika zaidi ni wanawake na hivyo kuwepo uwezekano mkubwa wa kuambukiza watoto kipindi wanapozaliwa. Pamoja na jitihada zote zinazofanywa, lakini bado kuna watoto ambao wanaambukizwa. Aidha, UKIMWI unasababisha vifo vya wazazi na kuacha watoto yatima ambao hatima yake ni kuishi Mitaani. Wito wangu ni kuzingatia uadilifu katika ndoa na kuepuka ngono zembe. Tukifanya hivyo, tutaunga mkono kwa dhati kaulimbiu ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Tanzania bila UKIMWI inawezekana.

Mheshimiwa mwenyekiti, nakubalina na ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba Wizara iandae maandiko kwa lengo la kutafuta fedha. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tumeandaa utaratibu wa wadau kuchangia katika utekelezaji wa majukumu yetu; moja, kwa kupitia *basket fund,* lakini maandiko mengine zaidi tumeandika, tunasubiri kupata matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rushwa ya ngono mahali pa kazi, Wizara imepokea ushauri wa Kamati na itaangalia namna ya kutengeneza mfumo asili ambao utawawezesha waathirika kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi sana kuona Kambi ya Upinzani inatambua mchango wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii na nataka tu kuwakumbusha kwamba Ilani yetu imetuagiza hivyo na ndiyo maana mnaona hivyo. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa mchango mkubwa kama tulivyoagizwa na Ilani yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende moja kwa moja katika hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Nianze kuhusu ongezeko la watoto wa Mitaani na wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Kambi ya Upinzani wamezungumzia sana, pamoja na Waheshimiwa Zaynabu M. Vullu, Mheshimiwa Abuu H. Jumaa, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Mohmoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Hussein N. Amar, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mheshimiwa AnnaMaryStella J. Mallac na Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo wote hawa wamezungumzia hili. Hata hivyo, wengine waliozungumzia walikuwa wanauliza Serikali inafanya nini na watuhumiwa ambao wanawafanyia watoto ukatili wanachukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kujibu hili ambalo linahusu ongezeko. Hadi sasa jumla ya watoto waliotambuliwa kuishi katika mazingira hatarishi na wanaoishi na kufanya kazi Mitaani ni watoto wapatao 849,051, walitambuliwa. Wengi wao wakiwa peke yao na wengine hasa wale wenye umri mdogo wakiwa na wazazi wao. Kati yao wasichana ni 407,544, yaani asilimia 48 ya watoto ambao wako Mitaani, na wavulana 441,507; yaani asilimia 52 katika hiyo idadi ambayo tumeona wako barabarani. Watoto hawa wanapatiwa huduma za elimu, afya, chakula na masada

wa kishieria na kisaikolojia kupitia wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, *Save the Children, Family Health International, World Vision, UNICEF*, na *Plan International.*

Waheshimiwa Mwenyekiti, wapo watoto ambao tumeweza kuwachukua na wanasaidiwa kwa namna hii. Hata hivyo, kila siku wanazidi kuja mjini. Kwa hiyo, hilo ni tatizo kubwa zaidi ambalo sasa Wizara yangu ikishirikiana na Tawala za Mikoa, hasa Ma-*RAS* na Wakuu wa Mikoa tunashauriana ni jinsi gani ya kuwaondoa katika Miji mikubwa, kwa sababu wimbi sasa limekuwa kubwa sana kama mnavyoona wako Mitaani na wazazi wao. Ukweli ni kwamba wanachafua hata mazingira ya Mji kwa sababu wanalala pale wao na familia zao, wanakwenda choo, ambacho hatujui wanakwenda wapi. Kwa hiyo, Miji imefikia sehemu mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni naamini tutafanikiwa kupunguza lile tatizo ambalo linazagaa katika Miji mingi, kwa kuwaondoa na kuwapeleka katika maeneo yao, pamoja na kwamba uwezekano wa wao kurudi ni mkubwa zaidi. Lakini ni heri tukiwaondoa sasa hivi, kuliko kuwaacha wanaendea kuishi kama walivyo.

Kuhusu ukatili dhidi wa watoto, Serikali imefanya nini na watuhumiwa wamechukuliwa hatua gani? Swali hilli limeulizwa na Mheshimiwa Faith M. Mitambo, Mheshimiwa Juma Othman Ally, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Tauhida Cassian Nyimbo, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Msheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga na Mheshimiwa Margareth A. Mkanga.

Wizara yangu hivi sasa imeandaa mkakati wa mawasilino ambao utatumia njia mbalimbali za uelimshaji umma, ikiwemo vikikundi vya ngoma, maigizo, nyimbo, *radio*, runinga, mikutano ya hadhara na Semina, ili kuelisha umma wakiwemo wazazi na watoa huduma za watoto, kuwapa haki zao za misingi ili wasikimbiie Mitaani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *TASAF* na Mashirika mengine yasiyo ya Serikali,

inaandaa *programme*, ya kuziwezesha familia kuwa na Miradi ya uzalishaji, yaani zile familia masikini kuwa na Miradi ya uzalishaji itakayoweza kuwakimu mahihitaji yao. *Conditional Cash Transfer Programmme*, ambayo iko chini ya *TASAF*. Tunaamini hiyo nayo itasaidia.

Wizara itaendlea kushirikiana na TAMISEMI, na wadau wengine, kuyawezesha Mabaraza ya watoto ili yaweze kufanya kazi yake ya kuelimisha wenzao kupitia vilabu vya watoto na makundi rika, kuhusu athari za kuishi na kufanya na kufanya kazi Mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Wizara yangu, ikishirikiana na wadau wengine Tanzania, ikiwa ni nchi ya kwanza kwa Afrika kufanya utafiti huu, unaonyesha viwango vya juu vya ukatili vya aina mbalimbali ukiwemo ukatili ya ngono wanaofanyia watoto.

Tuna takwimu ambazo zinatisha. Katika tafiti hizo imegundulika kwamba watoto watatu kati ya wasichana kumi, hufanyiwa vitendo vibaya, na mtoto mmoja kati ya kila wavulana saba, wamewahi kuhujumiwa kingono kabla hawajafika miaka 18. Kati ya watoto ambao wamehujumiwa, karibu wanne kati ya kumi ni wasichana na watatu kati ya kumi wavulana, wamehujumiwa karibu mara tatu kingono kabla hawajafikia miaka 18. Takwimu hizi zinatisha sana. Vitendo vya ukatili mara nyingi huwa ni pacha kwa mtoto na anaweza kuwa anahujumiwa kingono, kupigwa, na hata kunyanyaswa. Wahanga wengi wa matukio ya ukatili hupatwa na matukio zaidi ya moja.

Tafiti pia ilibaini kwamba wengi wa waathirika wa vitendo vya ukatili vya kingono, huathirika pia na maambukizi wa Ukimwi na VVU. Kwa kiwango kikubwa ukatili pia hasa ule wa viboko na unyanyasaji hutokea mashuleni. Kuna watoto ambao wako barabarani, hawataki kusoma wamekimbia viboko mashuleni, wamekimbia viboko kwa wazazi wao. Kuna ukatili mmoja hapa Mheshimiwa mmoja amezungumzia kwa uchungu, ni kweli ukatili unawasukuma watoto, wanaondoka nyumbani wanakwenda barabarani.

Mama unapika chakula, mtoto unampa kichwa, baba unampa paja. Mtoto yule anaona afadhali aende barabarani, akaombe, akanunue *chips* naye apate sehemu nzuri. Mimi naamini Waheshimiwa Wabunge, mtoto yule anastahili kula vizuri zaidi kuliko baba, kwani baba ameshakula siku nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tunazo kesi ambazo hadi hivi sasa zipo Mahakamani zinaendelea huko Mbeya, Shinyanga na Dar es Salaam. Katika matukio hayo Wizara imekuwa ikishirikiana na Jeshi la Polisi na Mahakama kuhakikisha haki inatendeka kwa waathirika. Aidha, Wizara imeandaa mpango kazi wa miaka mitatu wa kuzuia ukatili dhidi ya watoto ambao umezinduliwa hivi karibuni, unaoainisha majukumu na wajibu wa kila mdau katika kukomesha ukatili dhidi ya watoto.

Wizara pia imekamilisha uanzishaji wa mtandao wa simu ya watoto, yaani *Child Helpline number 116* ambao utatumika na jamii wakiwemo watoto wenyewe kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lazima mtoto umfahamu, kwa namba hii unaweza ukaipiga unapoona mahali popote mtoto anafanyiwa ukatili. Atakuja kuchukuliwa na atasaidiwa na kama kuna kuchukuliwa hatua, yule ambaye anamhujumu mtoto au anamtesa mtoto naye pia atachukuliwa hatua.

Wizara kupitia mkakati wake wa mawasiliano utaongeza uelewa kwa wananchi kuhusu vitendo vya ukatili kwa watoto na athari zake kisaikolojia, kimwili na kijamii kwa njia ya vitini, vipeperushi, redio, runinga na vikundi vya utamaduni vya kijamii.

Aidha, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitatumika kama vituo vya kutolea elimu kuhusu jinsi ya kudhibiti vitendo vya ukatili kwa watoto. Wizara itaendelea kuhimiza Halmashauri za Wilaya na Manispaa kuendelea kuunda Kamati za Ulinzi na Watoto.

Kambi ya Upinzani na pia Mheshimiwa Khatib S. Haji Konde wanataka kujua kuhusu elimu ya watoto yatima. Wanasema watoto yatima wapate elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Wizara inashirikiana na Wizara ya Elimu, Afya na Ustawi wa Jamii TAMISEMI, pamoja na wadau wa maendeleo ya watoto katika kuwatambua watoto yatima ili kuwapatia haki ya elimu. Hii haki tayari ipo kwa sababu shule tunajua kwamba hakuna ada lakini wanakuwa wanakosa vifaa muhimu vya shule. Kwa hiyo, Kamati yetu imemua kulifikiria hili jambo jinsi ya kuwahudumia watoto hawa.

Hivi sasa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wamekuwa wakiweka orodha ya watoto yatima kwa nia ya kuwapatia huduma za elimu, chakula na mavazi kama inavyohitajika. Tayari yapo mashirika yasiyo ya Kiserikali yanawapa huduma watoto ambao wamekuwepo katika maeneo mbalimbali. Kupitia mpango wa kuhudumia watoto walio katika mazingira hatarishi, *NCPA 11* itaendelea kuwatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii kuwabaini watoto yatima na kuwapatia huduma stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rebecca Mngodo Mbunge wa Viti Maalum alitaka kujua Wizara inashiriki vipi katika kusaidia Viongozi wa Mabaraza ya Watoto? Hadi sasa kuna jumla ya Mabaraza 87 ambayo yanafanya kazi vizuri. Wizara katika kuongeza ushiriki wa watoto katika kuzungumzia masuala yao imekuwa ikiwezesha Viongozi wa Mabaraza ya Watoto kushiriki katika mikutano mbalimbali.

Kuhusu ajira kwa watoto, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo amezungumzia kuhusu kudhibiti ajira kwa watoto. Wizara imeandaa na kupitisha Sheria ya Mtoto namba 21 ambayo inaeleza kwamba kuajiri mtoto ni kosa la jinai. Hii ni Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inayozungumzia kinagaubaka kwamba kuajiri mtoto ni kosa. Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mkataba wa haki ya watoto ya Umoja wa Mataifa na ule wa Afrika ambao nchi imeridhia.

Hata hivyo, kuna kazi ambazo watoto wanaruhusiwa kufanya, kazi ambazo hazitawaathiri.

Mheshimiwa Mbunge, alikuwa anazungumzia kwamba mtoto anauza dukani; siyo vibaya kumweka mtoto dukani akaanza kujifunza zile *skills* za kuwa mfanyabiashara. Lakini awe na umri kuanzia miaka 13 na kuendelea mbele. Sheria inakataza mtoto kupewa kazi ambayo itamwathiri na ina madhara kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rebecca Mngodo ameshauri kwamba iwekwe sheria ya mimba za utotoni. Lakini kwa mujibu wa mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu haki na ustawi wa mtoto wa sheria namba 21 ya mwaka 2009, kumpa mimba mtoto na ndoa za utotoni ni moja ya vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu. Wizara imeendelea kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu haki na ustawi wa mtoto katika Kanda zote ili waelewe wajibu wa mikataba hiyo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu itahakikisha kwamba suala la kuwarudisha watoto shuleni baada ya kujifungua linatekelezeka.

Suala lingine ambalo aliuliza Mheshimiwa Mngodo ni kuhusu masuala ya UKIMWI. Wizara imekuwa ikifanya jitihada ya kuelimisha jamii kupitia mihadhara, redio, runinga na vipeperushi kuhusu athari za masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya *NGOs*, Kambi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine pia wameuliza kuwa kumezuka mashirika mengi yasiyo ya kiserikali pamoja na vituo vingi ambavyo vimesajiliwa kwa mgongo wa kuwasaidia watoto yatima. Hali halisi na tafiti zilizopo ni kwamba *NGOs* na vituo hivyo vinatumia mwanya huo kuepuka kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usajili wa mashirika yasiyo ya Kiserikali namba nne ya mwaka 2002 inayosimamiwa na Wizara yangu inayosimamiwa na Wizara yangu inasajili Asasi zisizo za kiserikali zikiwemo zile zinazomiliki vyuo vya kulelea watoto yatima. Aidha, vituo vya kulelea

watoto yatima kwa ujumla wake hupatiwa usajili na kuratibiwa kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa mujibu wa takwimu tulizonazo, Asasi zisizo za kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya kutoa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi, ni 202 na kati ya hizo 47 ndiyo zinazomiliki vituo vya kulelea watoto yatima. Asasi hizi hupatiwa usajili baada ya Wizara yangu kupata maoni kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine limeulizwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi na Kamati ya Bunge pia ilitaka kujua kwamba pamoja na ongezeko la mashirika yasiyo ya Kiserikali hadi kufikia 675 ni mashirika machache ambayo unaweza kuona mchango wake wa moja kwa moja katika kusaidia jamii katika Sekta ya Afya, Elimu, Mifugo, Kilimo na Mazingira. Pia baadhi ya mashirika haya yamekuwa yakijinufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa mashirika yanayosajiliwa chini ya Wizara yangu kupitia sheria niliyoitaja hapo juu, unaainisha kikamilifu kupitia uchambuzi wa taarifa za mwaka zinazowasilishwa na Asasi husika. Wizara yangu imeandaa mwongozo wenye maeneo muhimu unaowezesha kubaini mchango wa Asasi hizi. Maeneo haya ni pamoja na kujua mapato na matumizi ya Asasi, michango ya wahisani, michango ya ndani, mali zinazomilikiwa, pamoja na michango kutoka Serikalini.

Asasi zilizosajiliwa chini ya Wizara yangu zimesambaa katika Wilaya na Mikoa mbalimbali. Kwa mujibu wa takwimu tulizonazo ni kwamba zipo *NGOs* 868 katika ngazi ya Wilaya, na 559 katika ngazi ya Mikoa, 4085 ngazi ya Taifa na 222 za Kimataifa.

Mheshimiwa Fatuma Mikidadi alisema kwamba *NGOs* ziache kushabikia maandamano ya wanaharakati na kwamba baadhi ya *NGOs* mipango kazi yao ni kushambulia Serikali, waaswe. Mheshimiwa Mikidadi ni kweli hilo unalolisema na kwamba wanavunja sheria namba 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005. *NGOs* ni

Asasi za kujitolea zinazoanzishwa katika ngazi ya Wilaya na Mikoa, Taifa na Kimataifa kwa lengo la kusaidia jamii; hazigawani faida na wala siyo kwa ajili ya siasa. Ni kosa kubwa tunapoona kwamba kuna *NGO* inashabikia masuala ya kisiasa, tuna *website* yetu, ni vyema kama mkitoa taarifa ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Felix Mkosamali Mbunge wa Kibondo alisema kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali yanashindwa kutekeleza majukumu yake. Wizara yangu kupitia Bodi ya Taifa ya uratibu wa mashirika hayo imetoa matangazo kuzikumbusha Asasi hizi kutoa taarifa zao za kazi na fedha kwa mwaka. Ndiyo jinsi tunavyoweza kuwadhibiti, hii ikiwa ni hatua ya awali kisheria kabla ya Bodi haijatoa tamko la kuzifuta Asasi hizo, kwa sababu tuna uwezo wa kuzifuta. Takribani mwezi mmoja uliopita Wizara yangu ilitoa tangazo kuzitaka Asasi zote kuwasilisha taarifa zake za mwaka ili kuweza kubaini uhai wa Asasi hizo.

Waheshimiwa Wabunge, wale Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zenu ni wasajili wa Asasi hizi. Kwa hiyo, kwa haraka kabisa mnaweza kwenda kwa Maafisa Maendeleo wa Jamii, wao ndio wanatakiwa kujua shughuli wanazozifanya katika maeneo yenu. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kusubiri moja kwa moja kama inajulikana kama hii ni *NGO* na haifanyi vile inavyotakiwa, ni vyema ukienda kumfahamisha Afisa Maendeleo ya Jamii na taarifa tutazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine zito ambalo limezungumzwa sana ni kuhusu Benki ya Wanawake Tanzania. Upanuzi na huduma; Hili limezungumzwa na Kamati ya kudumu ya Maendeleo ya Jamii, Msemaji wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Rebecca, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Margareth Mkanga na Mheshimiwa Rajab Mbarouk.

Benki imeandaa mpango mkakati wa miaka mine. Mkakati huo umeainisha haja ya benki kujitanua na kuwafikia

wananchi wote wa Tanzania kwa kufungua matawi na vituo vya mikopo nchi nzima kwa awamu.

Waheshimiwa Wabunge, benki mpaka sasa imefanikiwa kuwa na vituo pamoja na *branch* mbili; Makao Makuu yapo Dar es Salaam, lakini pia tuna *branch* nyingine ambayo tunafungua pale *Aggrey Street* Dar es Salaam lakini kuna vituo Dodoma na Mwanza. Benki pia imetoa mikopo ya pikipiki kwa wafanyakazi wa Halmashauri ya Mwanga Mkoani Kilimanjaro, wafanyabiashara wadogo wadogo Mererani Mkoani Manyara na vilevile benki inatarajia kufungua vituo vya kutoa mikopo katika Mikoa ya Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafaniko ya benki ni kwamba hadi kufikia Machi 2013 benki imetoa mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali yenye thamani ya Sh. 12,149,873/=. Mikopo hiyo imewanufaisha wajarisiriamali 15,028 wakiwemo wanawake 11,931 sawa na 79% na wanaume 3,097 sawa na 21%. Hivyo ni dhahiri kuwa wanawake ndiyo wanufaika wakubwa wa mikopo hii ya Benki ya Wanawake, lakini pia na wanaume wamo. Lakini pia Benki ya Wanawake imeendelea kutoa mafunzo ya wiki tatu kwa wajasiriamali kabla ya kuwapatia mkopo. Mpaka Machi, 2013 wajasiriamali 10,200 walipatiwa mafunzo. Kati ya hao wanawake 9,000 sawa na 94% vilevile wapo wanaume 612 ambao ni 6% ambao nao pia wamepata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza mtaji wa benki, Serikali itaendelea kutoa kiasi cha Shilingi bilioni mbili kila mwaka kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2015 kama utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliyoitoa wakati wa maadhimisho ya siku ya wanawake iliyofanyika Kitaifa Tabora. Aidha, benki imedhamiria kutafuta mtaji kwa kuuza hisa katika soko la hisa baada ya kukamilisha taratibu za uuzaji wa hisa hizo. Mazungumzo ya uuzaji wa hisa yanaendelea kati ya benki na mamlaka ya soko la mitaji ili kuuza hisa kupitia dirisha la *Enterprise Growth Market* linaloratibiwa na soko la mitaji la Dar es Salaam yaani *Dar es Salaam Stock Exchange.*

Mfuko wa maendeleo ya wanawake kupatiwa fedha na Serikali, hili limesemwa kwa uchungu sana na Waheshimiwa Wabunge wengi. Ni kweli ni kipindi kimepita kidogo kabla hatujapata fedha. Tunaunga mkono ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii kuwa mfuko huu upatiwe fedha na Serikali kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2013/2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Halmashauri kuchangia 5% ya mapato yao katika mfuko wa maendeleo wa wanawake; Mheshimiwa Dkt. Lyatonga Mrema Mbunge wa Vunjo ameulizia hilo na Mheshimiwa Kuruthumu Mchuchuli pia amezungumzia hayo. Nakubaliana sana na Mheshimiwa Dkt. Mrema kuwa pamoja na Serikali kutoa agizo la Halmashauri kuchangia 5% ya mapato yao katika mfuko wa maendeleo ya wanawake, Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuzikumbusha Halmashauri husika kupitia barua na mikutano ya kisekta ya maendeleo ya jamii.

Hata hivyo, naendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa vile wao ni Wajumbe wa Kamati ya mkopo ngazi za Halmashauri, basi waendelee kuhimiza Halmashauri zao kuchangia mfuko huu ili wanawake wengi zaidi wapate mikopo kupitia mfuko huu. Sote tunakubali kwamba ukimwezesha mwanamke, umeiwezesha familia na hivyo umeliwezesha Taifa zima. Tunapokuwa katika mikutano yetu ya Halmashauri ni lazima tuhakikishe kwamba hili linatekelezwa yaani 5% ya makusanyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa sheria ya kuwabana wakopaji kurejesha fedha za mfuko wa maendeleo ya wanawake; hili limezungumzwa na Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga na Mheshimwa Moshi Kakoso Mbunge wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwafahamisha kuwa kila Halmashauri imewekewa utaratibu wa kufuatilia marejesho ya fedha za mfuko kutoka Halmashauri husika. Wizara yetu itaendelea kuzifuatilia Halmashauri kurejesha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo niliyoweza kujibu kwa sasa hivi. Lakini kabla sijamaliza, naomba nichukue nafasi hii kusema kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania na watoto wetu ni wasihi na kuziomba jamii tukatae na tukemee vurugu na uchochezi unaotokea mahali mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na amani tuliyonayo ndiyo maana sisi wanawake tunaweza tukafanya ujasiriamali, tukauza mama ntilie. Kunapokuwa na fujo mama ntilie hawezi kwenda kuuza mamantilie, lakini pia watoto wetu hawawezi kwenda shule na hivyo tutakaoathirika zaidi ni sisi akina Mama. *(Makofi)*

Wanawake wa Tanzania ni wanawake wanaopenda amani ndiyo maana katika fujofujo zote hizi humwoni mwanamke ndani, lakini ukimwona mwanamke katika fujo hizo ujue ana matatizo au kaingia kwa bahati mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia wanawake wenzangu penye fujo panatokea majeruhi ambao wanawake ndiyo tunawahudumia wakiwa hospitali. Penye fujo wanawake wenzangu panatokea vifo na sisi wanawake tunabakia na watoto, tunakuwa wajane na tunatakiwa tulee watoto wetu. Tuulizane, jamani kulikoni? Kwa sababu wanaofanya fujo ni watoto wetu sisi.

Kwa hiyo, nawaomba akina mama tuwe katika mstari wa mbele kabisa, yaani wanawake wote wa Tanzania, tuwashirikishe akina baba, najua akina baba pia hawapendi, lakini sisi ndiyo tunaowalea watoto zaidi. Basi tuwafundishe wachukie vurugu na Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wananchi ili waweze kujiendeleza kwa kupitia fursa mbalimbali ambazo zinawekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe wananchi wote na wanawake kwamba hizi fursa za maendeleo haziwezi kukupigia hodi, fursa unaifuata na kuitafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuwaomba tudumishe amani na upendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kif. 1001 - *Admin. & Human Resou. Mgt ..*Tsh. 1,280,841,769/=

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi nilipenda kufahamu, ni lini Serikali itakuja na Sheria ya kuanzisha Tume ya Taifa itakayosimamia masuala ya usawa wa jinsia, yaani *National Gender Equality Commission,* ili ifanye kazi ya ukaguzi wa kijinsia. Tume hii sasa ndiyo itakayoweza kusimamia, kutathmini na kuchunguza pale ubaguzi unapodhihirika. Tume kama hizi tayari zipo huko Kenya, Uganda na Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumeshuhudia sisi wenyewe michango mbalimbali ya Wajumbe waliochangia wakiwamo akina baba, naomba niwapongeze kwamba wametutendea haki. Lakini manung'uniko yote haya ya sisi wanawake yatatuliwa na Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii itakuwa kama Tume nyingine ambazo zipo kama Tume ya Haki za Binadamu na nyinginezo. Nilikuwa naomba tamko la Serikali kuhusiana na

uundwaji wa Tume hii, ili wanawake pia tuweze kutendewa haki katika baguzi mbalimbali.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kupata maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilipochangia Wizara hii niliomba kwamba fedha zilizotengwa ambazo zilikuwa zinakwenda kwenye Halmashauri, kwenye Mfuko wa Wanawake, sasa hivi zimehamishwa na ndiyo zinazopelekwa kwenye Benki ya Wanawake. Wote tunajua kwamba, kwa sababu Benki ya Wanawake ina bajeti finyu, haijaweza kufikia wanawake wengi na pia haijafikia Mikoa mingi. Fedha hizi wote tunaelewa zilikuwa zinakwenda kwenye Halmashauri na zilikuwa zinawezesha wanawake kupata mikopo, hasa waliopo maeneo ya vijijini; pia zilikiwa zinawezesha Halmashauri kuchangia asilimia tano (5%). Sasa hivi tunaelewa baada ya hizi fedha kutokwenda Halmashauri pia hazichangii, zinasema mbona zile fedha za kwanza haziji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kwamba Serikali itafute fedha mahali popote ili tuwatendee haki hawa wanawake na ili Halmashauri zote nchini ziendelee kupokea hizi fedha. Halmashauri nyingine tunajua ni changa na mapato yake ni madogo, hivyo hizi fedha zingeweza kusaidia vikundi vya wanawake vijijini. Hata kama ni utaratibu utawekwa kwamba wapate kupitia kwenye *SACCOS* zao na nini, lakini fedha ziende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na ninaelewa kabisa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inawajali wanawake na imefanya kazi kubwa na kweli ni kubwa na katika nchi nyingi ni ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litakuwa limewasaidia wanawake kupata mitaji. Nikaomba kwamba, zile fedha zikirudishwa kule, zitafutwe fedha kwa ajili ya Benki ya Wanawake ambazo zitawezesha kuifanya Benki hii kuwa na matawi ambayo yataweza kuwafikia wanawake wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapata jibu lolote. Naomba nipate jibu, na kama sitajibiwa vizuri, nina kusudia la kuondoa Shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia, nilihoji kuhusu *NGOs* hizi ambazo zimekuwa zinaanzishwa huku na kule hovyo hovyo na hatuzifuatilii. Sasa nataka majibu ya Wizara, kwanini isiweke mfumo wa kuanza kuzifuatilia *NGOs* ambazo zimekuwa zinaomba fedha nje, ikiwa ni pamoja na kuzifanyia *audit*, kuzikagua kwenye fedha ambazo wanapewa kama kweli zinakwenda kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko, watu wanalalamika kwamba *NGOs* zinazoshughulikia masuala ya Ukimwi, fedha zile haziwafikii walengwa. Sasa kwanini Serikali isiweke utaratibu wa kuzikagua hizi *NGOs* katika fedha ambazo zimekuwa zinaingia kwenye akaunti zao kama zinakidhi kweli malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikahoji kuhusu hizi *NGOs* kwamba kunakuwa na *NGOs* ambazo zinasajiliwa lakini hazifanyi majukumu yake, kwa nini Wizara isiwe inazifuta? Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba, tuwe tunaripoti kwenye Halmashauri zetu.

Mimi nilichosema ni kwamba, nataka iwe kama ilivyo kwenye Wizara ya Ujenzi, kwamba Wakandarasi huwa wanapewa Semina kufundishwa namna ya kuandika miradi na kadhalika. Nao pia wawe na utaratibu huo na zile *NGOs* ambazo zinaonekana hazieleweki ziwe zinafutwa badala ya kuwa na mlundikano wa *NGOs* na wengine wanafanya utapeli, wanaanzisha *NGOs* na kuombea fedha kutoka kwa wafadhili mara moja, halafu *NGO* inapotea. Wakipigiwa simu hawapatikani. Kwanini Serikali isije na utaratibu unaoeleweka kuhusu hizi *NGOs*? Naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua kwamba, Wizara hii mambo yake ni mtambuka na ilitakiwa kuwe na *proper*

*coordination* na Wizara nyingine zote kwa mambo yanayohusiana na Wizara hii. Lakini inaonekana wazi hali halisi sivyo ilivyo; hata jana tumeona kwenye Wizara ya Afya kwamba, uzazi salama bado ni matatizo na kadhalika. Hata katika mambo ya kilimo, akina mama ndio wazalishaji wakubwa huko vijijini, lakini pembejeo haziwafikii na licha ya uwezo wao mdogo, hatujaona namna Wizara hii inavyo-*coordinate* haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, hata hili suala ambalo Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri kuhusu hawa watoto wa Mitaani, lakini naomba ufafanuzi juu ya hiki kituo ambacho kitawekwa, kweli hawatarejeshwa kwa wazazi? Kitakuwa wapi? Je, ni kwa watoto wa Mji mmoja tu wa Dar es Salaam au kitahusu Tanzania nzima, kwa Miji yote ambayo watoto kama hawa wanaonekana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba tupate ufafanuzi, hii mipango ikoje? Kama itatuingia vichwani ndiyo tuweze kuikubali. Naomba ufafanuzi.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 23 ametueleza kwamba, katika mwaka wa fedha 2012/2013 zilitoka jumla ya Shilingi milioni 48 kwenda katika Halmashauri za Wilaya sita tu, ambazo walifanikiwa kurejesha mkopo kutoka kwenye Mfuko wa *WDF*. Lakini changamoto kubwa katika fedha hizi za *WDF* sio wajasiriamali, wanaopewa ni mtu mmoja mmoja, siyo kikundi, lakini pia fedha zinatolewa kwa itikadi za kisiasa. Mimi nina ushahidi. Ndiyo maana hazirejeshwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda mbali zaidi, ule utaratibu wa Mfuko wa Wanawake *(WDF)* katika kutoa hizi fedha, unakaba Maafisa Maendeleo katika kudai marejesho ya zile fedha kwa watu ambao wamekopeshwa.

Kwa mfano, wanashindwa kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria kwa sababu utaratibu wa mfuko hauruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo, kuna baadhi ya watu wanaomba fedha ziongezwe kwenye mfuko wa *WDF*, lakini kwa jinsi ambavyo unaendeshwa sasa hivi, hata kama utaongezewa fedha, fedha hizo zitakwenda kwa watu ambao sio wajasiriamali na ambao wanaweza kuziendeleza. Badala yake bado zitagawiwa kwa misingi ya kisiasa na wale ambao wana haki ya kuzipata watazikosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue, Wizara sasa inakuja na mkakati gani au inakusudia nini kubadilisha utaratibu wa ule mfuko ili hizi fedha hata kama zitakwenda katika Halmashauri zetu, basi zifike kwa walengwa na siyo kama sasa hivi ambapo zinakwenda kwa watu ambao siyo walengwa na ndiyo maana hazina tija. Je, Wizara inaniambia nini, utaratibu wa mfuko bado ni ule ule? Kama ni ule ule, hata fedha zikienda malengo ya mfuko hayafanikiwi. Je, wanabadilisha hizi taratibu za mfuko ili kuwafanya watu wanaokopa warudishe? Sheria ziwabane! Warudishe na wasifikiri fedha wanazopata ni za bure. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali itufahamishe hatua inazochukua kuhakikisha kwamba kunakuwa na *play grounds* za kutosha za watoto hasa kwenye Miji. Kwenye Miji mingi sana hivi sasa *play grounds* nyingi zimechukuliwa na watu, zimenyang'anywa na wengine wamejenga majumba, mabaa na mahoteli. Kwa hiyo, watoto wetu na hasa Mijini wanakosa mahali pa kwenda kucheza. Serikali inasema nini kuhusiana na suala hili na inachukua hatua gani kuhakikisha Miji yetu inakuwa na *play grounds* za watoto wetu?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba, bado suala la udhalilishwaji kwa wanawake na kwa mabinti zetu hasa kingono unaendelea, kama Waziri mwenyewe alivyozungumza katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea sasa wakati Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho angeeleza hatua ambazo Serikali inakusudia kuchukua kupambana na viashiria

ambavyo vinasababisha akina mama pamoja na watoto kudhalilishwa kijinsia hasa kwa upande wa ngono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kwamba, hivi sasa mabinti zetu na baadhi ya akina mama wanatembea uchi kabisa. Bado miaka michache sana ijayo nadhani watatembea uchi wa mnyama kabisa barabarani. Unakutana na binti amevaa kinguo kimemkamata mwili mzima, yaani kinatisha na maungo nyeti yako nje kabisa, kabisa, kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uhamasishaji wa ngono ambao unafanywa na akina mama wenyewe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kwenye majumba ya muziki, sijui inakuwaje! Wanaume wanavaa vizuri, lakini akina mama ni mpaka wavae vichupi, sijui ndiyo muziki unanoga; mimi sielewi! Nataka Waziri atuambie, hivi Wizara inalionaje jambo hili? Katika kusema hili, siingilii uhuru wa akina mama kuvaa, kwa sababu imefikia mahali sasa hivi watoto wanatoka nyumbani wamevaa vizuri, lakini kwenye mabegi yao wana nguo za uchi ambazo wanakwenda kubadilishia mbele ya safari. Je, hiyo ndiyo biashara au namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, hivi Wizara inajua kwamba kuna baadhi ya hoteli pale Dar es Salaam, kuna mziki unachezwa uchi wa mnyama kabisa, dada zetu wanachezeshwa uchi wa mnyama kabisa na wanapewa fedha kidogo? Huu ni udhalilishaji. Wizara inasemaje kuhusu mambo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilichangia juu ya mikopo hasa kwa makundi ya akina mama. Mara nyingi Serikali imekuwa ikitoa mikopo, lakini mikopo mingi imekuwa ikienda maeneo ya mijini. Je, akina mama wanaoishi vijijini,

ni kwanini mikopo hiyo haiwafikii? Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba na akina mama wanaoishi vijijini ambao ndio wengi wananufaika na mikopo hiyo ya Serikali? *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimechangia kwa maandishi na ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake cha hotuba kuanzia ukurusa wa 1- 46 sijaona hata neno moja la Chuo cha Maendeleo cha Malya. Je, chuo hiki amekifuta?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri unapojibu, utaje jina la aliyeuliza swali na kisha utoe jibu lake.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba sasa kuna umuhimu wa kuanzisha Tume ya Usawa wa Jinsia, yaani *Gender Equality Commission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba katika nchi kwa mfano za Kenya, *South Africa* na Uingereza, kuna sheria ambazo zimeanzisha Tume maalum za kushughulikia masuala ya jinsia. Umuhimu wa Tume hizi ni kama Wizara hapa kwetu, kwa sababu Wizara ni sehemu ya Serikali, lakini *at the same time* inatakiwa kupiga debe kuhusu haki na maendeleo ya wanawake. Kwa hiyo, tukianzisha Tume ni kweli unakuwa na chombo huru ambacho kinaweza sasa kikafanya kazi kwa ajili ya ku-*promote* haki za wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna Tume ya Utawala Bora na Haki za Binadamu. Kazi za Tume hii ni ku-*promote* haki za makundi yote; wanawake, watoto, vijana na kila mtu. Kwa hiyo, bado tunaweza tukatumia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, katika ku-*promote* masuala ya usawa wa kijinsia. Hata hivyo, kama Mheshimiwa

Mbunge anaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo basi tunaomba apendekeze Muswada maalum. Kulikuwa na chombo binafsi cha BAWATA – Baraza la Wanawake Tanzania, ambacho hakikuwa cha Serikali. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge alete pendekezo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni la Mheshimiwa Richard Ndassa, kwamba, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malya hakijatajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mheshimiwa Richard Ndassa kwamba, Wizara inakijali na kukithamini Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malya. Kwa mfano; mwaka wa fedha wa 2008/2009 Wizara ilitumia takribani Shilingi milioni 173 kwa ajili ya kukarabati chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la mwisho ni la Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa kwamba, jinsia ni masuala mtambuka lakini anaona kama hakuna *proper coordination* na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo chombo maalum, tunaita *Gender Focal Persons* ambacho tumekianzisha katika kila Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na katika Halmashauri. Kwa hiyo, Wizara ina-*coordinate* vikao vya wale Maafisa wa Madawati wa Jinsia katika kila Wizara.

Kwa hiyo, tuna *formal structure* ambayo tunaita *gender micro working group, micro policy*. Yaani hiyo sasa tunajadili kama unavyosema, kwa sababu Maendeleo ya Jamii hawezi kujua Kilimo anafanya nini, Maji anafanya nini, Elimu anafanya nini na kadhalika.

Kwa hiyo, *gender micro working group, micro policy* ambayo inahusisha pia wadau wa maendeleo, *NGOs* na *Gender focal persons* wa kutoka Wizara zote, ndiyo *the proper policy framework* ya kujadili masuala ya jinsia hasa *mainstreaming of gender equality.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, kuhusu fedha za *WDF* na fedha za Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana yeye pamoja na Waheshimiwa Wabunge karibu wote ambao wameona umuhimu wa kuendelea au kuufufua ule mfuko kwa kuupatia fedha. Mfuko ulikuwa unaendelea kutokana na faida ambayo tulikuwa tumeipata, ndiyo maana kuna mahali tumetoa Shilingi milioni 48 ambazo tulikuwanazo tu. Kwa hiyo, tunashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu kitu ambacho tutafanya, tunajua Kamati ya Maendeleo ya Jamii, imeshughulikia suala hili kikamilifu na tutaendelea kuongea na Serikali ili tuweze kupata fedha za Benki ya Wanawake na *WDF*. Benki ina umuhimu wake kwa sababu hizi fedha zikienda Benki zinatumika kwa kuongeza miundombinu. Fedha zile ambazo tumesema wanawake wamekopeshwa, ni *deposits* za wanawake wa Dar es Salaam, Pwani na sehemu nyingine ambazo wameweka, ndizo hizo zimekopeshwa. Lakini fedha ambazo Serikali inaipa Benki, zinakwenda kusaidia kuongeza matawi katika maeneo mengine. Kwa hiyo, bado tunahitaji fedha ziende Benki, lakini bado tunahitaji sana fedha za *WDF.* Kwa hiyo, tutaendelea kulifuatilia hili na kuiomba Serikali waweze kutupatia fedha kwa ajili ya *WDF* kwani tumeshakuwa na mazungumzo mengi kuhusu suala hilo. Nakushukuru sana Mheshimiwa tutaendelea kulifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyefuatilia alikuwa ni Mheshimiwa Mkosamali. Katika jibu langu nimesema kwa kupitia Bodi ya Taifa ya Uratibu Mashirika haya yote yanatakiwa yatoe taarifa zao za kazi na fedha wanazozipata kwa wakati. Ni kazi kubwa sana *NGO's* kwa sababu hata kupata taarifa zao kutoka kwa wale wanaowapatia fedha pia ni vigumu. *Donors* wengine ni wagumu, wana usiri kutuonyesha kwamba wamewapa fedha kiasi gani; wengine wanapeleka fedha kwenye *NGO's* za kisiasa. Kwa hiyo,

inakuwa vigumu sana kusema. Lakini sisi tunaendelea kuzifuatilia kwa njia hiyo kwa sababu ile Bodi ina kazi mojawapo ni hiyo ya kutathmini jinsi wanavyofanya kazi na hivyo tutajua. Lakini nasikitika kama kuna hizo wanazosema zipo lakini hazifanyi kazi, ndiyo maana nimekwambia kwa maeneo ya Kibondo au Kasulu kama zipo mahali pa kwanza kwenda ni kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii akwambie, maana yake yeye *NGO's* zikienda Wilayani zinatakiwa zifanye kazi na Afisa Maendeleo ya Jamii ndio anamkusanyia watu, ndio anafanya kazi naye. Kwa hiyo, itakuwa rahisi sana na sisi tutapata hizo habari kwamba kuna *NGO's* ambazo hazifanyi vile ambavyo zilikuwa zimeandikishwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli anasikitika sana kwamba zilitoka Shilingi milioni 48. Ningependa nimfahamishe kwamba hizi fedha sisi kwa upande wetu kwa sasa hivi tunafanya tathmini ya Mfuko huu. Lakini *so far,* Mfuko huu umefanya vizuri kwa sababu tuliwawekea *condition*; unapewa Shilingi milioni nne kila Halmashauri, sisi hatukuongezei mpaka urudishe zile Shilingi milioni nne tuzione, maana yake wale waliokopa wamezirudisha, basi tunakupa Shilingi milioni nane. Kwa mfumo huo tumeweza kuona akina nani hawajarudisha. Nii wachache sana ambao wameshindwa kurudisha kwa sababu motisha yake ni kwamba unaporudisha unapata fedha nyingi, unakopesha wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba unasema wanakopeshwa watu fulani fulani. Mheshimiwa Mbunge wewe ni Mjumbe katika ile Kamati ya kutoa ile mikopo. Naomba uwe mkali ili uhakikishe kwamba hizi fedha zinakwenda kwa walengwa. Tumeweka makusudi, kuna Madiwani wa Viti Maalum pale na kuna Mbunge ambaye anaingia katika ile Kamati ya Kugawa hizi fedha.

Mheshimiwa Zitto nakushukuru sana mwanangu kwa swali zuri sana la viwanja. Hili ni tatizo ambalo tumekuwa tukipata taabu nalo sana. Kila Mji unapopimwa vinapimwa viwanja vya watoto kwenye *master plan* zao. Kinachotokea ni Halmashauri zinazembea kuweka vifaa maalum vya

michezo kwa watoto. Sisi Wabunge wote hapa ni Madiwani, tuweke bajeti ya kuhakikisha maeneo haya yanawekewa bembea na michezo mbalimbali ya watoto. Lakini kwa sababu yanakaa bure, mwisho wake watu wanaanza kuweka vioski, wanaweka biashara zao, vingine vinakuwa vichaka tu. Kwa hiyo, kwa kupitia Bunge hili, naomba sana Waheshimiwa Wabunge watoto wetu tuwapende, wawe na maeneo ya kuchezea, lakini hawatayapata kama sisi hatutakuwa msitari wa kwanza kupanga bajeti katika Halmashauri zetu za kutengeneza viwanja hivi kwani viko chini ya hizo Halmashauri zdetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selasini anazungumzia udhalilishaji wa kingono hasa mabinti zetu wanatembea (hilo neno alilolisema mimi silijui), mimi nasema wanatembea utupu. Kwetu tunasema utupu, hatusemi kama ulivyosema wewe au kwa lugha nyingine wanatembea utupu na siku hizi watoto wa mjini wanasema wanavaa vichupi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kama jamii itachukia hivi vichupi na wao hawatovaa. Wanaume wengi zaidi ndio wanaohamasisha hivi vichupi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo! *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la jamii. Ni sisi jamii tunasema tunataka twende wapi, Serikali peke yake haiwezi. Si atavaa khanga kumbe ndani kavaa chupi, akienda anavua! Sisi watoto wetu wakitoka nyumbani wanatoka vizuri, hatujui huko wanakokwenda. Huko wanakokwenda wanawakuta akina baba. Mara nyingi katika maeneo hayo huwakuti akina mama. Kwa hiyo, nawaomba sana jamii ichukie haya mavazi yanayoitwa vichupi, wavae vizuri. Tunahitaji vijana wetu wavae kwa heshima.

Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja Mheshimiwa Sereweji amesema kwa uchungu sana kuhusu hizi nguo za utupu, kwa kweli hazistahili. Kwani unaonyesha nini cha

ajabu? Kwa hiyo, vijana wetu tuwaombe, tunajua huu ni wakati wa utandawazi, wanaangalia *fashion* kwenye mitandao kwenye TV na kadhalika kesho wanavaa mzazi humwoni. Mimi najua kwamba wazazi wengi kwa kweli hawapendi, lakini watoto huko wanavutiwa na wale ambao wana-*encourage* mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye muziki, kwamba kwa nini mtoto wa kike avae kichupi, mtoto wa kiume amevaa vizuri? Hata wanaume mnaonyesha *underwear* zenu, mnavaa katakei. Zile katakei, pia ni utovu wa nidhamu kwa wanaume, maana yake nguo ya ndani haitakiwi kuonekana. Wanavaa hicho kitu sijui katakei wanasema, haitakiwi pia. Kwa hiyo, tukataze vichupi na hizo nyingine ambazo mnakata sehemu fulani hivi; hiyo kei hiyo! Kwa hiyo, naomba jamii tushirikiane kwa pamoja tumalize hili tatizo. Huko nyuma sana lilitokea, lilimalizwa. Hata sasa tukilichukia litapotea. Kwa hiyo, Serikali inaweza kufanya mambo mengi. Hili nalo mnataka tulitungie sheria, kwamba nguo nazo tuzitungie sheria? Wakati huo umepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimeyamaliza.

**MWENYEKITI:** Bado Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli na Mheshimiwa Selasini kwamba kuna baadhi ya watoto wanacheza utupu sijui!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA WANAWAKE, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Mbunge amezungumzia hoteli wanazocheza utupu, ndiyo yote hayohayo! Tusiende, tuzisuse hizo hoteli. Kwa nini unakwenda hoteli ukatazame utupu

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kwa kweli hatuna taarifa ya hoteli hizi za utupu. Zamani nilikuwa najua Ulaya

kuna kitu kinaitwa *Stricties*, sasa kama na hapa zipo, sijui zinapata leseni kutoka wapi. Lakini nina hakika nchi yetu haitoi leseni kwenye hoteli kama hizo.

Kwa hiyo, kwa sababu sisi Wabunge tuna uwezo wa kutoa ripoti na hiyo hoteli iko katika eneo lenye Watendaji wa Kata, lina Serikali yake likatoe ripoti kwamba hapa kuna mambo ya utupu utupu yanaendelea.

Mheshimiwa Kakoso anazungumzia kuhusu mikopo kwamba inakwenda mijini. Kwa mikopo ya *WDF* ambayo inatolewa Serikalini haichagui, inakwenda kwa Wilaya zote. Nadhani kule Wilaya yako ni mpya, inawezekana haijapata. Ndiyo maana tunahangaika tupate fedha zaidi na zile Wilaya mpya tufikiwe. Lakini kila Wilaya ilipata na kama hawakupata mwaka 2012 na mwaka 2011 ni kwamba hawajarudisha zile tulizowapa mwanzo. Hatutoi mkopo kama hatujaona marejesho. Mikopo hii ilikuwa hasa kwanza ni chachu ya kuwafundisha wanawake kujua kukopa na kurudisha. Kwa hiyo, ni lazima tujue kwamba zimerudishwa, baadaye wale waliokopa mwanzo hawakopi tena, watakopa wengine na hawa wengine watakwenda kwenye Benki za kawaida.

**MWENYEKITI:** Bado swali la Mheshimiwa Kuruthum.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Kuruthum nimeshamjibu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaridhika na majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto lakini hukutoa hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Ndiyo natoa hoja ya kuondoa Shilingi sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Huwezi kutoa hoja mara ya pili.

Mheshimiwa Zitto huwezi kusimama mara mbili na Mheshimiwa Selasini huwezi kusimama mara mbili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mng'ong'o ulijibiwa na akasema analifanyia kazi, anahakikisha atalishughulikia. Kama umetoa Shilingi unataka tukuhoji sasa, unabakisha?

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika naomba niendelee kutoa hoja yangu, ninajua kabisa kwamba nimejibiwa na Waziri. Lakini tunaelewa kwamba fedha hizi zikitolewa zitagusa Halmashauri nyingi na wanawake wengi wa Vijijini na tunaelewa kwamba, na mimi nakiri hizi fedha zilikuwa hazichagui Chama, walikuwa wanapewa wanawake wote, zilikuwa hazina itikadi na kila mwanamke alikuwa anapewa ili mradi yuko kwenye kikundi. Hazikujali itikadi ya mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, napenda Serikali iniambie hizo fedha Shilingi bilioni mbili zinahamishwa zinarudi kwenye ule mfuko na fedha nyingine zinatafutwa kuweka kwenye Benki ya Wanawake? Ndiyo hoja yangu. Kama hiyo haipo, nitatoa Shilingi na tujadili. Nipewe jibu, hiyo fedha inapatikana? Ndiyo nataka niambiwe, kama haipatikani natoa Shilingi. Naomba tujadili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuna yoyote mwingine anataka kuchangia?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mng'ong'o anaeleza hoja ya msingi kuhusu fedha hizi kuongezwa kwenye Benki ya akina mama. Kama walivyoeleza akina mama ni asilimia 51, kwa hiyo, mimi namuunga mkono hoja yake. Hata kama zinabaki hizi Shilingi bilioni mbili, watuambie zinakwenda kwa akina mama wa maeneo gani ya nchi hii? Tunataka fedha hizi kama hamwongezi fedha kutoka hizi Shilingi bilioni mbili mlizotenga, fedha hizi ziende kwa akina mama wa Vijijini, maana ndio wenye matatizo makubwa kuliko akina mama wa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja yake, waende wakatafute fedha waiongezee hii Benki kwenda kupeleka fedha hizi vijijini kwa akina mama ikiwemo na kule Kibondo waweze kupata fedha kutoka kwenye Benki

hii ya akina mama. Hizi Shilingi bilioni mbili hazitoshi kabisa kwa akina mama asilimia 51 wa nchi hii.

**MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kuchangia katika hili kwa sababu naungana na Mheshimiwa Mkosamali kwa maana ya Mheshimiwa Kakoso waliokuwa wakiulizia suala la Maendeleo kwa Wanawake Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa kweli Serikali itueleze hizo fedha inazitoa ama haizitoi. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mng'ong'o.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati yetu tumehoji sana Wizara hii na kuanzia mwaka 2005/2006 fedha kwenye Mfuko wa akina mama hazijawahi kupelekwa. Nasi hatukuridhika kwa sababu sasa hivi fursa za akina mama kupata fedha kwenye ngazi za Halmashauri sasa hawapati. Kwa hiyo, ni jukumu letu Wabunge wote tuone kwamba Serikali ina haja ya kurudisha na kutunisha Mfuko huo wa akina mama. Sasa hivi wanatumia kigezo cha Shilingi bilioni mbili zinazopelekwa kwenye Benki ya Wanawake ambayo ni kitu tofauti kabisa na ule Mfuko. Kwa hiyo, Kamati inasisitiza kwamba Serikali irudishe ule Mfuko na ile *Vote* wameshaifuta. Tunaomba nayo iweze kurudishwa ili fedha ziweze kuwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, fedha ziweze kutafutwa. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kimsingi hili suala hapa tunalozungumza inapaswa limguse kila mtu. Akina mama hawa hawana vitu vinavyoweza kuwafanya wakakopesheka kwenye Benki yoyote. Huu Mfuko ndiyo njia pekee waliyokuwanayo ya kuweza kupata fedha angalau kwa urahisi wakaanzisha shughuli zao ndogo ndogo. Benki hii ya Wanawake iko Dar es Salaam. Labda kama Serikali mnatuambia kwamba akina

mama wa Dar es Salaam pekee katika nchi hii ndio wenye haki ya kupata fursa ya fedha. Vinginevyo, ni lazima fedha itafutwe ili Halmashauri zote ziweze kupata. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Huu ni ukweli ambao uko dhahiri kabisa. Kwa mfano, akina mama walio wengi wako Vijijini na ndio wana shida kuliko sehemu za Mijini.

Ukiangalia kijiografia fedha hizi kuwekwa katika Benki ya akina mama haisaidii akina mama kwa adha kubwa waliyonayo. Turejee, Baba wa Taifa alivyoandika kwenye kitabu cha Ujamaa. Ukilinganisha akina baba wale wa vijijini wanafanya kazi lakini hawalingani na wale wa Mijini. Lakini akina mama wa vijijini ndio wazalishaji wakubwa na takwimu zinaonyesha, akina mama hawa wakipewa misaada kupitia fedha hizi kwenye Halmashauri wanarejesha kwa sababu wanafahamika, wanafuatiliwa wanajulikana wako wapi. Kwa hiyo, siyo rahisi wakapotea kama maeneo mengine yalivyo. Benki hii ya Wanawake ili itafika lini maeneo ya vijijini ikiwemo kule Serengeti, Machochwe, Masinki, ukienda Nata, Ikoma itafika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ziende katika Halmashauri. Uzoefu unaonyesha kwamba siku za nyuma walikuwa wanafanya vizuri. Kwa hiyo, hata *Vote* hiyo ambayo imeshafutika ni kuwanyanyasa akina mama. Mbona akina mama hawa wakati wa harakati za kutafuta kura ndio wanawekwa msitari wa mbele? Kwa nini wasisaidiwe katika mazingira haya ambayo yatasaidia katika ujasiriamali na shughuli nyingine? Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mng'ong'o. *(Makofi)*

**KAIMU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI – MHE. SAMUEL J. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ina kawaida ya kuwasikiliza sana Waheshimiwa Wabunge wanapotoa hoja. Hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wote katika hatua hii kwa uzito

mkubwa sana. Nikiwa ni Kiongozi wa Shughuli hizi kwa sasa, naliona ni jambo ambalo linafaa kutazamwa. Bahati mbaya tu utaratibu hauruhusu sasa hivi tukaweza kuhamisha fedha kwenda kwenye kifungu kingine. Tutashauriana na Mwanasheria Mkuu hapa ambaye nilianza kusema naye na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu atakayerudi hapo kesho, halafu tutafanya uamuzi mmoja kati ya maamuzi mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimoja tunachoweza kufanya ni kuweza kulitekeleza hilo katika mwaka wa fedha huu. Lakini hilo naliona gumu kwa sababu bajeti ya Benki ya Wanawake tayari nayo imekwishapita katika vikao vyake na walikuwa wakizitazamia fedha hizi. Kwa hiyo, la pili tunaloweza kufanya ni kuhakikisha tunapoanza mpango mpya wa fedha kwa bajeti ya mwaka 2014/2015, basi mwezi Novemba tunapokuwa hapa Dodoma, tulijadili, tuweze kuhamisha sasa kuanzia kipindi hicho ili bajeti hiyo iweze kuzingatia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa Wabunge ambao wamechangia hoja yangu akiwemo Dkt. Kamani, Dkt. Kikwembe, Dkt. Kebwe na Wajumbe wote ambao wamechangia wakiwemo Wajumbe wa Kamati, kwa sababu Dkt. Obama Ntabaliba alikuwa anawakilisha Kamati kama Makamu Mwenyekiti na ambaye leo amesoma, pia Mheshimiwa Mkosamali na mwishoni mchango nilioupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema toka mwanzo kwamba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inajali sana Wanawake na mpaka imetufikisha hapa tulipo toka mwanzo niliposema. Hoja yangu siyo kwamba Benki ya Wanawake inyang'anywe fedha, hoja yangu siyo hiyo. Hoja yangu ni kwamba fedha zilizokuwa zinakwenda kwenye Mfuko wa Wanawake ziende Shilingi bilioni mbili, fedha za Benki ya Wanawake ziongezwe, ndiyo hoja yangu.

Hoja yangu ni kwamba fedha zote tunazitaka, kwa sababu wanawake wote hawawezi kupata mkopo kwenye fedha hizo za Mfuko. Wanawake wengine watapata fedha kutoka kwenye Benki ya Wanawake na imefanya kazi nzuri. Lakini wanawake wengi walioko vijijini ambao hawakidhi vigezo, wataendelea kupata fedha kutoka kwenye huo Mfuko na Halmashauri zetu zitaendelea kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Benki hizo haiwezi kufika haraka Mikoani, kwa hiyo, wachache watakwenda kupata na wengine watapata huku na wanawake wote tutakuwa tumefikiwa na pamoja na Taasisi nyingine ambazo zinatoa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna Kamati ya Bajeti na Serikali yangu hii najua ni sikivu, najua Serikali yangu ni sikivu, hili wameliona na wameona kwamba linatugusa kila mtu. Mimi nairudisha Shilingi, lakini naomba hizo fedha zikatafutwe kwenye Bajeti hii. Ndiyo hoja ambayo ninayo na naomba hizi fedha zisije mwaka ujao, ni mwaka huu huu fedha hizi zitafutwe mwaka huu huu wa fedha. Kama tumeweza kutafuta fedha za Wizara nyingine, tunapata kigugumizi gani kutafuta fedha za wanawake ambao ndio wanaohangaika kila siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanahangaika katika shida na kama Wajumbe wenzangu walivyosema, wanawake ndio washirika wakubwa katika kupiga kura na kutuingiza humu ndani pamoja na kutafuta kura kwa vyama vyote. Naomba hizo fedha zipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha hoja yangu, najua kwamba Kamati ya Bajeti ipo, imo humu inasikia; Serikali yangu pale imesikiliza; Kiongozi yuko pale ametoa maoni yake na ni mazuri, nakubaliana nayo, lakini naomba isiwe mwakani. Tunazitaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi najua kwamba itatafuta. Ahsante sana na Shilingi

nairudisha, lakini fedha hizi zipatikane Bajeti hii na Benki iendelee kufanya kazi zake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mng'ong'o na hakika umesimama kidete kutetea haki za wanawake. Nakushukuru sana.

Nakushukuru vile vile Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu kwa *intervesions* zako na kutoa busara zako na kufikisha kifungu hiki kiweze kupita.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ..................Shs 495,829,200/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* .......................Shs 296,412,200/=
Kif. 1004 - *Internal Auditor* ................................Shs 128,204,200/=
Kif. 1005 - *Gov Communication Unit* ............Shs 90,868,300/=
Kif. 1006 - *Procurement Manaement Unit* ....Shs 123,741,800/=
Kif. 1007 - *Info, Communication and Tech*.....Shs 81,116,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Training and Folk Dev. Colleg*... Shs 6,004,139,200/=

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti niko kwenye *Item 221400 - Hospitality Supplies and Services.* Mwaka kifungu hiki mwaka 2012 kifungu hiki kilipangiwa jumla Shilingi milioni 19. Lakini sasa ni Sh. 1,114,000,000. Haya ni masuala ya vinywaji tu na mambo mengine. Kwa nini fedha hii inaongezeka nyingi kama hivi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezeka mwaka huu kwa sababu ni kwa ajili ya kulipia chakula kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 55 vyote na ni kwa mujibu wa taratibu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwamba kila mwanafunzi atakayefanya

masomo ya Sekondari au ya Elimu ya Ufundi, anatakiwa kutumia Sh. 2,500/= kwa siku.

Kwa hiyo, hizi hela ndiyo katika ile kuthibitisha kwamba Serikali ina dhamira ya dhati ya kuboresha vyuo. Ndiyo maana imeamua kuzifunga hizi hela Shilingi bilioni 1.1 kwa ajili tu ya chakula cha wanafunzi ili wanafunzi wetu waweze kuwa *attracted* katika kujiunga na Vyuo vyetu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Community Development* ……. Shs 3,593,908,321/=
Kif. 2003 - *Comm. Dev. College Tengeru*... Shs1,042,080,000/=
Kif. 3001 - *Gender Development* ………….Shs 351,603,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Children Development* ………….Shs 322,018,000/=

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki ndicho ambacho kimetenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya watoto. Nchi yetu asilimia 50 ya watu wote wa nchi hii ni watoto ambao wako chini ya umri wa miaka 15. Lakini fedha ambazo zimetengwa hapa ni Shilingi milioni 322 tu katika Bajeti ya zaidi ya Shilingi trilioni 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri anifahamishe katika hizi fedha, haya mafungu yote hapa ya hii *Sub-Vote 3002* iko wapi fedha ya kupita kukagua viwanja vya watoto ambavyo vipo kwenye *Master Plan* ya Miji yote, lakini vimeporwa na watu wachache? Fedha ziko wapi hapa kwenda kukagua? Kwa sababu ni jukumu la Wizara kuhakikisha kwamba hivi viwanja vinakuwepo na haviporwi!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mwenyekiti fedha zinazoonekana hapa ni za uendeshaji wa Ofisi. Kutokana na ufinyu wa Bajeti hizi ndiyo tulizoweza

kupanga. Lakini fedha nyingine za masuala yanayohusu maendeleo ya mtoto zipo kwenye *Development. (Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – Non-*government org*.................... Shs 243,735,800/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kif. 1001 - A*dmn & Human Resou. Mgt*........ Shs 400,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Train. and Folk Dev Colleges*.... Shs 6,400,000,000/=

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naongelea kifungu 2001 kasma 6329. Wizara katika bajeti yake ya mwaka 2011/2012 walitenga Shilingi milioni 394 ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Sofi, lakini mpaka leo hakuna kinachofanyika pale.

Swali langu ni kwamba, katika Shilingi bilioni mbili hizi za mwaka huu: Je, nazo zimo kwa ajili ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Sofi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Chuo cha Sofi kimo kwenye mpango mkubwa kabisa wa kuboresha hivi vyuo ili vifundishe mafunzo ya *VETA*.

Kwa hiyo, chuo kile kitapata karakana na pia walimu wake wameshakwenda kupata mafunzo yanayotolewa katika chuo cha *VETA*.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilisema Chuo cha Maendeleo cha Kibondo kina miaka kumi, tangu mwaka 2003 hakijawahi kupata hata Shilingi moja ya fedha za maendeleo. Sasa imeongezeka hapa Shilingi bilioni 1.5.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anaiambie, Kibondo watapata hata Shilingi moja? Kwa sababu wana zaidi ya miaka kumi wanaondoka kavukavu. Atuambie Kibondo tutapata hata kitu kidogo hapa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie kwamba Mheshimiwa Mkosamali kwamba kwanza Vyuo vyote 55 vya Maendeleo ya Wananchi vitafanyiwa maboresho kutokana na ile *support* tuliyoipata kwa ajili ya *education sector development programme.* Lakini katika mafunzo yale ya *VETA* awamu ya kwanza tumeanza na Vyuo 25. Lakini Mheshimiwa Mkosamali nikuthibitishie kwamba awamu ya pili Kibondo kiko katika mpango wa kufanyiwa marekebisho na maboresho ili sasa tuanze kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana wa kibondo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Community Development* ............Shs 100,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - *Comm. Dev. College Tengeru* .............Shs 0/=
Kif. 3001 - *Gender Development* .............Shs 2,546,062,000/=

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nina swali hapo kwenye *sub vote 2003* - Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Tunatambua kwamba chuo hiki ni kikongwe na kinadahili wanafunzi mbalimbali ili tuweze kupata Maafisa

Maendeleo wa Jamii wengi iwezekanavyo. Lakini hakuna fedha zozote zilizotengwa za maendeleo katika Chuo hiki. Naomba nipate maelezo kwanini hakuna fedha zilizotengwa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Tengeru ni kweli hapa inaonyesha hakuna pesa za maendeleo, lakini chuo hiki sasa hivi kiko kwenye mpango wa *retention*.

Kwa hiyo, kinatumia fedha zinazopatikana kutoka kwenye ada na fedha hizi tunauhakikanazo kwa sababu wanapata mikopo kutoka Serikalini. Lakini pia kuna marekebisho ya Vyuo, kinachotoa shahada ni Tengeru na siyo Rungemba.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Children Development* ............ Shs 464,610,000/=

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ile ile ya viwanja vya watoto kuchezea katika Miji. Waziri alisema kwamba fedha zipo kwenye maendeleo na *sub vote* na 3002 nimeangalia *item* zote hakuna hiyo fedha. Naomba Mheshimiwa Waziri atutolee ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika fedha hizi, tunazo fedha za ufuatiliaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008. Katika ufuatiliaji huo katika ile sera, pia tunazungumza kuwepo kwa viwanja vya watoto. Lakini sisi siyo wajengaji, sisi ni wahamasishaji. Halmashauri zifanye kazi yake ya kutengeneza hivyo viwanja vya kuchezea watoto. Nakushukuru kwa kupitia wewe Halmashauri huko wamesikia. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, ningependa Mheshimiwa Waziri aniambie umakini wa Wizara au Serikali katika kujali maendeleo ya

watoto kwa sababu inaelekea kwa miaka mitatu mfululizo sasa 2011/2012, 2012/2013 na sasa 2013/2014 fedha yote iliyoko hapa ni fedha tunayotarajia kutoka nje.

Sasa hawa watoto kama ni watoto wa Watanzania hatutengi hata senti kumi angalau kuonyesha kwamba tulikuwa na nia lakini tumeshindwa. Sasa hapa tunaondoka na mategemeo gani kwamba kweli hizi shughuli zilizopangwa hapa zitaweza kufanyika?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za maendeleo kwa watoto kwamba Serikali haikutenga; kwanza ni kutokana na ufinyu wa bajeti imetufikisha hapo. Lakini *UNICEF* ni wafadhili wazuri tunafanya nao kazi kwa karibu sana na karibu miradi yetu yote hata ufuatiliaji wa masuala ya watoto mengi tumefanya bega kwa bega.

Kwa hiyo, tuna uhakika wa kupata fedha hizi. Lakini pindi fedha za ndani zikitosheleza, basi zitawekwa kwenye bajeti ya watoto.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilikuwa nasimamia *sub vote* 3002, kasma 5414. Unakuta kwamba hawa wafadhili pamoja na kutoa hizo fedha, lakini mwaka huu wamepunguza sana kutokana Shilingi milioni 61 za mwaka uliobita mpaka Shilingi milioni 46.5 na wakati huu nchi yetu matatizo ya watoto bado yanaendelea na yanaongezeka. Lakini cha kukazia zaidi, hela ya ndani hakuna hata senti tano. Sasa tunamjali motto? Si tunadanganyana jamani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ndizo tulizopata kutoka kwa wafadhili na sisi kwa upande wetu kama nilivyosema, kuna ufinyu wa bajeti, lakini kwa yale ambayo *UNICEF* wameona wanaweza kutusaidia kwa upande wa watoto ni hayo, na mengi ni katika kuandaa mfumo wa ulinzi wa mtoto na utekelezaji hasa wa ile *Child Helpline* kuifanya ifanye kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirejea)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2013/2014 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nawashukuru na kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa umahiri wenu, mmefanya kazi kubwa sana na mmeonyesha kwa kweli mnafaa na ni timu na mwende nayo vizuri.

Sasa kuna tangazo hapa la Semina kwa Wabunge wote. Naomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa kutakuwa na Semina kuhusu Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* Jumapili tarehe 12 Mei, 2013 saa 4.00 asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, sasa naomba kuliahirisha Bunge mpaka hapo Siku ya Jumatatu Saa tatu Asubuhi.

*(Saa 1.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 13 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*